31 MEI, 2013

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Thelathini na Tisa - Tarehe 31 Mei, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo ni Kikao cha Thelathini na Tisa Mkutano wa Kumi na Moja. Katibu!

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatayo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na maswali, naomba niwajulishe tu kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko safari, lakini kwenye kiti pale anayekaimu kwa shughuli za Serikali Bungeni ni Mheshimiwa Samuel J. Sitta. *(Makofi)*

Na. 312

### Kutenga Makazi kwa ajili ya Jamii ya Waadzabe

**MHE. NEEMA M. HAMID** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kutenga makazi kwa ajili ya Wahadzabe ambao hujishughulisha na urinaji wa asali na kukusanya matunda ili jamii hii pamoja na mila zao isipotee?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimwa Neema Mgaya, Mbunge nwa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamii ya Wahadzabe ambayo iko katika kundi Kihistoria la Khoisan inapatikana katika Bonde la Ufa la Kaskazini mwa Tanzania hususan Wilaya ya Mbulu, Karatu, Iramba na Meatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya jitihada mbalimbali katika kuhakikisha kuwa Jamii hii haipotei na pia inapata huduma muhimu za kijamii kama zilivyo jamii nyingine katika nchi yetu. Nia ya Serikali ni kuibadilisha jamii hii kwa kuiwezesha kupata mahitaji na huduma muhimu za kijamii bila kuathiri tamaduni zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga maeneo ya makazi ya Wahadzabe, na kupeleka huduma za jamii kama elimu, maji na afya. Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, jamii ya Wahadzabe wametengewa maeneo katika Vijiji vya Dumanga na Mongo wa Mono, na kujenga shule za Msingi katika vijiji vya Yaeda Chini (Shule za Bweni), na Endagulda na Sekondari moja katika kijiji cha Yaeda Chini.

Pia imechimba visima vya maji katika vitongoji vitatu vya vijiji hivyo na kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na inakusudiwa kupeleka miradi mingine mikubwa, ikiwemo ya maji ya bomba katika vijiji vya Yaeda na Mongo wa Mono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua Utamaduni wa jamii hii, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na Hanang kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wameweka mikakati ya kuhifadhi utamaduni wa jamii hizi za kihistoria katika kituo cha utamaduni cha Haydom-Mbulu. Aidha bila kuathiri utamaduni wa jamii hii, Serikali imelenga kuwabadilisha kabila la Wahadzabe kuwa wakulima na wafugaji bora wa nyuki ili kujitosheleza kwa chakula.

Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba jamii hii imepatiwa mafunzo ya kilimo cha Mhogo na ufugaji wa Nyuki kwa kupatiwa Mizinga 123.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa n aswali moja tu dogo la nyongeza, nilikuwa ntataka kujua, pamoja na yote haya Serikali iliyofanya. Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba vijana wa Kihadzabe wanapata fursa ya kupata mikopo kama wanavyopata vijana wengine ili kuweza kuendeleza biashara zao za kurina asali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nimpongeze Mheshimiwa Neema Mgaya kwa jitihada zake hizi za kuiona hii jamii kwamba nayo inaendelezwa kama vile tunavyowaendeleza Watanzania wengine bila kuwabagua, lakini wakati huo huo tukiendelea kuhakikisha kwamba tuna hifadhi tamaduni zao ili zisije zikapotea kama nilivyoeleza hapa.

Sasa kuhusu hili suala la kwamba hao vijana walioko katika hizi Halmashauri wanasaidiwa, hatuwaondoi katika mfumo mzima wa Halmashauri, katika Halmashauri tiunatenga asilimi atano kwa ajili ya vijana, na tunatenga asilimia tano kwa ajili ya akina mama.

Kwa hiyo, hatuwaodoi katika huo mfumo, lakini pia anavyosema Mheshimiwa Mgaya hapa, ni kwamba upeleke focus maalum kwa sababu hili ni kundi ambalo kidogo kama vile limeachwa nyuma ya mfumo, ili tuweze kulisaidia.

Kwa hiyo, tutakwenda kuangalia sasa kwa kiasi gani hao nao tunaweza tukawa-*consider*, lakini tukitumia mfumo huu hu wa Halmashauri, na ndiyo maana nimesema hapa kwamba kumekuwa kuna taratibu za kuona kwamba wanapata hata hiyo mizinga, wanapata shughuli nyingine za kilimo bora na cha kisasa ili waweze kuondoka katika hali ile ya umasikini. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina swali dogo tu la nyongeza, kwanza nikubaliane na Serikali kabisa kwamba ilifanya kazi kubwa sana ya kuwaandalia mazingira hawa ndugu zetu Wahadazabe, pia kuna kabila lingine la Watindiga ambalo linafanana kabisa na la Wahadzabe, ambalo pia najua Serikali ilifanya juhudi ya kuwajengea shule pamoja na hospitali, mfano mzuri ni katika Mkoa wa Singida, Iramba kule maporini kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa habari ambazo ninazo na kwa uhakika amabao ninao ni kwamba, zile shule ambazo zilijengwa na Serikali pamoja na Kanisa, wale Wahadzabe na Watindiga walizikimbia, na wameendelea kuingia porini kuishi porini. Kwa hiyo, watoto wale wa Wahdzabe hawana nafasi tena ya kwenda shuleni.

Je, Serikali iko tayari sasa kwenda kufanya utafiti wa kina, hususan Mkoa wa Singida kuangalia ni kwa namna gani inaweza kushawishi hiyo jamii ya Watindiga na Wahadzabe ili waweze kurudi katika maeneo ambayo walitengewa na Serikali na kuwasomesha watoto wao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Christowaja, hivi kumbe Wahadzabe na Watindiga ni kabila mbili tofauti.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimwa Christowaja G. Mtinda, kama ifuatavyo:-

Anachosema Mheshimiwa Christowaja ni kweli, wakati tulipokuwa tunatafuta haya majibu, ilionekana *once upon a time*, wakati wa Mwalimu, kuna hata na nyumba ambazo zilikuwa zimeandaliwa kwa ajili ya haya makundi ambayo yanazungumzwa hapa, na ambazo zinaonekana kwamba ziliachwa hivi hivi, haziendelei kutumika, na tunaiona hii kama ni sehemu ya changamoto, lakini pia wakati unapoangalai masuala ya udamaduni ni lazima uwe mwangalifu sana, uweze kwenda nao kwa taratibu, *gradually* ili kutokuathiri sasa hizo tamaduni zao, lakini wakati huohuo ukihakikisha kwamba wanaingizwa katika mfumo huo wa kisasa wa teknoloji na *high take.* Tungekwenda kwa mwendo huu tunaokwenda tusingeweza kusafiri kwenda mpaka Uchina, kwa sababu kusingekuweko na Ndege, tungekuwa tuna kaa tu tunawinda na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho tutakifanya hapa ni kwamba, tutaziagiza hizi kwa maana ya haya mazungumzo yanayokuja hapa. Tutaziagiza Halmashauri zetu, tufuatilie kwa karibu, madarasa yael yamejengwa kule, n ashule zimejengwa kule, tumejenga nyumba kule, sasa tungetaka kuona haya makundi kidogo kidogo tinawapeleka kwa namna ambayo wanaelimishwa, ili waweze kuiona *a one to one function* kati ya hiyo *development* na maisha yao. *Otherwise* watabaki tu wa kuokota matunda na kuwinda huko msituni, kitu ambacho nadhani si *target* yetu sisi kama taifa. (*Makofi*)

Na. 313

**Kufufua Barabara ya Mjerumani**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA (K.n.y. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** aliuliza:-

Barabara ya zamani ya Mjerumani itokayo kijiji cha Isanga - Wilaya ya Mbozi–Kijiji cha Kisanga - Wilaya mpya ya Kalambo ni fupi kuliko zote kuunganisha Mkoa wa Rukwa na Mbeya, Kigoma, Katavi, Tabora na nchi jirani za Zambia, Burundi na *Congo DRC.*

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuifufua barabara hiyo kulingana na umuhimu wake kiuchumi hasa ikizingatiwa kuwa kukosekana kwa daraja la mto Kalambo ndiyo kikwazo kikubwa cha kutokamilika kwa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mjerumani inaanzia Mkao wa Mbeya katika kijiji cha Isanga hadi Kakosi na Ilonga katika Wilaya mpya ya Momba na kuendelea katika Mkoa wa Rukwa kupitia vijiji vya Mambwenkoswe, Kalepua, Mwimbi, Kamawe hadi Kasitu (kwenye eneo la Mto Kalambo) katika Wilaya mpya ya Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukufua barabara hii, Timu ya watalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kwa kushirikina na wataalamu kutoka ofisi ya *TANROADS* Mkoa wa Rukwa mwezi Februari, 2013 ilitembelea barabara hiyo na kuikagua kwa lengo la kuifanyia matengenezo.

Aidha, ili kufufua barabara hii sehemu ya Kisatu hadi Kasanga kutahitajika ujenzi wa daraja kubwa katika mto Kalambo ili kuunganisha kijiji cha Kisatu na Nondo kuelekea kuelekea katika eneo la Kasanga.

Tathimini ya awali inaonyesha kuwa zinahitajika shilingi milioni 217.5 kwa ajili ya kujenga daraja na shilingi milioni 858.0 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe. Hivyo, gharama za matengenezo ya barabara na daraja kwa makadirio ya awali zinafikia shilingi bilioni 1.075.

Mheshimiwa Naibu Spika, azima ya Serikali ni kuijenga barabara hiyo ili kuwaondolea kero ya usafiri wananchi wa maeneo hayo. Kwa mantiki hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kalambo anaagizwa kufanya upembuzi yakinifu wa barabara hiyo ili kujua gharama halisi na hivyo kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, kwanza nashukuru kwa ufafanuzi wa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa vile usanifu wa awali unaonyesha gharama karibu ya bilioni 1.7 na Halmashauri ya Kalambo, katika makusanyo yake, hayazidi milioni 500.

Je, Serikali ipo tayari kuisaidia Halmashauri ya Kalambo ili kuwezesha matengenezo ya barabara hiyo?

Swali la pili, kutokana na shida iliyopo ambayo imeanza kukua kwa wananchi wa Halmashauri ya Kalambo, nini udharura wa Serikali kaytika kuwasaidia wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko *light*, Halmshauri ya Kalambo ile ni mpya, *own source* yake kama anavyosema, siyo milioni 500, ni milioni 700.5, ndiyo *own source* yake, hata ukiwaambia waende wakajenge wenyewe hawataweza wale, na fedha za barabara zilizopelekwa katika Wilaya hii mpya ya Kalambo hapa ni shilingi milioni 500, ndizo tumezipitisha hapa, kwa hiyo, unaweza ukaona tu kwamba haitawezekana.

Kwa hiyo, tunachokisema hapa, hii barabara kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe na hilo daraja liweze kujengwa pale la wakati wa Mjerumani, na bahati nzuri mimi nimekwenda katika hilo daraja, nalifahamu, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Kandege, ni Mbunge ambaye anapigania sana maendeleo ya watu wake, anahangaika nao kweli, hata kama hayupo hapa nadhani itakuwa ni sababu hiyo hiyo, ya kwamba anaendelea.

Mimi nataka nimpongeze sana, hapa cha kufanya hapa, cha kwanza, kwanza kabisa tumeagiza Halmashauri ifanye *feasibility study* ijue kiasi halisi kinachohitajika kwa ajili ya hii barabara, hiyo ya kwanza.

Sasa anazungumza habari ya udharura, udharura ni kupita kwenye barabara ya lami, kule ambapo tunajenga sasa hihi, maana yake apoitie Sumbawanga, pale wanatakiwa waende kilomita 112, kitu ambaho ni bugudha, lakini sasa hatuna jinsi kama mvua zitakuwa zimenyesha, lazima wapitie katika ile barabara. *Otherwise* hatuna namna ya kwenda kuweka magogo pale ni pagumu sana. Lakini mimi naomba tu wafanye haraka, watutengenezee hizo twakwimu, walete katika maombi maalum, halafu tutazungumza na Wizara ya Fedha tuone jinsi ya kuwasaidia. (*Makofi*)

Na. 314

**Kima cha chini cha Mishahara**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Serikali ilitangaza kima cha chini cha Mshahara kwa mfanyakazi kuwa ni shilingi 170,000/= kwa mwaka wa 2012/ 2013.

(a) Je, kwa nini Serikali haijaweka na kutoa tamko la kima cha chini cha mishahara kwa Mashirika ya watu binafsi pamoja na Kampuni kubwa za wawekezaji?

(b) Je, kwa nini Kampuni zenye uzalishaji mkubwa lakini wanalipa mishahara midogo kuliko kima cha chini cha Serikali?

(c) Je, kwa nini Kampuni binafsi hazitoi mikataba mirefu ili mfanyakazi apate haki zake?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimwa Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, lenye kipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi inasimamiwa na Bodi za Mishahara Kisekta. Bodi za Mishahara Kisekta zinaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, mishahara katika Sekta binafsi inapangwa kulingana na aina ya uzalishaji, mazingira ya kazi na eneo kwa sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 29 Mei, 2013 wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara Kazi na Ajira kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Serikali ilitoa tamko la kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi *(Private Sector)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni zenye uzalishaji mkubwa kulipa mishahara midogo, Serikali inalipokea suala hili kama changamoto. Bodi zilizoundwa kisekta na ambazo tayari zimeshaanza kazi ya utafiti zitaendelea zitabaini uhalali wa ulipaji wa mishahara kwa watumishi wa kila sekta husika.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini Na. 6 ya mwaka 2004, Mikataba ya kazi ipo ya aina tatu ambayo ni; Mkataba usio na ukomo wa muda, Mkataba wa muda maalum kwa Mameneja na kazi za taaluma, pamoja na Mkataba wa kazi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwajiri yoyote hapaswi kuajiri mfanyakazi kinyume na aina ya mikataba kama nilivyokwisha itaja hapo juu na kwamba aina zote tatu za mikataba ya kazi zinakubalika kisheria.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, napenda niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa amekili kwamba kuna Mashirika yake makubwa ambayo yanalipa kiwango cha chini cha mishahara, na ameunda Tume kwa ajiri ya kubaini changamoto hiyo.

Je, ikigundulika kwamba kuna Mashirika yanafanya uzalishaji mkubwa na wamewalipa mishahara midogo wale wafanyakazi, Serikali itachukua hatua gani?

Swali la pili, imetokea kwamba kuna mashirika wanaajiri wafanyakazi wa muda mfupi, wanaita *Season Labour*, na wale wanakwenda, miezi mitatu mitatu, na wanafanya kazi kwa muda wa miaka mingi bila kuajiriwa, kupewa mikataba ya kudumu.

Je, Serikali ikija kugundua, kwamba mtu amefanya kazi kwa muda mfupi mfupi, na hakupata haki zake, itaweza kuchukua hatua gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu Maswali mawili ya Nyongeza ya Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, kama hivi ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumetangaza kwenye wakati kuwasilisha Bajeti yetu hapa. Mishahara hii kwa kila sekta itatangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Kwenye Gazeti tutaonyesha viwango kamili ambavyo vitalipwa, kwa sekta zote 12.

Sasa kama kutakuwa na Kampuni ambayo itakwenda kinyume na malipo yatakayokuwa yameonyeshwa kwa kila sekta. Au kuna zile sekta ambazo zimewekwa kidaraja, kwa kila daraja, ni kwamba hatua kali za Kisheria zitachukuliwa kwa sababu atakuwa amevunja Sheria. Lazima alipe hicho kama kiwango cha chini. Lakini waweze wakalipa kiwango cha juu zaidi kutegemea na uzlishaji.

Pili, kuhusu wanaoajiriwa kwa Mikataba isiyo ya muda mrefu. Nimesema, kuna mikataba aina tatu. Na lazima wafanyakazi waangalie katika mikataba ya aina tatu ile. Mikataba usiokuwa na ukomo. Mikataba ya wale *Professionals,* ambayo inakuwa ni ya muda maalum au Mameja, na Mikataba ya kazi maalum. Ni mikataba hiyo mitatu tu. Hakuna Mkataba unaoitwa Mkataba labda wa *Temporary* au wa muda.

Sasa akipewa Mkataba wa aina hiyo lazima alipwe kutegemea na aina hiyo ya Mkataba na Mwajiri hawezi kwenda kinyume na Mkataba huo. Kama akienda kinyume na Mkataba aliompa basi, sheria itachukua mkodo wake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nilikuona Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimwia Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wetu wote nchini, hutegemea sana siku ya Mei Mosi hutangazwa kiwango cha mshahara ama kupanda au kutokupanda.

Je, Serikali inafikiri ni utaratibu huu mzuri huu wa wafanyakazi kungojea hali ya Kiongozi kutangaza kiwango cha chini au kikubwa cha mshahara. Haioni kwamba wakati umefika sasa kuwa na utaratibu ambao kila mfanyakazi atajua kiwango chake cha kuongezewa mshahara kinakuja ni *automatic,* badala ya kungojea hii hali ya kutangazwa tangazwa.

Je, huu ni utaratibu mzuri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, rafiki yangu kama hivi ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kutangaza mishahara kwa siku za karibuni, siyo kwenye majukwaa au kwenye Mei Mosi. Kwa watumishi wa Serikali, mishahara wanaikuta tayari kwenye *pay slip* zao. Lakini wakati wa kusoma Bajeti yake, Waziri wa Utumishi anaweza kuonyesha tu viwango kulingana na ongezeko la Bajeti ya mishahara kwamba Bajeti ya mishahara imeongezeka na kwa maana hiyo mwaka huo wafanyakazi wategemee nyongeza ya mishahara watakapopokea mishahara yao.

Kwa upande wa Sekta Binafsi, kama ambavyo Waziri wa Kazi na Ajira, amefanya. Mishahara hii hutaangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Ila anaweza kutoa mwelekeo, kwamba hali ni nzuri kwa maana mishahara itaongezeka ama kwenye Bajeti ama Mei Mosi. Lakini kujua hasa mshahara wa mfanyakazi ataona kama ni Sekta Binafsi ataiona kwenye Tangazo la Gazeti la Serikali. *(Makofi)*

Na. 315

**Ucheleweshaji wa Maamuzi ya Kesi Zilizokamilika**

**MHE. CLARA D. MWATUKA** aliuliza:-

Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha, kesi zisizohitaji uchunguzi au ambazo uchunguzi wake umekamilika kutotolewa uamuzi kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuweka wazi kwamba kesi zote za jinai zinazopelekwa katika Mahakama zetu ni lazima zifanyiwe upelelezi wa kina kabla hazijafunguliwa Mahamani. Kesi zikikisha funguliwa Mahakamani, Sheria na Kanuni zilizopo za uendeshaji wa Kesi zinataka Kesi isikilizwe na kutolewa uamuzi mapema ila kama kuna sababu ya msingi inayosababisha kuchelewesha maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sababu kadhaa ambazo zinasababisha ucheleweshaji wa maamuzi kwa kesi ambazo upelelezi wake umekamilika. Sababu hizo ni pamoja:-

(i) Wingi wa kesi zinazofunguliwa ikilinganishwa na idadi ndogo ya watumishi waliopo.

(ii) Sababu za kiufundi za kisheria yaani *(Legal Technicalities)* zinazosababisha mapingamizi ya kisheria na hivyo kukwamisha kwa muda ukamilishaji wa maamuzi/ uamuzi mapema.

(iii) Bajeti finyu inayosababisha:-

- Vikao vya kusikiliza kesi za Mahakama Kuu kutofanyika mara kwa mara.

- Vile vile upungufu wa virtendea kazi kwa upande wa Mahama za chini na Wadau wake.

- Kutopatikana kwa fedha za kuwalipa mashahidi.

(iv) Kutopatikana kwa mashahidi kwa wakati na kunakosababisha kesi kluahirishwa mara kwa mara.

(v) Mahabusu kutofikishwa Mahakamani siku za kusikiliza kesi zao.

(vi) Dharua kwa watendaji/pande muhimu kwenye kesi Mahakamani, kama vile Hakimu, Mwendesha, Mashtaka, Wakili wa Utetezi, Mshtakiwa na Wazee wa Baraza.

(vii) Lakini nyingine ni pamoja na uhamisho wa Mahakimu. Unaosababisha Kesi isiendelee, hadi atakapopatikana Hakimu mwingine wa kuendelea kusikiliza Kesi hiyo au kuanza kuisikiliza upya kwa kadri Sheria itakavyohitaji kwa Kesi husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Clara Mwatuka, ameridhika. Ninakushukuru sana, na Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema atauliza swali la nyongeza.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, inaonyesha wazi kwamba sababu inayosababisha au inayopelekea mambo yote haya kutokea ni ufinyu wa Bajeti.

Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kuiongezea Idara hii pesa ili isizidi kuwachelewesha Mahabusu Mahakamani na kuwanyima haki zao? *(Makofi)*

Swali la pili, Mheshimiwa Rais alipotemembelea Magerezani, alishauri kwamba kesi ndogo ndogo zitozwe faini, ili kupunguza msongamano wa Mahabusu Magerezani, pia kupunguza idadi ya kesi Mahakamani. *(Makofi)*

Je, Mheshimiwa Waziri, utekelezaji wa suala hili umefikia wapi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ametaka kujua endapo Serikali inaona ni muhimu kuiongezea Mahakama fedha. Ni kweli Serikali inaona ni muhimu kuiongezea fedha, na kama utakumbuka tarehe 3 Mei, 2013 tulipopitisha Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Idara ya Mahakama iliongeweza katika Mipango ya Maendeleo, Shilingi Bilioni 20 na kufanya hivi sasa

kuwa na Shilngi Bilioni 42.7. Lakini pia kwa upande wa fedha za Matumizi yaani *(OC)* mwaka huu tumetengewa Shilingi Bilioni 86.6, tofauti ni mwaka 2012, ambapo tulikuwa na takriban Shilingi Bilioni 57.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia siyo haya tu. Bunge lako Tukufu kupitia Kamati ya Bajeti na kupitia Wizara ya Fedha, imeiongezea Kurugenzi ya Mashtaka Shilingi Bilioni 10 zaidi kwa ajili ya *(O.C)* ili kuweza kuhakikisha basi tunafanya ziara za mara kwa mara katika Magereza yetu na kuhakikisha kwamba tunawatoa wale wote ambao wamebambikizwa kesi. Lakini pia kufahamu ni kesi gani za muda mrefu, ili ziweze kusikilizwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini endapo miaka ijayo ikiruhusu, tutashukuru pia tukiongezewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili, kuhusiana ni kwa nini sasa hatutumii utoaji wa faini au adhabu mbadala na utekelezaji wake umefikia wapi baada ya agizo la Mheshimiwa Rais, alipotembelea Magereza. Ni kweli aliagiza hivi, lakini pia ni kauli mbiu na niadhma ya Mahakama kutumia adhabu mbadala na ndiyo maana hivi sasa kwa kushirikiana na Mratibu wa huduma za jamii, Hivi sasa katika Mahakama nyingi tayari tunao Waratibu wa Huduma za Jamii, na adhabu hizi mbadala tayari zimekwisha kuanza kutolewa katika mikoa mingi ikianzia na Dar es Salaam, na tayari matunda tumeishaanza kuyaona.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tumsikilize mtu mwenye uzoefu mkubwa katika eneo hili Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Kesi za JInai tu zinazochelewa Mahakamani. Hata kesi za madai. Mfano mzuri ni kule Himo. Serikali imetangaza mji wa Himo upimwe, watu wajenge. Barabara zitengenezwe, lakini kwa muda wa

miaka 11 kuna kesi Mahakamani inayozuia ujenzi wa Mji ule na Mahakama inajua, Wizara ya Katiba na Sheria mnajua. Hata mimi nimekulalamikia, kwamba haiwezekani tuwe na mji usiopimwa, usiojengwa watu wana kesi Mahakamani, kwa kipindi cha miaka 11 hakuna upelelezi. Wanao dai wako pale pale na tunao daiwa tuko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri aniambie. Hatima ya mji wa Himo ni nini, na kesi iliyopo Mahakamani kwa miaka 11?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabsia ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mrema kwamba tayari jana tarehe 30 Mei, 2013 Mheshimiwa Jaji Mziray, ameishafika katika Mahakama hiyo na tayari ameishaanza kusikiliza na ana wiki mbili atakuwa ana vikao vya Mahakama kwa ajili ya kusikiliza kesi tatu. Inaweza ikaonekana ni kesi chache. Lakini ni kesi ambazo zina wadai wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, kwa sababu ndani siku 14 tunatarajia kesi hiyo ya kwako ya wadai 700 itakuwa imeshatolewa hukumu. Lakini nikuombe uwaambie wadai hao 700 wajaribu kufika Mahakamani. Kwa sababu kesi hiyo inaendelea na kila siku ushahidi unatolewa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa kweli Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa jibu hilo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Swali langu ni jepesi tu lakini ni la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kumekuwa na ucheweshaji mkubwa sana wa kesi, ambao pamoja na mambo mengi unachangiwa na kushindwa, kufikishwa

Mahakamani kwa Watuhumiwa. Nikitoa mfano wa Mahakama ya Wilaya ya Hai. Mahabusu ambao wako katika Magereza ya Karanga, ambayo iko katika eneo la Manispaa ya Moshi, hupelkwa katika kesi zao katika Wilaya ya Hai, mara moja kwa wiki. Kama kwa bahati yoyote ile mbaya au nzuri Hakimu akawa hayupo au sababu nyingine yoyote, ina maana watasubiri wiki nyingine tena ya Alhamisi nyingine kupelekwa Mahakamani. Kwa hiyo, watu wanakaa Magerezani bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali, atuambie, kuna utaratibu gani wa kumaliza tatizo hili, kwa sababu wako watu wengi ambao wanateseka kukaa sana Magerezani kwa sababu tu ya kushindwa kufikishwa Mahamani. Kwa nini tunawaadhibu watu kwa kesi ambazo hazistahili? *(Mkofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimwia Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Mbowe, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa jukumu la kusafirisha Mahabusu ni Jukumu la Jeshi la Polisi. Lakini kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam, hivi sasa jukumu la kusaifirisha Mahabusu liko chini ya Magereza. Wote tunatambua kwamba Polisi wamekuwa wakifanya kazi nzuri, lakini wanakbailiwa na ukosefu wa mafuta. Lakini pia wanakbiliwa na uhaba wa Magari.

Hivi sasa tayari Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, anajitahidi kuzungumza na Wafadhili mbali mbali, lakini pia kupitia Wizara ya Fedha kuona ni kwa namna gani basi wanaweza wakongeza Idadi ya Magari na Mafuta kwa ajili ya kuongezea magari haya kuwasafirisha Mahabusu.

Lakini siyo hiyo tu, kupitia Mradi wa *Programme* wa Maboresho wa Sekta ya Sheria tumekuwa tukinunua Mabasi mbali mbali na tumekuwa tukiyasambaza katika mikoa mbali mbali. *(Makofi)*

Na. 316

**Kuboresha Huduma ya Maji Makambako**

**MHE. SELEMANI S. JAFO (K.n.y. MHE. DEO KASENYENDA SANGA)** aliuliza:-

Mji wa Makambako unakua kwa haraka na idadi ya watu zaidi ya 50,000 wakati miundombinu ya maji iliyopo inatosha kuhudumia watu 15,000 tu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma hii ya maji ili kuwasaidia wakazi wa Makambako?

**NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimwia Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mji wa Makambko unakua kwa kasi na idadi ya Watu inaongezekana kila mwaka. Ongezeko hilo la watu linasababisha kuongezeka kwa mahitaji ya maji kwa wakazi wa mji huo. Ili kuboresha huduma ya maji kwenye mji huo, mwaka 2008/2009, Serikali ilitumia Shilingi milioni 90, kwa ajili ya kuchimba visima virefu viwili (2) pamoja na kukarabati mfumo wa usambazaji wa maji.

Pia Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *American Cultural Resources Assossosion (ACRA).* Imechimba jumla ya visima vinne (4) na kati ya visima hivyo vilivyochimbwa visima vitatu (3) vilipata maji. Visima hivyo vina uwezo wa kutoa jumla ya lita 614,400 kwa siku ambazo zitaongeza huduma ya maji kufikia asilimia 62. Hadi sasa, ujenzi wa miundombinu ya maji umekamilika kwa asilia 90 na visima viwili (2) vimeanza kutoa maji.

Aidha, katika kuendelea juhudi za kuboresha upatikanaji wa maji katika mji wa Makambako, wa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 150 zitakazotumika kwa ajili ya upanuzi wa chanzo cha maji pamoja na kuboresha mfumo wa usambazaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya muda mrefu, mwezi Machi, 2012, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina pamoja na uandaji wa makabrasha ya zabunni. Serikali inandelea kutafuta fedha ili kuanza ujenzi huo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, natambua juhudi kubwa zinazofanywa katika mji wa Makambako. Lakini kwa ajili ya kutafuta tatizo hili na mpaka hivi sasa katika mwezi Septemba, mpaka mwezi Desemba, mara nyingi sana mji huu unakuwa na shida na kadhia kubwa kwa wananchi wa mji wa Makambako.

(a) Je, Serikali ina mpango gani kutengeneza kikosi kazi, kuhakikisha kwamba hii pesa iliyotengwa na hii Miradi inakamilika ili mradi kuondoa tatizo kubwa la watu wa mji wa Makambako?

(b) Kwa kuwa mji wa Makambako sambamba na ule mji wa Kisarawe shida zao za maji. Na kwa kuwa Serikali, kwa nia ya dhati imeona kwamba ni vema kuhakikisha miundombinu kutoka Mipera na Kimbiji inasaidia kuletwa katika jiji la Kisarawe. Lakini kwa kuwa mradi huu unawezekana ukachelewa sana kukamilika.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba kisima kilichochimbwa pale katika eneo Vigama katika mji wa Kisarawe, ambacho kimefunikwa sasa hivi kina mika mitatu. Kikaweka miundombinu, ili maji yale yakaingia katika mfumo wa maji kuwasaidia Wana-Kisarawe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili analolisema Mheshimiwa ni kweli. Pale Makambako inavyokuwa idadi ya watu wamefika 100,000. Idadi ya watu waliopo pale ni kubwa kwa sababu ya biashara zinazofanyika kati ya Zambia na nchi yetu ya Tanzania.

Kwa hiyo ninakubaliana naye. Na *capacity* iliyopo pale *tank* tunalopeleka pale, tunalotegemea litafanya kazi ile. Tanki lile lina uwezo la lita 100,025. Kwa maneno mengine kila mwananci aliyeopo pale ni kama anapata lita 1.2 na 1.3. Kwa hiyo Mheshimiwa Jafo pale ana *point* kubwa, ninakubaliana na yeye.

Ukiangalia hesabu inaonyesha kwamba ili kukamilisha mpango mzima wa wananchi wote waliopo pale Makambako wapate maji safi na salama, unahitaji Shilingi Bilioni 57.7. Sasa unaweza ukaelewa kwamba hili tatizo ni kubwa. Lakini mimi niadhani tumeleza hapa mambo ambayo tunayafanya. Vile visima vyote nilivyovitaja hapa tutahakikisha kwamba vinatoa maji safi na salama kwa ajili ya kuwasaidia wananchi.

Kwa hiyo, nilitaka nitoe hizi takwimu tu kuonyesha *magnitude* ya *problem* iliyopo pale na *population* iliyoko pale Makambaku ni kubwa inakuwa kwa hiyo kuna jambo la msingi linalosemwa hapa ambalo tutaendelea kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili ni pamoja na lile la Kisarawe alilolizungumziwa Mheshimiwa Jafo, tumeweka katika utaratibu kama mmemsikiliza vizuri Waziri wa Maji alipokuwa anawasilisha hapa hotuba yake. Mamlaka zote za Maji, na Mamlaka zote za miji, zote zilizopo katika nchi hii, zimewekewa utaratibu maalum na ni nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiki anachokisema Mheshimiwa Jafo kwa maana ya kile kisima kilichopo pale, tutakachofanya hapa ni kujaribu kwenda kuangalia vizuri anachokisema ili niweze kupata, kwa sababu sikujua kwamba atauliza Swali la namna hiyo ili tuweze kusaidiana na yeye.

Habari ya kuunda kikosi maalum kwa ajili ya maji, hizi Mamlaka zote tunazozitaja hapa zina Mamlaka za Maji labda kitu ambacho tunakifanya hapa ni kuboresha tu hizo Mamlaka za Maji zilizopo kule ili tuweze kusaidiana na kuhakikisha kwamba tunaondoa hili tatizo. *(Makofi)*

Na. 317

**Tatizo la Maji Katika Mji wa Shirati**

**MHE. ESTHER M. MATIKO** aliuliza:-

Mji wa Shirati ulikuwa na Mamlaka ya Maji chini ya Kanisa la *Menonite Tanzania* (*KMT*) ambapo usambazaji wa maji haukuwa tatizo lakini mwaka 2004 KMT ilikabidhiwa Mamlaka ya Maji Serikalini na tangu wakati huo kumekuwa na kero kubwa sana ya maji.

(a) Je, kwa nini Serikali imeshindwa kutengeneza mashine iliyoharibika ili kurejesha huduma ya maji kwa wananchi?

(b) Je, gharama ya kutengeneza mashine hiyo ni kiasi gani na kama ni kununua msahine nyingine itakuwa kiasi gani cha fedha ambacho Serikali haiwezi kumudu tangu mwaka 2004?

(c) Je, ni kwa nini Serikali inaendelea kuwalipa mishahara wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji wakati hawafanyi kazi yoyote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI NKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kulikuwepo na tatizo la upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Mji wa Shirati kutokana na kuharibika kwa mashine. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imenunua na kufunga pampu tatu pamoja na mota mbili kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa Shirati na hospitali za Shirati na Rao. Kazi hizo zimeboresha huduma ya maji katika eneo la Shirati na katika hospitali hizo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mashine zilizokuwa zikihudumia mji wa Shirati ziliharibika kutokana na kuungua kwa mota zake. Hata hivyo, ilibainika pia kuwa mashine hizo zilikuwa na uwezo mdogo kukidhi mahitaji ya maji ya sasa kwa wakazi wa Mji wa Shirati. Aidha, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hapo juu, ununuzi wa pampu mpya tatu, mota mpya mbili na kurudishia umeme uliokatwa uligharimu jumla ya shilingi milioni 500.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji katika mji wa Shirati inasimamiwa na Jumuiya ya Watumiaji Maji Shirati (*Shirati COWSO*). Watumishi waliopo kwenye Jumuiya hiyo hufanya kazi kwa mkataba na hulipwa pale inapotokea kazi ya kufanya. Watumishi hao hufanya kazi za ulinzi wa nyumba ya mashine, uendeshaji mashine, ukusanyaji maduhuli na matengenezo madogomadogo ya miundombinu ya mradi huo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ingawaje kuna rekebisho kidogo kwani kwa karatasi niliyopewa gharama halisi wameniambia ni shilingi milioni 100 lakini Mheshimiwa Naibu Waziri ananiambia ni shilingi milioni 500. Sasa sijui lipi ni sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali ilinunua na kuweka mota kwenye Hospitali ya Shirati lakini kwa taarifa zilizopo ni kwamba baada ya miezi mitatu tu ile mashine ilikufa ambayo ilikuwa ni ML 91, sasa inawezekana kabisa hii mashine ambayo Serikali imenunua na kufunga ilikuwa haina kiwango na tukizingatia umuhimu wa hospitali kwamba tunahitaji maji. Nataka Serikali inihakikishie vipi itaboresha huduma ya maji katika Hospitali ya Shirati kwa kwenda kununua pampu ambayo ni imara na ambayo ita-*sustain* matumizi.

Pili, kwa kuwa, matatizo ya maji na hasa kwa Mkoa wa Mara wanawake tumekuwa tukiteseka sana na kwa mwaka huu tu tumeshuhudia mama mjamzito ameamka alfajiri kwenda kutafuta Mto Mara akakamatwa na Mamba ikabidi apate *pre-labour.* Nataka Serikali inihakikishie kwamba itawezaje sasa kutoa kipaumbele katika Majimbo yote ya Mkoa wa Mara kuhakikisha kwamba tatizo la maji kwa akina mama ambao tunatembea kilomita nyingi na tunaamka usiku kitu ambacho kinapekea hata wengine kupata talaka linatatulika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, nilimwona Mheshimiwa Wassira anaangalia kwa umakini!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI NKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI)**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba aniwie radhi kwamba ni kweli kwamba nimepitiwa tu hapa, ni shilingi milioni 100 kama unavyosema, ukikaa hapa ni kitimoto wakati mwingine inakuwa ni shida, lakini ni shilingi milioni 100 na hii karatasi niliyonayo hapa imeandikwa hivyohivyo naomba *Hansard* isahihishe kwani *she is right* na ni sahihi anavyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pampu, hii habari ya pampu anayoisema hapa nilijua itaulizwa, kwa hiyo, nimeuliza Shirati karibu mara kumi wakaniambia pampu za mwanzo ni kweli zilikuwa na mushkeli na ndizo zilizoharibika. Hizi pampu tunazozigumza sasa ni pampu mpya. Mimi nasema kabisa kwamba hapa tunachozungumza sasa kama Mheshimiwa Matiko anakuwa Tomaso kwamba ana wasiwasi na hizo sasa tusubiri tuzione kama zitaleta matatizo tutakuja kueleza. lakini sasa nisemeje?

Niseme tunazing'oe tena na zile ambazo zimeletwa mpya pale au ambazo tumeweka mpya na zile mota? Ninachosema hapa ni kwamba tumecheki tumerudia na tume-cross check na asubuhi hii tume-*cross check* tena na Shirati ili kuhakikisha kwa sababu nilijua hili swali litakuja hapa. Kwa hiyo, mimi *I stand to be corrected* anaweza akaja ofisini tukacheki vizuri aipate *from the horses mouth* ili tuweze kuwa vizuri. Nilijua hilo litakuja.

La pili, kuhusu Mama anayesema hapa ni jambo la kusikitisha kwamba Mama sasa kwa sababu ya matatizo ya maji yaliyopo pale amekwenda kule ameparamiwa na wanyama na kadhalika, hili ni jambo ambalo kama Taifa tumelipokea na Serikali linatusikitisha kwamba linatokana na tatizo la maji lililopo vijiji vyetu na unaona kwamba amepata matatizo hayo na kwamba mbele kule inaweza ikasababisha na talaka na kadhalika. Wanawake wakaachika kwa sababu ya tatizo hilo la maji. Ni kweli inaweza ikatokea hivyo kwa sababu Mama akienda kwenye maji huwezi kupambanua kwamba ni maji tu au kuna mambo mengine yanayoendelea kule na kadhalika. Inaweza kuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi sisi tuseme hivi, hii Shirati inayosemwa hapa ungeweza ukaondokana na tatizo lake kama ingekuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Shirati yaani ungekuwa na mamlaka ungekuwa na *authority,* ndiyo maana hapa tunazungumza *Association,* na *Association* inaanzishwa wakati unapokuwa na vikundi viwili vinaanzishwa pale ndiyo inaanzishwa pale. Kwa hiyo, utaona kwamba hata ukienda ule mpango wa maji ili kuona kama mradi wa maji katika huu mji wa Shirati upo unakuta kwamba haipo.

Sisi tutamshauri Mheshimiwa Waziri wa Maji kuona kwamba Shirati iangaliwe kwa jicho tofauti. Mimi nimefika Shirati na hao Kanisa la *Menonite* ambao wanatusaidia tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya pale. Tutakwenda kumshauri Waziri kwa sababu mpango uliopo ni wa miji midogo ndio ulipo pale, sasa Shirati kwa sababu siyo mamlaka ya Mji mdogo na hili nitoe changamoto pia kwamba tuliwahi kuwashauri mwanzishe Mamlaka ya Mji mdogo pale ili muweze kupata huduma kwa mujibu wa hicho kitu tunachokizungumza hapa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, na mimi nikubaliane na wewe kwamba sababu za talaka zipo nyingi.

Wizara ya Maliasili na Utalii, swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele!

Na. 318

**Matumizi ya Nyuki Wadogo kwa Asali**

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE** aliuliza:-

Je, ni kwa nini watumiaji wengi wa Asali wanapenda zaidi kutumia Asali ya Nyuki wadogo kwa matumizi yao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Asali ya Nyuki wadogo hupendwa na watu wengi kutokana na uwezo wake wa kutibu magonjwa mbalimbali ya wanadamu. Uwezo wa kutibu magonjwa mengi unasababishwa na Nyuki hawa wadogo kutembelea mimea mingi zaidi wakati wa kutengeneza Asali kuliko Nyuki wakubwa. Utafiti kutoka nchi za Amerika ya Kusini unaonesha Nyuki wadogo wanatembelea mimea yenye maua (*Foraging*) mara mbili zaidi ya idadi ya mimea inayotembelewa na Nyuki wakubwa. Kwa kuwa, dawa nyingi zinatokana na mimea, Asali ya Nyuki wadogo ina uwezo wa kimatibabu zaidi ya (*Medicinal Value*) kuliko ile ya Nyuki wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine inatokana na ladha na riha ya ukakasi au ugwadu ambao haikinaishi. Hapa nchini Tanzania utafiti kuhusu Nyuki wadogo na Asali yake bado uko katika hatua za awali. Kwa hiyo, Wizara haina takwimu sahihi ni magonjwa aina gani yanatibiwa na Asali ya Nyuki wadogo kuliko ile ya nyuki wakubwa. Utafiti uliofanyika katika nchi za Guatemala, Mexico na Venezuela unaonyesha kuwa Asali ya Nyuki wadogo inasaidia akina Mama waliojifungua kupona upesi *(post birth recovery),* maradhi ya mfumo wa chakula, mfumo wa hewa, kuimarisha mfumo wa uzazi kwa akina Mama (*female fertilite*), kutibu maradhi ya ngozi na kusaidia macho kuona vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Asali ya Nyuki wadogo (wasiouma) haipatikani kwa wingi ikilinganishwa na nyuki wakubwa (wanaouma), hii ni kutokana na maumbile yao kuwa madogo ambapo uzalishaji wao ni lita moja hadi tano kwa kundi la Nyuki. Wakati Nyuki wanaouma uzalishaji wao ni lita tano hadi ishirini kwa kundi. Nichukue fursa hii kuwaomba wananchi watumie Asali za Nyuki wote kwa kuwa viini lishe na viini tiba katika Asali hizo ni sawa.

Pia niwaombe wafuge Nyuki wasiouma karibu na makazi yao endapo hakuna shughuli zinazotumia viatilifu. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, maelezo ya Serikali yamekiri kwamba Asali ya Nyuki wadogo ina uwezo zaidi wa kimatatibabu kuliko kitu kingine chochote. Je, kwa nini utafiti huu usiende sambamba na ule wa mti wa Mrigariga uliotumiwa na Babu wa Loliondo Mchungaji Ambilikile Mwaisapile, kwa nini utafiti huu usiende sambamba ili kubaini magonjwa ambayo Asali ya Nyuki wadogo wanaweza kutibu kwa binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kaika Telele, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimhakikishie tena Mheshimiwa Telele na nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba utafiti wa faida zinazopatikana kimatibabu na kilishe za Nyuki wadogo hapa nchini zinaendelea na utafiti wa jumla katika tasnia ya Nyuki unaendelea. Pili, Serikali katika hatua mbalimbali imeendelea kuangalia na kufanya kufanya utafiti wa mti wa Mrigariga kwa sababu wote tunafahamu shughuli ambayo alikuwa anaifanya Babu wa Loliondo ilihamasisha watu wengi nchini na katika Bara la Afrika na tuliambiwa hata nje ya Afrika watu wamekwenda Loliondo na tunaamini kwamba tafiti hizo zitakapokuwa zimekamilika hatutasita kuleta majibu hapa Bungeni.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, siku ya uzinduzi wa ufugaji Nyuki kitaifa ulifanyika Mkoani Singida Wilayani Manyoni na Mheshimiwa Waziri Mkuu na akawaahidi wanawake wajasiriamali Singida kwamba atawapa mizinga 120 na mizinga 100 kwa kila Wilaya baada ya kuona juhudi za Mkoa wa Singida kwa kutundika mizinga.

Je, ni lini hiyo mizinga itafika Singida?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika Singida katika uzinduzi wa siku ya ufugaji wa Nyuki hapa nchini na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi mizinga hiyo 120 kwa ajili ya akina Mama na mizinga 100 kwa kila wilaya na nimhakikishie Mheshimiwa Chilolo kwamba ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inatekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na tunajiandaa na tutaitekeleza mapema iwezekanavyo.

Na. 319

**Kiwanda cha Kusindika Nyama – Mbeya**

**MHE. ALIKO N. KIBONA (K.n.y. MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE)** aliuliza:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu atalipotembelea Kiwanda cha Kusindika Nyama Mbeya aliuagiza Uongozi wa Kiwanda hicho kwamba kama kiwanda bdo hakijapata mwekezaji basi kiwekwe katika mpango wa haraka wa kukifufua.

(a) Je, kiwanda kimeishapata mwekezaji?

(b) Kama bado hakijapata mwekezaji, je, ni lini Serikali itakifufua kiwanda hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale Mbunge wa Mbeya Vijijini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Kiwanda cha Nyama cha Mbeya ambao ulianza mwaka 1975, ulisimama mwaka 1978 kutokana na ukosefu wa fedha. Kutokana na mabadiliko ya kisera yaliyoelekeza kuwa shughuli nyingi za kiuchumi zifanywe na sekta binafsi, mnamo mwaka wa 2008 *PSRC* ilianza kutafuta mwekezaji makini atakayekiendeleza, juhudi ambazo hazikuzaa matunda.

Mnamo mwezi Machi mwaka 2013, Shirika la *Consolidated Holdings Cooperation (CHC)* lilitoa tangazo la kutafuta mwekezaji kwenye magazeti. Kufuatia matangazo haya, hadi tarehe 24/4/2013 iliyokuwa siku ya mwisho ya kupokea maombi, makampuni matatu ya *Jovet Tanzania Limited, Tanfroz Tanzania Limited na Tandam Farms* yalikuwa yamejitokeza na kamati ya wataalam imeanza kuyafanyia tathmini na mapendekezo yake yatapelekwa kwenye Bodi ya *CHC* kwa maamuzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge kuvuta subura hadi hapo uamuzi utkapotolewa. Aidha, napenda kumjulisha kuwa, iwapo *CHC* haitampata mwekezaji makini anayekidhi vigezo vilivywekwa Wizara itatekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kufufua kiwanda hiki kwa kukiombea fedha kwenye Bajeti ijayo.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba wakulima wa Chai wa viwanda, Miwa wana viwanda, Kahawa wana viwanda, Pamba wana viwanda, Nyuki wana viwanda, Zabibu wana viwanda na kadhalika. Kwa nini na ni sababu gani zimesababisha taifa letu lenye mifugo mingi ya kutosha mpaka sasa hivi tukose kiwanda cha Nyama ambacho kingewaongezea wakulima wetu thamani ya mifugo yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, majosho ya mifugo vijijini mengi yamekufa, *operation* ya chanjo kama tulivyozishuhudia siku za nyuma hazipo tena, Mabwana Mifugo wengi wanaishi mijini, inaonyesha kabisa kwamba hatuko makini na sekta hii ya mifugo. Ni nini sasa au ni lini Serikali itaweza kurekebisha jambo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mazao mengi yana viwanda lakini Serikali ina mikakati ambayo tumeianza ya kufufua viwanda vilivyokuwepo zamani na kujenga vipya na kwa taarifa tu ya Mheshimiwa Mbunge katika ukanda huo wa Kusini tayari kiwanda cha nyama kimejengwa Iringa kilichogharimu jumla ya shilingi milioni 596 na hii imefanywa Serikali imechangia mfuko wa *ASDP* na *UNIDO* imechangia. Baada ya kiwanda hiki kuanza kazi mwezi Desemba kingine kitajengwa Mbeya kwa mtindo huohuo wa kuchangiwa na mifugo hiyo niliyoitaja ambayo imechangia machinjio ya Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kweli miundombinu mingi inahitajika na hasa ya maji na majosho na katika mkakati na mpango wa kuendeleza sekta ya mifugo, mapendekezo yapo na tutakapoleta Bajeti yetu leo tunaomba mtuunge mkono ili angalau harakati hizi za kujenga miundombinu kwa ajili ya mifugo iweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la chanjo mwaka jana tulipitisha sheria iliyobadilisha maabara kuu ya mifugo kuwa wakala na kwa sasa wakala wana uwezo wa kutengeneza chanjo kadhaa zikiwemo ya *SBPP, Foot and Mouth* na mdondo kwa wafugaji wa kuku.

Kwa hiyo, kwa hili la chanzo tuna uwezo sasa kutengeneza lakini tunahitaji kuwezeshwa zaidi kifedha ili jitihada hizi ziweze kuwanufaisha wafugaji wetu kokote waliko waliko katika nchi yetu.

Na. 320

**Ahadi ya Njia Mbili Kutoka Morocco – Kawe**

**MHE. RITA LOUISE MLAKI** aliuliza:-

Tatizo la mafuriko na uharibikaji wa barabara ya *Old Bagamoyo* eneo la *TMJ Hospital* na *Mayfair* limekuwa kubwa na baya kwa muda mrefu kiasi cha kusababisha msongamano mkubwa wa magari na ajali wakati mwingine.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

(b) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuijenga barabara hiyo toka Morocco hadi njia Panda ya Kawe, kwa kiwango cha njia mbili?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Meheshimiwa Rita Louse Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mafuriko na uharibifu wa barabara ya *Old Bagamoyo* eneo la *TMJ Hospital* husababishwa na kutozingatiwa kwa Kanuni Kanuni za ujenzi wa majengo katika eneo husika ikiwa ni pamoja kujenga kuta za majengo, kuziba mifereji, kutupa takataka katika mifereji inayopitisha maji na kadhalika. Hata hivo, ili kutatua tatizo la mafuriko katika barabara ya Old Bagamoyo eneo la *TMJ Hospital* na *Mayfair* linalojulikana kama Bonde la Mpunga, Wizara kupitia *TANROADS* tayari usanifu wa kina wa mfumo wa maji ya mvua *(storm Water Drainage System)* umefanyika na kukamilika.

Kazi ya ujenzi wa mfumo wa maji ya mvua katika eneo la Bonde la Mpunga inatarajiwa kuanza na kukamilika katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kwa sasa Mhandisi Mshauri anakamilisha makabrasha ya kuitisha zabuni.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya kujenga barabara kutoka Morocco hadi njia panda ya Kawe kuwa njia nne (4 *lane dual carriageway*) imeanza kwa kukamilisha usanifu. Serikali inatafuta fedha ili ujenzi uweze kuanza mapema iwezekanavyo.

**MHE. RITA LOUISE MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanatupa matumaini wananchi wa Kata ya Mikocheni, hususan Bonde la Mpunga katika jimbo la Kawe. Ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa, katika juhudi za kujinusuru na mafuriko haya wananchi wanaoishi katika Kata ya Mikocheni hususan eneo la Bonde la Mpunga na lililopo nyuma ya *Engene Petrol Station,* wamejenga kuta holela ili kujinusuru kila mtu na nyumba yake, kwa maana hiyo hata tutakapojenga mifereji mikubwa bado kuna watu wataathirika na mafuriko ya wenyewe kwa wenyewe.

Je, Serikali itakuwa tayari kuniunganisha mimi na hao wahandisi watakaoshughulikia mradi huo ili tuweze kupata ushauri na maelezo ya kuwasaidia wananachi hawa?

Swali la pili, kwa kuwa, barabara ya kuanzia Morocco hadi Kawe ambayo imeishafanyiwa usanifu lakini bado haijatengewa fedha itachukua muda mrefu kabla ya kujengwa, sasa foleni imehama au kupugua katika barabara ya Ali Hassan mwingi na sasa imeongezeka barabara ya chini ya Afrikana mpaka Morocco.

Je, Serikali itakuwa na mpango gani wa kutupatia msaada wa dharura ikizingatia hali halisi ya foleni?.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mlaki kwa shukurani ambazo ametoa kwa Serikali. Pili niseme tu kwamba, masuala ya kujenga kuta kiholela, Manispaa ya Kinondoni inabidi ichukue hatua. Hili ndilo tatizo kubwa ambalo tunalipata kwenye barabara ile. Watu wanajenga zile kuta na hawaweki matoleo ambapo maji yanaweza kupita, hivyo mvua zikinyesha barabara nzima inakumbwa na mafuriko. Naomba nitoe agizo kwa Manispaa ya Kinonondoni kuchukua hatua na kuwaelekeza hawa wenye nyumba ambao wamejenga bila mpangilio, waweze kubomoa kuta zile ili maji yaweze kupita kwa kufuata mkondo wake.

Kuhusu sehemu ya pili ya swali lake juu ya mpango wa dharura, nafikiri ili kupunguza msongamano ni lazima barabara ile ijengwe kwa njia 4 kama nilivyosema kwenye jibu la msingi. Hata hivyo, tutaendelea kuitengeneza barabara ile iweze kutumika kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara. *(Makofi)*

Na. 321

**Utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu**

**MHE. ASHA MUHAMED OMAR** aliuliza-

Je, kwa nini utaratibu wa utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu usirudishwe kuwa kama wa zamani kwa Zanzibar kupewa nafasi zake kwa idadi maalum ili kuepusha vitendo vya upendeleo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Muhamed Omar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tangu Serikali ilipoanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu mwaka 1994 hatujawahi kuwa na utaratibu wa Tanzania Zanzibar kupewa nafasi zake kwa idadi maalum ya wanafunzi. Kuanzia wakati huo mikopo

ilitolewa na iliyokuwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, hadi ilipoanzishwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu mwaka 2004. Sheria ilyounda Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa ELimu ya Juu, imeelekeza mikopo kutolewa kwa mtanzania yeyote mhitaji aliyepata udahili katika chuo cha elimu ya juu chenye ithibati na mwenye kutimiza vigezo vilivyowekwa bila kujali anatoka sehemu gani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kabila lake, dini yake au itikadi yake ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, huzingatia taratibu za kisheria, miongozo mbalimbali na vigezo ambavyo hutolewa kila mwaka bila kuwa na vitendo vya upendeleo. Vigezo huangalia zaidi uhitaji wa mwombaji, vipaumbele vya taifa, ukomo wa Bajeti ya Serikali pamoja na sifa za kitaaluma za mwombaji wa mkopo.

**MHE. ASHA MUHAMED OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nakubaliana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa upande wa Zanzibar huwa ni kazi ngumu kwa mwanafunzi mwenye sifa hizo kupata mikopo.

Je, ni kwanini sasa kusiwe na idadi maalum ya wanafunzi wanaotoka Zanzibar ili kuondokana na usumbufu unajiotokeza?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba, mwongozo wa utoaji wa mikopo unaangalia hasa uhitaji wa mwombaji. Je, huyu mwombaji ana uhitaji?

Hilo ndilo kubwa zaidi na haliangalii anatoka upande gani katika nchi yetu. Vijana wa Zanzibar kama vile vijana wa Tanzania Bara wamekuwa na nafasi sawa ya kupata mikopo. Kila mwaka vijana wa Zanzibar wengi zaidi walikuwa wanapata mikopo kufuatana na mahitaji yao. Watatofautiana chuo na chuo, mwaka fulani wanapata wanafunzi wengi zaidi, mwaka mwingine wanapata

wanafunzi wengi zaidi wenye mikopo. Hata hivyo, kila mwaka idadi hiyo imekuwa ikiongezeka kama ambavyo idadi ya jumla ya wanafunzi wanaopata mikopo imeongezeka sana. Tangu ilipoanza mwaka 1994 ambapo wanafunzi 6061 walipata mikopo, mpaka mwaka huu wa masomo ambapo ni wanafunzi elfu 98 na ushee ambao wamepata mikopo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda kama mnavyoona naomba tuchukue swali la mwisho la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa.

Na. 322

**Vyuo vya Walimu wa Shule za Awali**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Je, Serikali inajua idadi ya vyuo vilivyosajiliwa kufundisha Walimu wa Elimu ya Awali (Chekechea) tu hapa nchini na ni vingapi vya Serikali na ni vingapi ni vya watu binafsi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Elimu ya Awali ni elimu inayotolewa kwa watoto wenye umri wa miaka 5 hadi 6 ambao wanaandaliwa kuingia Elimu ya Msingi (Darasa la kwanza). Elimu ya Chekechea *(Nursery)* ni elimu ya malezi inayotolewa kwa watoto wenye umri wa kati ya miaka 3 na 4 chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya ELimu na Mafunzo ya Ufundi, ndiyo yenye jukumu la kusajili shule za Awali, Msingi na Sekondari na pia Vyuo vya Ualimu. Kutokana na Mtaala

wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti wa mwaka 2009, mafunzo ya Uallimu wa Elimu ya Awali ni mchepuo mmojawapo katika Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti (Daraja A). Michepuo mingine ni Cheti cha Elimu ya Michezo na Cheti cha Elimu ya Kawaida. Kwa mantiki hiyo sifa za kujiunga na mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali ni sawa na sifa za kujiunga katika mafunzo ya Cheti Michezo na Cheti Kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila chuo cha ualimu kilichosajiliwa kutoa mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti na ngazi ya Stashahada, kinaweza kutoa mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali kutegemeana na uwepo wa wakufunzi wa Elimu ya Awali. Kwa sasa vyuo vya Ualimu vya Serikali vinavyoweza kutoa mafunzo ya ualimu wa Elimu ya Awali Ngazi ya Cheti ni 34 na visivyokuwa vya Serikali ni 89.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Niulize maswali mawili mafupi tu.

Swali la kwanza, kwa kuwa, hapa nchini tatizo kubwa ambalo linajitokeza mara kwa mara ni kwa wanafunzi wa Darasa la I – VII kumaliza shule bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, ambapo nadhani ni kutokana na kukosa haya madarasa ya awali.

Je, Waziri haoni kuwa sasa ni wakati mwafaka kwa kila shule ya msingi kuwa na madarasa haya ya awali kwa sababu Walimu wengi ambao wamefuzu madarasa hayo wamo mitaani?

Swali la pili, katika jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri amesema kuna idadi ya vyuo 123 (34 + 89). Kwa swali langu ambalo linasema hapa kwamba, walimu wengi ambao wamefuzu elimu hiyo ya kufundisha madarasa ya wali wamo mitaani. Je, Waziri anaweza akatamka sasa kwamba, walimu hao ninaosema wako mitaani huko wakiwa hawana shule za kufundisha, wajitokeze na kwa tamko lake wamuone nani ili shule hizi ziweze kupata walimu wa madarasa ya awali? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kuhusu hitaji la kuwa na darasa la elimu ya awali katika kila shule ya Msingi. Hiyo ndiyo sera yetu kwa sasa na ndiyo ahadi ya Chama cha Mapinduzi na tunaenda nayo kwa kasi sana.

Hivi karibuni tumemaliza zoezi maalum ambalo limeangalia namna ambavyo tunaweza tukaboresha elimu ya msingi kwa kusisitizia elimu ya awali na elimu ya msingi katika ngazi za chini kwa maana ya darasa la I na II.

Kwa hiyo, tutaelekeza fedha na nguvu zetu zote katika eneo hili ili tuweze kutekeleza kile ambacho Chama Cha Mapinduzi kimeahidi katika Ilani yake.

Swali la pili, kuhusu walimu wa elimu ya awali. Kwanza nasikitika kama kuna walimu hao wako huko kwa sababu tunawahitaji sana na tunaendelea kufungua nafasi nyingi zaidi katika shule zetu kwa madarasa ya elimu ya awali.

Sekta binafsi pia imetuunga mkono kwa mazingira wezeshi ambayo tumeyaweka. Wao nao wamefungua madarasa mengi sana katika shule zao za elimu ya awali. Tunawahitaji sana walimu hao wa elimu ya awali. Waandike barua zao kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nafasi hizo tunazo tutawapatia.

Wale walimu wa Chekechea siyo walimu wa Elimu ya Awali na dhamana ya mafunzo ya Elimu ya Chekechea, Sheria Na. 21 ya Mtoto imetoa mamlaka ya mafunzo ya chekechea kwa Kamishina wa Ustawi wa Jamii ambaye anasajili pia vyuo vya Ualimu wa Elimu ya Chekechea na Vituo vya Chekechea.

Kama wako walimu hao vituo viko vingi, jumla 670 nchi nzima. Vyuo vya Elimu ya Awali navyo viko vingi, viko 17 kimoja kikiwa cha Serikali. Tunawahitaji walimu hawa wajitokeze mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yameisha na muda kwa kweli haupo upande wetu kabisa. Kwa haraka haraka naomba niwatambulishe wageni tulionao katika Ukumbi wa Bunge.

Tunaye Balozi wa India hapa nchini, Shri Debnath Shaw, *Indian Ambassador to Tanzania,* karibu sana. Yupo pia Afisa kutoka Ubalozi wa India, Ndugu, G.K Pant, karibu sana.

Ninao wageni wangu maalum kutoka Kongwa ambao ni machifu, wamekuja kutembelea hapa na kuleta salamu kwa niaba ya wenzao. Mzee Tumaini Ndumula, Mzee Ngeke Nyamwanji na Mzee Jackson Sekwao. Karibuni sana wazee wangu, muwaambie Kongwa kijana wenu niko salama. Ahsanteni sana, kaeni. (*Makofi*)

Pia nina wageni 22 kutoka Dayosisi ya *Central Tanganyika* kutoka kule *District Designated Hospital* ya Mvumi pamoja na *Diocese of Central Tanganyika, Makey House Dodoma*. Pale mlipo wale wageni 22 naomba msimame. Wako pale karibuni sana. Wanajishughulisha sana na masuala ya afya na hasa matatizo ya macho kwa nchi nzima. Karibuni sana leo mjifunze masuala ya Bunge. (*Makofi*)

Kwa ajili ya mafunzo kuna wanafunzi wa Vyuo vya *UDOM* na *Saint John,* pale mlipo karibuni sana. Hivi ni vyuo vikuu vilivyo po hapa mjini Dodoma na vyenye sifa kubwa sana hapa nchini. Tunakaribisha vijana wetu mjifunze masuala ya Bunge.

Wanafunzi na walimu kutoka shule ya Sekondari ya Chilonwa kule kwa Mzee Chibulunje. Ahsante sana, Walimu na wanafunzi wote kutoka kule Chilonwa. Naona Mzee Chibulunje amefanikiwa kuleta mpaka na walimu kutoka nje ya nchi. Karibuni sana na ahsanteni sana Wanafunzi na Walimu kutoka Chilonwa. (*Makofi*)

Wanafunzi kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari *cha Dar es Salaam City College,* pale mlipo. Ahsanteni sana hapo mlipo. (*Makofi*)

Pia tuna madaktari wetu na timu nzima ya wauguzi na kadhalika waliokuja kwa ajili ya kufanya vipimo mbalimbali na kuwashughulikia Waheshimiwa Wabunge kwa umahiri mkubwa sana. Madaktari pale mlipo, karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge wanashukuru sana kwa huduma ambayo mmeitoa kwa wiki nzima, wanaomba wakati mwingine mkipata nafasi mtutembelee tena hapa Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa makofi hayo.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Iddi Azan anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kesho tarehe 1 Juni, 2013 kwenye Uwanja wa Jamhuri, kutakuwa na michezo ya mpira wa miguu na pete na *combine* ya *NSSF.*

Kwa hiyo itakuwa *NSSF* na Bunge kwa maana ya *football* na *netball.* Michezo hiyo itaanza Saa Kumi jioni na itaoneshwa *live* na Kituo cha Televisheni cha *Star TV.*

Mpira wa kesho ni *live,* utaonyeshwa na *Star TV,* mnakaribishwa wote kushangilia timu yetu ya Bunge. Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge Kamati ya Ufundi chini ya Profesa Majimarefu imeshamaliza kazi yake. (*Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 7.00, ukumbi Na. 227.

Katibu Msaidizi wa Wabunge Wanawake wa CCM Bungeni, Mheshimiwa Kisangi anaomba leo tarehe 31 saa saba mchana pawe na kikao cha Wabunge wote wanawake wa CCM katika ukumbi wa Pius Msekwa, mnaombwa kuhudhuria. Narudia tena akinamama wote Wabunge wa CCM mnaombwa saa saba ukumbi wa Msekwa.

Pia naomba niwatangazie watendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi pale mlipo naomba msimame. Ahsante sana Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote karibuni sana tunawatakia kila la kheri kwenye shughuli yenu ya leo hapo baadaye. *(Makofi)*

Pia kwa kumalizia naomba niendelee na masuala ya utaratibu. Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka jinsi siku ya jana ilivyokuwa haikwenda vizuri na wakati naahirisha Bunge niliomba Kamati ya Maadili waende wakutane ili watushauri namna gani tunaweza tukatoka pale tulipokuwa tumekwama jana. Kwa hiyo, kwa fursa hii ninamwomba Mheshimiwa Chiligati ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo lakini aliyekuwa anaongoza kikao hicho jana alitaarifu Bunge nini kimejiri na ushauri wao kwetu ni jambo gani.

Mheshimiwa Chilligati, kwa heshima nakuomba tafadhali.

**MHE. JOHN Z. CHILLIGATI (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, napenda kuwasilisha taarifa ya kikao cha jana ambacho kilihusu malalamiko ya Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim dhidi ya sehemu ya taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshiwa Wenje kuhusu bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuahirisha kikao cha jana jioni, uliitaka Kamati yetu ikae na iendelee kushughulikia suala hili. Kamati ilikaa na tuliamua tushirikishe marafiki wa Kamati kutoka vyama ambavyo vilikuwa vinahasimiana. Kwa hiyo, tulimwalika Mheshimiwa Mbowe akiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kama rafiki wa Kamati. Vilevile tulimwalika Mheshimiwa Hamad Mbarouk ambaye ni Kaimu Mwenyekiti wa *Caucus* ya CUF humu ndani ya Bunge. Vilevile tulimwalika Mheshimiwa Mary Nagu ambaye ni Kaimu Mnadhimu wa upande wa Serikali. Kwa hiyo, kwa hivi vyama, CHADEMA tulikuwa na Mheshimiwa Mbowe na Mheshimiwa Arfi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, lakini pia ni Mjumbe wa Kamati. Kwa madhumuni ya shauri hili tulimruhusu awe upande wa CHADEMA. Vilevile tulikuwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah, yeye ndiye Mnadhimu wa Wabunge wa *CUF* ndani ya Bunge, ni Mjumbe wetu lakini naye kwa madhumuni wa suala hili tulisema awe upande wa *CUF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwapa notisi fupi lakini wote walifika kwa muda mfupi kuonyesha kwamba na wenyewe jambo hili walilitilia maanani. Mazungumzo yetu yaliongozwa, kwanza tulisema hapa tutangulize maslahi ya nchi badala ya vyama vyetu. Vilevile tuzingatie suala la kurejesha mshikamano na upendo ndani ya Bunge kwa sababu katika zogo hili maneno yasiyofaa yalirushwarushwa kila upande, kwa hiyo tulikuwa na jukumu la kurejesha amani na upendo na mshikamano ndani ya Bunge. Vilevile tulizingatia suala la kukwamua bajeti ya Wizara hii ya Mambo

ya Nje ambayo ni dhahiri kwamba ilikuwa imekwama siku ya jana. Haya ndiyo yaliyotuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala ulivyoendelea, upande wa CHADEMA ukiongozwa na Mheshimiwa Mbowe alisisitiza mambo makubwa mawili pale kwenye Kamati. Kwanza, alisema walichokiandika kwenye hotuba yao kwamba *CUF* ni wanachama wa *Liberal International,* ni sahihi na kwamba hawa Waliberali moja ya mambo ya msingi katika sera zao ni uhuru wa mtu binafsi, hiyo ni pamoja na mambo ya ushoga, usagaji na kadhalika. Kwa hiyo, akasema sera hii ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, kwa msingi huu hawajafanya kosa na wao walikuwa wanazungumzia masuala ya U-*liberali* na sera za U-*liberali* hawakukusudia kabisa kuihusisha *CUF* katika hili. Kwa hiyo, wakasema wenyewe wako sahihi na hawako tayari kuomba radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kubwa alilolisisitiza kwenye Kamati Mheshimiwa Mbowe kwamba katika zogo hili *CUF* na wenyewe wameidhalilisha CHADEMA. Wameidhalilisha kwanza kwa kumtukana Mheshimiwa Wenje matusi mazitomazito, lakini pili hotuba yao baadhi ya Wabunge wa *CUF* waliichanachana na kuitupa, wakasema hili nalo lizungumzwe na wenyewe limewaumiza, limewakera, limewaudhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Mbowe alisema kwa sababu ya vurugu za *CUF* kikao kiliahirishwa, hili nalo alisema si sawa, nalo vilevile ni kosa lizungumzwe. Kwa hiyo, hayo ndiyo makubwa mawili aliyoyasema Mheshimiwa Mbowe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *CUF*, Mheshimiwa Mbarouk alikiri kwamba ni kweli *CUF* ni wanachama wa *Liberal International,* huo Umoja wa Waliberali lakini alisema si sera zote za *Liberal International CUF* wanazikubali, si zote, kuna zingine hawamo, hawazikubali, likiwemo hili la ushoga na mambo ya usagaji kwamba wao halimo kwenye Katiba yao wala halimo kwenye maandishi yao yoyote, kwani hawalikubali na isitoshe

Tanzania kama nchi ilishalitolea msimamo suala hili pale tulipoambiwa na Mheshimiwa Cameroon kwamba nchi zinazoendelea zikitaka msaada basi ziunge mkono masuala haya; Tanzania ilitoa msimamo kwamba masuala haya hayakubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndio *CUF* wanasema kama nchi ilishatoa msimamo huo kwamba masuala haya hapa Tanzania hayakubaliki, inakuwaje tena yanaingizwa kwenye hotuba ya CHADEMA, halafu na sisi tunahusishwa? Kwa hiyo, wakasema hapa sisi kama chama *CUF,* tumepakwa matope, tumedhalilishwa, kwa hiyo, maneno hayo yafutwe na tuombwe radhi. Haya ndiyo yalikuwa makubwa ambayo *CUF* waliyasema kwenye kikao kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao kiliendelea kwa muda mrefu, tulikaa mpaka karibu saa 2.30 usiku kuanzia saa 11.00 jioni lakini baadaye tukaja kupata maelewano. Muafaka ambao tuliupata baada ya mazungumzo marefu sana ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kuhusu CHADEMA, tulikubaliana kwamba ili kujenga mshikamano ndani ya Bunge na kuondoa uhasama ndani ya Bunge na kwa vile yale maneno ya kwenye hiyo hotuba yaliumiza chama cha *CUF*, kwa hiyo, yale maneno ya sehemu ya tatu ya hotuba yao yote yaondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana hivyo na Kiongozi wa CHADEMA aliafiki hivyo kwamba yale maneno yanaondolewa, sehemu yote ya tatu, yanaanzia ukurasa wa 7 – 9, yote yale yaondolewe ili kuleta mshikamano, kuondoa uhasama na ili kuleta umoja ndani ya Bunge yaondolewe kwa misingi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwamba CHADEMA waiombe radhi *CUF* kwa sababu yale maneno, ingawa yanafutwa lakini tayari yalishaleta maumivu makubwa na uhasama mkubwa kati ya *CUF* na CHADEMA. Kwa hiyo, anaomba radhi kwa yale maneno ambayo yaliwakwaza

wenzetu wa *CUF*. Vilevile tulikubaliana kwamba Mheshimiwa Mbowe aombe radhi kwa Naibu Spika kwa sababu Naibu Spika jana alipotoa *ruling* kwamba sasa Mheshimiwa Wenje aombe radhi, afute yale maneno na ndipo aendelee na hotuba yake, Mheshimiwa Wenje hakufanya hivyo, nia ni kudhalilisha Kiti cha Spika, ni kosa. Kwa hiyo, kwa kosa alilolifanya Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Mbowe ataomba radhi ili vilevile kujenga tu heshima ya Bunge letu kwamba Kiti cha Spika lazima wakati wowote kiheshimiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ataomba radhi kwa Bunge lote kwa sababu jana Wabunge tumewasumbua sana. Kwa hiyo, nalo vilevile kiungwana tu kwamba jamani samahani tuliwasumbueni lakini sasa limekwisha, tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *CUF*, muafaka ambao tuliufikia jana usiku ni kwamba Mnadhimu wa *CUF,* awaombe radhi Wabunge wa CHADEMA kwa sababu ya lugha za matusi zilizotoka upande wa *CUF* kwenda kwa Mheshimiwa Wenje, nalo vilevile si jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile awaombe radhi CHADEMA kwa kile kitendo tu cha kuchanachana ile hotuba yao na kuitupa, si uungwana na iliwaudhi CHADEMA kuona kwamba hotuba yao inachanwachanwa na kutupwa, hilo sio uungwana hivyo waombe radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mnadhimu wa Wabunge wa *CUF* amwombe radhi Naibu Spika kwa zile vurugu walizozifanya mpaka Naibu Spika akaahirisha kikao. Hilo nalo si uungwana, hivyo tulisema basi na wao wawe waungwana wamwombe radhi Naibu Spika kwa zile fujo ambazo zilipelekea Bunge likaahirishwa hapo jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mnadhimu wa Wabunge wa *CUF* naye aliombe radhi Bunge kwa ule usumbufu ambao Wabunge mliupata kwa siku ya jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo tuliyoafikiana na nina imani kwamba pande zote mbili, ule moyo wa maridhiano waliounyesha jana usiku, watakuwa waaminifu na waungwana watamke humuhumu ndani yale tuliyokubaliana na ni haya ambayo niliyoyasoma, nina imani watafanya hivyo. Siamini kwamba kuna mtu usiku huu atakuwa ameshageuka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini kwamba usiku huu atakuwa ameshageuka halafu ayakane yote haya ambayo nimeyasema. Haya ndiyo tuliyokubaliana, naamini wenzangu watakaposimama watakubali haya haya ndiyo tuliyoyasema na sisi Kamati tunaamini kama haya yakitekelezwa, ugomvi utakuwa umekwisha, amani imerudi na tutasonga mbele kama timu moja, Bunge moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Chilligati na Kamati yako kwa kazi nzuri na kwa kweli wamefanya kazi mpaka usiku kwelikweli na mchana wote jana walikuwa kwenye kazi hii hii, tunawashukuru sana Kamati ya Maadili kwa hatua hiyo. Sasa kama haya ni kweli tuyathibitishe katika utaratibu huu ufuatao. Nitamwomba Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah atakuwa wa kwanza halafu na wengine watafuata, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah kuhusu yaliyosemwa.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH - MNADHIMU WA *CUF*:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia leo hii kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Chama cha *CUF,* sina budi nikupe pole, lakini pia nikupongeze kwa hatua uliyochukua kuweza kulidhibiti Bunge kuendesha shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende pia kuwapa pole, Mheshimiwa Waziri wa Mambo wa Nchi za Nje na Ushirikiano

wa Kimataifa na Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa usumbufu mkubwa walioupata tarehe 30 Mei, 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwape pole Wabunge wenzangu wote waliokosa nafasi ya kujadili hotuba hii tarehe 30 Mei, 2013 kutokana na mzozo uliotokea hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, niipongeze Kamati yangu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikiongozwa na Kapteni Mstaafu Chilligati kwa hekima kubwa iliyofanya kufikia ufumbuzi wa suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rajab Mbarouk, Mbunge wa *CUF* ambaye alikuwepo katika Kamati yetu lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Mbowe ambaye pia naye alikuwepo katika Kamati yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Mary Nagu kwa kujumuika na sisi katika kufikia maamuzi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitendo kilichodhahiri kwamba chama cha CHADEMA, kwa makusudi au kwa bahati mbaya au kwa kutokuelewa, kukidhalilisha chama cha *CUF* katika hotuba yake. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, napenda nimpongeze kwa kusimama kwa niaba ya *CUF* kuomba utaratibu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chama cha *CUF* katika kufikia maamuzi haya kiliweka mbele maslahi ya wananchi wake na maslahi ya Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze chama cha CHADEMA katika kikao chetu kwa mambo matatu. Jambo la kwanza, kujua kosa lao katika hotuba yao. Jambo la pili, kukubali kuyafuta maneno yote yaliyoidhalilisha *CUF* katika hotuba yao. Tatu, kukubali kuomba radhi kwa chama cha *CUF* na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hotuba ya CHADEMA iliidhalilisha *CUF,* ni dhahiri Waheshimiwa Wabunge wa CUF damu ilichemka na ikalazimika kutoa maneno ambayo hayastahiki kutolewa Bungeni. Napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Chama cha *CUF*, kuwaomba au kutoa samahani kwa wale wote walioguswa na maneno haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme kuwa Wabunge wote tufanye kazi kwa kulijenga Taifa letu. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya *CUF*. Sasa ninaomba nimwite Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba ametufikisha hapa salama na alituongoza vizuri katika kikao chetu cha jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili kwa taarifa aliyoiwasilisha mahali hapa. Katika *spirit* ya *reconciliation* yaani katika dhamira ya usuluhisho na kurejesha amani ndani ya Bunge letu na mshikamano wetu kama Wabunge, sina sababu ya kuhoji chochote katika mawasilisho aliyoyafanya Mheshimiwa Chiligati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, niombe tu kurekebisha jambo moja dogo sana katika mambo aliyozungumza Mheshimiwa Chiligati. Kwa kutambua kuwa miongoni mwa Wajumbe ambao walialikwa katika kikao kile tulikuwa vilevile na Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema ambaye naye mchango wake ulikuwa ni muhimu na ushauri wake ulikuwa ni wa msingi sana. Kwa hiyo, kibinafsi, napenda kutambua uwepo wa Mheshimiwa Mrema kwenye kikao kile kama Kiongozi wa Upinzani, kama Kiongozi mzoefu

katika Taifa ambaye naye mchango wake ulitusaidia kufika tulikofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mnadhimu, Kiongozi mwenzetu kutoka upande wa chama cha Wananchi *CUF*. Nilipokwenda kwenye Kikao kile ambacho binafsi ninakiheshimu, nilitanguliza kusema jambo moja ambalo ninaomba nilirudie mahali hapa. Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kauli ile haikuwa yake binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile ilikuwa ni kauli ya Kambi. Ndiyo sababu kama kauli ya Kambi ni lazima sisi wote tuwe na *collective responsibility* kama ambavyo naamini hata wenzetu upande wa Serikali kauli inayotolewa na Waziri siyo kauli binafsi ni Kauli ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kumtukana, kumdhalilisha, kumtusi Mheshimiwa Wenje kama vile jambo lile ni lake binafsi, ni dhahiri halikuwa jambo la kiungwana wala jambo la kistaarabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge wenzetu wa Chama cha Wananchi *CUF,* walionekana kukwazika sana na sehemu ya ile hotuba ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Wenje. Kwa kweli ni wajibu tu kwamba *whether* maneno yale yana ukweli au hayana ukweli, walikwazika. Kwa kukwazika huko ni ustaarabu kukubaliana kuombana radhi kwa sababu haitakuwa na maana yoyote kama tutafanya vyama vyetu ni vya muhimu kuliko Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyama vya siasa hivi ni vyombo vya wananchi. Ni vyema tukaelewa vilevile kuwa tunapoparagana huku ndani ya Bunge, Taifa nalo linakuwa katika sintofahamu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunalazimika kukubali katika wakati mwingine kumeza **fried** zetu kama

walivyofanya wenzangu wa *CUF* na sisi tutafanya hivyohivyo kwa sababu wote tunajenga nyumba moja, tusigombane kwa sababu ya vito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo makubwa katika nchi hii ya kuzungumza na tukatofautiana katika misimamo kuliko hili jambo. Jambo hili haliwezi kuwa lina msingi mzito kuliko ulazima wetu wa kujenga umoja wa Kitaifa na kujadili yale mambo ambayo tunafikiri yana maslahi zaidi kwa nchi yetu. Vilevile katika mikakati yote ya harakati, wanazungumza kwa lugha ya kijeshi kwamba tu-*withdraw,* labda pengine nisiende mbali sana lakini niseme tu kwamba unaweza kujitoa katika mstari wa mbele katika jeshi ni sehemu ya mkakati tu wa kazi na kwa maana hiyo, niseme kabisa kwa wenzangu wa *CUF* wala wasifikiri kuwa ninajaribu kuyumbisha maneno mahali hapa hapana, sijaribu kutunga maneno wala kuyumbisha maneno, napenda niwaombe radhi sana Waheshimiwa wenzangu wa Chama Cha Wananchi *CUF* na ninapenda vilevile kumwomba radhi Mheshimiwa Naibu Spika, tumeairisha Bunge mara mbili bila sababu za msingi. Tukitafuta nani ni mshindi, wala haitausaidia sisi kama Bunge wala sisi kama Taifa. Nawaomba sana wakubali *apology* yetu, tuendelee kufanya kazi ndani ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote vilevile poleni sana kwa usumbufu wote ambao ulijitokeza katika siku ya jana. Tumejikuta tunatafakari tulikoangukia pengine tumepata *wakeup call* ya kutafakari tulikojikwaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu na ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana Kamati ya Maadili, niwashukuru sana Wabunge wa Chama Cha CUF na hasa Msemaji wao wa leo Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah lakini vilevile niwashukuru Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na hasa kwa

maneno mazuri sana ya kujenga yaliyosemwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe. Natumaini kazi waliyoifanya kutwa nzima ya jana inatuweka mahali pazuri sana. Mimi niseme tu kuwa sisi wote humu ndani ya Bunge, tunamwamini Mwenyezi Mungu na katika kufanya hivyo mara nyingi tunafanya toba kwa makosa mbalimbali, sisi Wakristo tunasema kwa makosa ambayo tumeyafanya kwa mawazo, kwa maneno, kwa matendo au kwa kutotimiza wajibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ninatumaini katika yote haya tumejifunza, tutulie, tujirekebishe, Taifa zima linatutazama, sisi ni mfano wa jamii ya Tanzania, tuwe makini na yale ambayo tunayatamka Bungeni sote kabisa kama ambavyo Kiti kimekuwa kikisisitiza tangu tumeanza Bunge hili la kumi. Katika eneo ambalo Bunge hili limelaumiwa sana, ni kauli zetu za humu Bungeni. Naendelea kuwaasa Waheshimiwa Wabunge wote kabisa, kujiepusha na kauli ambazo kwa kweli hata unapoiweka unajua kabisa kuwa nitawaudhi watu wengine, nyingine zimevumiliwa huko nyuma, huenda zisivumiliwe huko mbele lakini tujitahidi kuzirekebisha, ziko nyingi sana za kirejareja, nyingi sana, tuzingatie makubaliano.

Kesho kama shughuli ya kutengua Kanuni itakayofuata muda mfupi ujao itakubalika, tutakutana kesho, matarajio yetu na mapendekezo ni kwamba kesho tumalize Wizara hii ya Mifugo na Wizara ya Mambo ya Nje. Kwa hiyo, ni matumaini yangu ni kwamba hiyo sehemu ya tatu haitasomwa, hayatajitokeza yale ya siku zile ambapo tunakubaliana kitu fulani kisifanyike halafu watu wanaenda kufanya kitu kilekile na kama mambo mengine yote yatakwenda kama tulivyokuwa tumekubaliana.

Baada ya maelezo hayo, sasa nimwite Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ili atupatie pendekezo alilo nalo.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kusema na kwa sababu umesema lakini ninaomba pia kusoma utenzi wa 154 wa Kitabu cha Mfasihi Mkuu wa nchi hii Shaaban Robert, aliandika tarehe 5/4/1958, miaka 55 iliyopita alisema:-

*"Chuki jambo la udhia,*
*Siyo jema kutaradhiwa,*
*Na kama litadhiriwa,*
*Tutamezwa na ushenzi,*
*Siyo vyema kurudi tena*
*Ushenzi wema hauna*
*Lakini dawa hapana*
*Ila sera ya mapenzi ''*

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya yanatoka katika kitabu cha Mapenzi Mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa kwa hili ambalo limefanyika asubuhi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, kwa mujibu wa Kanuni ya 153 (1) na kwa shabaha maalumu, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge wa kushughulikia bajeti ya Serikali pamoja na shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa, umepangwa kumalizika tarehe 28/6/2013;

Na kwa kuwa ratiba ya shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu wa Kumi na Moja, imepangwa kwa kuzingatia Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka huu;

Na kwa kuwa awali uwasilishaji wa majadiliano ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ulipangwa uwe

kwa siku moja jambo ambalo lingeruhusu wachangiaji wachache sana;

Na kwa kuwa ni ukweli usiopingika kuwa Wizara hii inahusisha sekta mbili za Mifugo na Uvuvi ambazo zinawalenga wananchi walio wengi moja kwa moja moja;

Na kwa kuwa katika Kikao cha Kamati ya Uongozi wa Bunge kilichofanyika katika Ukumbi wa Spika tarehe 30/5/2013, Wajumbe wa Kamati hiyo waliohudhuria waliazimia kuliomba Bunge likubali kuiongezea Wizara hii siku moja kwa kufanya kazi siku ya Jumamosi tarehe 1/6/2013 yaani kesho;

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka huu, Bunge haliwezi kukutana na kufanya kazi siku za Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko;

Na kwa kuwa ili kuliwezesha Bunge kuweza kukutana siku ya Jumamosi yaani kesho tarehe 1/6/2013, ni lazima Bunge litengue Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka huu kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1).

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Moja, Kanuni ya 28 (15) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28 (15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kuwa Bunge halitakutana siku za Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko, itenguliwe na badala yake Bunge lako Tukufu likutane siku ya Jumamosi, tarehe 1/6/2013 yaani kesho kuanza saa tatu asubuhi hadi saa nane mchana, isipokuwa kwamba siku hiyo hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kufikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sote tumeafiki, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kesho siku ya Jumamosi sote tufike, tujitahidi tufanye kazi zilizoko Mezani kwa siku ya kesho. Kama nilivyosema tunaweza kabisa kwa uendeshaji bora hapa tukamalizika shughuli za Wizara ya Mifugo saa tano kamili, tutawaomba tumalizie masaa matatu yatakayobakia kwa Wizara ya Mambo ya Nje ili pasiwe na kiporo tena ili Jumatatu tuendelee na ratiba zetu kama kawaida.

Baada ya hatua hiyo, sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge nimkaribishe Mheshimiwa Mwenyekiti Jenista Muhagama aweze kuendelea na shughuli zilizoko Mezani.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Muhagama) Alikalia Kiti*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi kuendelea kupoteza muda, hiyo Miongozo tutaisikiliza baadaye, Katibu!

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali - Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

**MWENYEKITI:** Naomba nimwite Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti

wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2012/2013 na mwelekeo wa kazi za Wizara kwa mwaka 2013/2014. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/ 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zao za kuongoza, kusimamia na kuendeleza amani, utulivu na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mheshimiwa Mbunge mwenzetu; Hayati Salim Hemed Khamis aliyekuwa Mbunge wa Chambani. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa jimbo alilokuwa analiwakilisha. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwakumbuka wananchi wenzetu waliopoteza maisha kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushauri, maoni na ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maandalizi ya bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri, mapendekezo na maoni ya

Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi kwa hotuba yake nzuri yenye kutoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sekta za mifugo na uvuvi na changamoto zilizopo. Sekta ya mifugo ni moja kati ya sekta zilizopewa umuhimu katika kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Nchini (MKUKUTA II). Mifugo hutoa ajira, lishe, nishati, mbolea na hutumika kama wanyamakazi na benki hai. Baadhi ya mifugo ikiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, nguruwe ni chanzo cha mapato ya haraka wakati wa hali ya ukame na njaa, hususan maeneo ya vijijini. Aidha, mifugo na bidhaa zake huokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza mazao hayo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012, sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 3.9 mwaka 2011 na kuchangia asilimia 4.6 katika pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2011. Kulingana na takwimu zilizopo, idadi ya mifugo nchini inafikia ng'ombe milioni 22.8, mbuzi milioni 15.6 na kondoo milioni 7.0. Pia, wapo kuku wa asili milioni 35.5, kuku wa kisasa milioni 24.5 na nguruwe milioni 2.01. Ulaji wa mazao ya mifugo kulingana na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*, 2011) ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu mmoja kwa mwaka. Kwa upande wa nchi yetu, viwango vya ulaji wa mazao hayo kwa sasa ni wastani wa kilo 12 za nyama, lita 45 za maziwa na mayai 75 kwa mtu mmoja kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uvuvi hufanyika katika maeneo ya maji chumvi na maji baridi. Nchi yetu ina ukanda wa pwani wa bahari wenye urefu wa kilometa 1,424 ambao umegawanyika katika eneo la Maji ya Kitaifa

*(Territorial Sea)* lenye ukubwa wa kilometa za mraba 64,000 na eneo la Bahari Kuu lenye ukubwa wa kilometa za mraba 223,000. Eneo la maji baridi linajumuisha maziwa makuu matatu ambayo ni; Ziwa Victoria (kilometa za mraba 35,088), Ziwa Tanganyika (kilometa za mraba 13,489) na Ziwa Nyasa (kilometa za mraba 5,700), maziwa ya kati na madogo 29, mito na maeneo oevu. Aidha, ukuzaji wa viumbe kwenye maji unafanyika kwenye maeneo hayo na maeneo ya nchi kavu yenye maji ya kutosha ambapo kuna mabwawa 20,134 ya ufugaji samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi huchangia katika upatikanaji wa lishe bora, ajira, kipato kwa wananchi, pato la Taifa na hivyo kuchangia katika kuondoa umaskini. Sekta hii imekua kutoka asilimia 1.2 mwaka 2011 hadi asilimia 2.9 mwaka 2012 na kuchangia katika pato la Taifa kwa asilimia 1.4. Vilevile idadi ya wavuvi wadogo imeongezeka kutoka 177,527 mwaka 2011/2012 hadi wavuvi 182,741 mwaka 2012/2013 na zaidi ya wananchi milioni 4.0 wameendelea kutegemea shughuli za uvuvi katika kujipatia kipato kutokana na biashara ya samaki, uchakataji wa mazao ya uvuvi, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi na biashara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013 sekta za mifugo na uvuvi zimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Uwekezaji mdogo wa Serikali na sekta binafsi katika sekta za mifugo na uvuvi na hasa katika uzalishaji, uvunaji, usindikaji na masoko ya mazao ya mifugo na uvuvi;

(ii) Kutopatikana kwa mikopo ya kutosha na yenye masharti nafuu kwa ufugaji na uvuvi ikilinganishwa na mahitaji yao;

(iii) Kasi ndogo katika kuainisha, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji endelevu ili kudhibiti kuhamahama kwa mifugo na hivyo kupunguza migogoro

baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa mazingira na ueneaji wa magonjwa ya mifugo;

(iv) Matumizi madogo ya mbegu bora za mifugo, pembejeo na huduma ya uhimilishaji pamoja na uhaba wa mbegu bora za samaki;

(v) Ukosefu wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi na hasa katika maeneo ya vijijini;

(vi) Kuenea kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo, hususan magonjwa ya mlipuko kutokana na uwezo mdogo wa kuyakabili kutokana na uhaba wa wataalam na vitendea kazi;

(vii) Uhaba wa maafisa ugani wa mifugo na uvuvi ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam hao pamoja na matumizi madogo ya elimu na teknolojia sahihi kwa ufugaji na uvuvi endelevu; na

(viii) Ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuzifanya sekta za mifugo na uvuvi kuwa endelevu zenye uzalishaji bora, zinazoendeshwa kibiashara na kuzingatia hifadhi ya mazingira kupitia sera, mikakati na programu zifuatazo:-

(a) Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006, Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2011) na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo ya miaka mitano (2011/12 – 2015/16) ambazo zinalenga kuongeza ukuaji wa sekta kutoka asilimia 3.1 mwaka 2012 hadi kufikia 4.5 kwa mwaka ifikapo mwaka 2016.

(b) Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake ya mwaka 1997 na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi ya miaka mitano (2011/12 – 2015/16) ambazo zinalenga kuimarisha

usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kuongeza ukuaji wa sekta kutoka asilimia 2.9 mwaka 2012 hadi kufikia 5.3 kwa mwaka ifikapo mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2012/2013 na mwelekeo wa Bajeti ya mwaka 2013/2014. Ukusanyaji wa Mapato. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 18,207,055,000.00. Kati ya hizo, shilingi 8,049,864,000.00 ni kutoka sekta ya mifugo na shilingi 10,157,191,000.00 ni kutoka sekta ya uvuvi. Hadi kufikia mwezi tarehe 21 Mei, 2013, kiasi cha shilingi 11,935,010,942.71 kimekusanywa na Wizara ikiwa ni sawa na asilimia 65.6 ya lengo. Sababu kubwa ya kupungua kwa maduhuli hayo ni kutokana na mtikisiko wa uchumi kwenye soko la samaki na mazao ya uvuvi la kimataifa pamoja na kupungua kwa maduhuli yatokanayo na mauzo ya ngozi ghafi nje ya nchi na kuwezesha kiasi kikubwa cha ngozi kusindikwa hapa nchini. Kati ya hizo, shilingi 4,721,898,802.72 zimekusanywa kutoka sekta ya mifugo (asilimia 58.6 ya lengo) na shilingi 7,213,112,140.00 zimekusanywa kutoka sekta ya uvuvi (sawa na asilimia 69.7 ya lengo). Katika mwaka 2013/2014, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 18,584,074,280.00. Kati ya hizo, shilingi 8,247,973,280.00 zitatoka kwenye sekta ya mifugo na shilingi 10,336,101,000.00 zitatoka kwenye sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya fedha. Katika mwaka 2012/2013, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 54,566,124,000.00. Kati ya hizo, shilingi 40,726,641,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 13,839,483,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 13,959,071,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi *(PE)* na shilingi 26,767,570,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengine *(OC).* Vilevile, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, shilingi 4,000,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 9,839,483,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 20 Mei, 2013, jumla ya shilingi 34,428,187,941.05 (sawa na asilimia 63.09) zimetolewa. Kati ya hizo, shilingi 29,433,287,941.05 (sawa na

asilimia 67.3) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo shilingi 27,773,854,092.68 (sawa na asilimia 94.4) zimetumika na shilingi 4,994,900,000.00 (sawa na asilimia 36.1) zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi 2,843,009,324.18 zimetumika (sawa na asilimia 56.9). Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 18,320,198,135.00 zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 11,113,089,806.05 kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC).* Kati ya fedha za maendeleo, fedha za ndani ni shilingi 944,989,300.00 na shilingi 4,049,910,700.00 ni za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubunifu na utekelezaji wa Sera na Sheria za Sekta. Wizara imeendelea kuratibu, kupitia na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mikakati na programu mbalimbali za kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kusambaza na kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake (1997). Jumla ya nakala 1,000 za Sera ya Taifa ya Mifugo (2006) na nakala 500 za Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mkakati (1997) zimesambazwa kwa wadau mbalimbali hapa nchini. Pia, elimu kwa wadau imeendelea kutolewa kupitia maadhimisho mbalimbali ya kitaifa ya wadau pamoja na mikutano ya kitaaluma ikiwemo sikukuu ya NaneNane, Siku ya Uvuvi Duniani, Siku ya Chakula Duniani na Wiki ya Uhamasishaji Unywaji Maziwa. Vilevile, Wizara imekamilisha kutafsiri Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2011) kwa lugha ya Kiswahili na kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake (1997).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kupitia sheria za sekta ya mifugo na uvuvi ili ziendane na Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) na kuboresha mazingira ya kibiashara. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:-

(i) Kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria za Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Sura 146, Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Sura 280 na Sheria ya Uvuvi Sura 279;

(ii) Kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mbari Bora za Wanyama *(Animal Breeding Act);*

(iii) Kuandaa marekebisho ya Kanuni ya Biashara ya Ngozi *(Trading in Hides, Skins and Leather Regulations, 2010)* chini ya Sheria ya Ngozi Sura 120;

(iv) Kuandaa Kanuni ya Viwango vya Tozo za Maabara za Uvuvi chini ya Sheria ya Uvuvi Sura 279 yenye GN. Na. 237, Kanuni ya Uingizaji na Uuzaji wa Maziwa na Bidhaa za Maziwa nchini chini ya Sheria ya Maziwa Sura 262 yenye GN Na. 329 na Kanuni tano (5) chini ya Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura 180 zenye GN. Na. 54, 55, 56, 57 na 58; na

(v) Kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Wanyama Sura 180 na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu sera, sheria na kanuni za sekta za mifugo na uvuvi. Aidha, itachapisha nakala 1,000 za Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2011) na kuzisambaza kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji. Pia, itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake (1997) na kuandaa Mkakati wa utekelezaji. Vilevile, Wizara itaendelea kufanya tafsiri ya Sheria ya Ustawi wa Wanyama Sura 154, Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Sura 156, Sheria ya Veterinari Sura 319, Sheria ya Biashara ya Ngozi Sura 120, katika lugha ya Kiswahili. Aidha, Wizara itakamilisha mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mbari Bora za Wanyama *(Animal Breeding Act)* na kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Ukuzaji Viumbe kwenye Maji *(Aquaculture Act).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa Sekta ya Mifugo. Uzalishaji na Biashara ya Mifugo na Mazao yake. Maziwa, katika mwaka 2012/2013, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia 3.6 kutoka lita bilioni 1.85 mwaka 2011/2012 hadi lita bilioni 1.92. Aidha, maziwa yanayosindikwa kwa siku yameongezeka kutoka lita 130,400 mwaka 2011/

2012 hadi lita 135,300 mwaka 2012/2013. Katika mwaka 2013/ 2014, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuimarisha ukusanyaji na usindikaji wa maziwa ili kuongeza usindikaji wa maziwa kufikia lita 160,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba ya Uzalishaji Mifugo ya Serikali yameendelea kuboreshwa kwa kupatiwa vitendea kazi ili kuongeza uzalishaji ambapo katika mwaka 2012/2013, Wizara imenunua ng'ombe wazazi 109 kwa ajili ya mashamba ya Ngerengere (61), Sao Hill (33) na Mabuki (madume bora 15). Aidha, jumla ya mitamba 1,306 imezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wadogo katika maeneo mbalimbali nchini kutoka katika mashamba ya Mabuki (301), Sao Hill (198), Nangaramo (101), Kitulo (77), Ngerengere (125) na NARCO (504). Vilevile, Chama cha Ushirika cha Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa Tanga (TDCU), Umoja wa Wafugaji wa Nyanda za Juu Kusini (SHILDA) na mashirika ya *Heifer Project Tanzania (HPT) na Farm Friends* yamesambaza jumla ya mitamba 9,741.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya uzalishaji mifugo kwa kuboresha miundombinu na kuyapatia vitendea kazi pamoja na kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha na kusambaza mitamba bora kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza tija katika uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa, Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – *NAIC Usa River* pamoja na vituo vya uhimilishaji vya Kibaha, Dodoma, Lindi, Mwanza na Mbeya vimeimarishwa. Jumla ya dozi 168,000 za mbegu bora zimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji ambapo ng'ombe 98,340 walihimilishwa ikilinganishwa na ng'ombe 81,300 mwaka 2011/2012. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa wataalam 115 wa uhimilishaji. Pia, Wizara imeanza maandalizi ya ujenzi wa vituo vipya vya uhimilishaji vya Mpanda na Sao Hill.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuimarisha uhimilishaji nchini kwa kuzalisha

dozi 190,000 za mbegu bora za uhimilishaji, kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Uhimilishaji cha Sao Hill na Mpanda na kuanzisha kituo kingine cha Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyama - ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe. Katika mwaka 2012/2013, uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani 448,387 mwaka 2011/2012 hadi tani 466,047 (ng'ombe tani 299,581, mbuzi na kondoo tani 115,652 na nguruwe tani 50,814) mwaka 2012/2013. Aidha, idadi ya ng'ombe walionenepeshwa imeongezeka kutoka 132,246 mwaka 2011/2012 hadi ng'ombe 155,206 mwaka 2012/2013 Pia, katika juhudi za kuongeza uzalishaji na ubora wa nyama, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeandaa na kusambaza nakala 1,000 za Mwongozo wa Unenepeshaji Ng'ombe kwa wadau ili kuhamasisha unenepeshaji wa mifugo. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha minada ya upili na ya mipakani ambapo minada ya upili ya Pugu na Kizota (Dodoma) imekarabatiwa na ujenzi wa mnada wa Nyamatala (Misungwi) na mazizi katika mnada wa Kirumi umekamilika. Pia, Wizara imenunua mizani minne kwa ajili ya kusimika katika minada ya Kizota na Pugu kwa ajili ya kupima uzito wa mbuzi na kondoo na minada ya Lumecha (Songea) na Sekenke (Iramba) kwa ajili ya kupima uzito wa ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Halmashauri imeendelea kuratibu biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2012/2013, ng'ombe 1,105,037, mbuzi 872,908 na kondoo 190,265 wenye thamani ya shilingi bilioni 951.2 waliuzwa minadani. Aidha, ng'ombe 1,705, mbuzi na kondoo 1,003 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.16 waliuzwa nje ya nchi na tani 126.2 za nyama ya ng'ombe, 667.8 za mbuzi na 88.4 za kondoo ziliuzwa nje ya nchi zikiwa na thamani ya shilingi bilioni 28.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa nyama itaendelea kuhamasisha wafugaji, wafanyabiashara ya mifugo na wadau wengine kuwekeza kwenye ufugaji wa kisasa

ukiwemo wa ranchi na unenepeshaji ili kunenepesha ng'ombe 175,000. Aidha, Wizara itakarabati miundombinu ya minada ya upili ya Igunga, Weruweru na Meserani na kuendeleza ujenzi wa minada ya Kirumi na Longido. Pia, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi bora ya mizani na utunzaji wa miundombinu ya minada ya mifugo na kutoa mafunzo kwa wakusanyaji maduhuli 50 na wafanyabiashara wa mifugo 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa nyama katika Kampuni ya Ranchi za Taifa *(National Ranching Company - NARCO).* Katika mwaka 2012/2013, *NARCO* kupitia ranchi 10 za mfano za Kagoma, Kalambo, Kikulula, Kongwa, Mabale, Missenyi, Mkata, Mzeri, Ruvu na *West Kilimanjaro* imeendelea kuzalisha, kunenepesha na kuuza mifugo kwa ajili ya nyama. *NARCO* ina jumla ya hekta 230,384 zenye uwezo wa kuweka ng'ombe kati ya 80,000 na 90,000. Kwa sasa, Kampuni ina jumla ya ng'ombe 20,214, kondoo 1,650, mbuzi 744, farasi 45 na punda 40. Katika mwaka 2012/2013, *NARCO* imezalisha ndama 5,718 kutoka ng'ombe wazazi 8,997; kununua na kunenepesha ng'ombe 8,076 kutoka kwa wafugaji na kuuza ng'ombe 13,438 wenye thamani ya shilingi bilioni 3.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Kampuni imetoa hati miliki ndogo *(sub-lease*) kwa vitalu vinane (8) katika ranchi ya Usangu na kufikisha idadi ya hati miliki ndogo 83 kati ya 104 zinazotakiwa kutolewa. Aidha, imetoa ushauri na mafunzo ya kusimamia ufugaji wa kisasa kwa wawekezaji watanzania 70 ambao wamemilikishwa vitalu ndani ya Ranchi za Taifa, ambapo ranchi hizo zimewekeza ng'ombe 54,300, mbuzi 4,400 na kondoo 1,800. Katika mwaka 2013/2014, *NARCO* inatarajia kununua na kunenepesha ng'ombe 14,580 wenye thamani ya shilingi bilioni 4.5. Aidha, Kampuni itaendeleza ujenzi wa machinjio katika Ranchi ya Ruvu ambao ulisimama kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na migogoro iliyojitokeza kati ya wawekezaji na wananchi katika ranchi za *NARCO* Mkoani Kagera, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Wizara ya Ardhi Nyumba na

Maendeleo ya Makazi na vijiji vinavyozunguka ranchi hizo itapima upya ranchi hizo ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu. Kwa kuanzia ranchi ya Kagoma itapimwa upya katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhamasisha ufugaji wa kuku kibiashara. Kutokana na juhudi hizi, uzalishaji wa nyama ya kuku na mayai umeongezeka kutoka mayai bilioni 3.5 mwaka 2011/2012 hadi mayai bilioni 3.7 na nyama ya kuku kutoka tani 84,524 hadi tani 87,408 mwaka 2012/2013 Aidha, Wizara imeshirikiana na *Heifer International* Tanzania kusambaza majogoo 1,520 kwa wafugaji 322 waliopata mafunzo katika Wilaya za Bagamoyo, Kilosa na Mvomero ili kuboresha kuku wa asili na kuongeza uzalishaji. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ufugaji wa kuku wa asili na wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuvutia usindikaji wa ngozi ndani ya nchi, Serikali iliongeza ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi kutoka asilimia 40 hadi 90 au shilingi 400 hadi 900 kwa kilo kutegemea ipi ni kubwa. Kutokana na hatua hiyo, usindikaji wa ngozi uliongezeka kutoka vipande vya ngozi ya ng'ombe 166,773 kati ya Januari na Juni 2012 hadi vipande 343,860 kuanzia Julai hadi Desemba 2012. Aidha, usindikaji wa ngozi ya mbuzi na kondoo uliongezeka kutoka vipande 778,023 hadi vipande 1,173,875. Idadi ya ngozi zilizosindikwa na kuuzwa nje ya nchi ni vipande 969,060 vya ngozi za ng'ombe na vipande 2,582,525 vya ngozi za mbuzi na kondoo vyenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 50.9. Kutokana na mafanikio hayo, Serikali imedhamiria kuzuia uuzwaji wa ngozi ghafi nje ya nchi. Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza usindikaji katika viwanda vya ndani, kuongeza ajira na kuondoa utoroshaji wa ngozi ghafi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Viwanda na Biashara, Halmashauri 65 na Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania imeendelea kusimamia na kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na

Viwanda vya Ngozi Nchini kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha uzalishaji, uhifadhi na usindikaji wa ngozi unaozingatia hifadhi ya mazingira katika Halmashauri 65 zinazotekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi;

(ii) Kujenga vituo vinne vya kutolea mafunzo ya uendelezaji wa zao la ngozi katika Halmashauri za Ngorongoro, Rombo, Sumbawanga na Bariadi;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wagani 650 kuhusu mnyororo wa thamani wa zao la ngozi na wadau wa ngozi 20 kuhusu uzalishaji bora wa ngozi, uhifadhi na usindikaji;

(iv) Kutoa mafunzo kwa wadau 3,408 wakiwemo wachinjaji/wachunaji 911, wawambaji na wachambuzi wa madaraja 561, wasindikaji 67, wafanyabiashara 325 na wafugaji 1,505 ili kuboresha zao la ngozi; na

(v) Kuhamasisha uanzishwaji wa Chama cha Wazalishaji wa Ngozi nchini ambacho kitasimamia maslahi ya wazalishaji wa ngozi wakiwemo wafugaji, wachinjaji na wakusanyaji wa ngozi katika Halmashauri zote nchini. Wadau wameandaa rasimu ya Katiba ya uendeshaji wa chama chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi katika Halmashauri 75 ikijumuisha 10 zilizoongezwa mwaka huu kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kusimamia taratibu za kuhakikisha kuwa ngozi zote zinazozalishwa machinjioni zinafikishwa viwandani kwa ajili ya kusindikwa hapa nchini;

(ii) Kujenga vituo sita vya kutolea mafunzo ya uendelezaji wa zao la ngozi katika Halmashauri za Kahama Mji, Mpwapwa, Sengerema, Tarime, Urambo na Jiji la Mbeya;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wadau kuhusu uzalishaji, uhifadhi na usindikaji wa ngozi unaozingatia hifadhi ya mazingira; na

(iv) Kuimarisha Chama cha Wazalishaji wa Ngozi nchini kwa kukipatia utaalam ili kisimamie vyema maslahi ya wazalishaji wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya rasilimali za ardhi, maji na malisho kwa mifugo na utatuzi wa migogoro. Wizara imeendelea kuzihimiza Halmashauri kutenga na kuendeleza maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo kwa lengo la kuipatia mifugo malisho na kuepusha migogoro ya mara kwa mara kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, Wizara imeendelea kuzielekeza Halmashauri kufanya tathmini ya uwezo wa ardhi katika maeneo yao kwa kuzingatia Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura180 ili kuwezesha kufuga kulingana na uwezo wa eneo. Hadi sasa, jumla ya vijiji 781 vimepimwa na kati ya hivyo, vijiji 479 vimeainisha maeneo ya malisho katika Halmashauri za Wilaya 69 katika Mikoa 21 na hivyo kufanya jumla ya maeneo yaliyotengwa kwa ufugaji kufikia hekta milioni 1.28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya hivi karibuni ya wafugaji kuingiza mifugo katika Pori la Akiba la Burigi, Msitu wa Hifadhi wa Biharamulo, Msitu wa Hifadhi wa Geita na Msitu wa Hifadhi wa Bukombe na Hifadhi ya Wanyamapori ya Maswa na katika maeneo mengine ambao mifugo yao iliathirika, yametokana na wafugaji kukosa malisho ya kutosha hususan wakati wa kiangazi. Nachukua nafasi hii kutoa pole kwa wafugaji wote walioathirika kwa namna moja au nyingine kutokana na matukio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kulifuatilia suala hili na inaahidi kuwachukulia hatua za kisheria watakaobainika kusababisha usumbufu na athari hizo. Aidha, Serikali inaendelea kuzihimiza Halmashauri kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya ufugaji na wafugaji wanashauriwa kufuga kwa kuzingatia Sheria ya Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo Sura 180 inayoelekeza kufuga

idadi ya mifugo kulingana na uwezo wa malisho na hivyo kupunguza tatizo la wafugaji kuhamahama linalosababisha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa rasilimali za ardhi na maji na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu katika mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho ya Vikuge (Kibaha), Sao Hill (Mufindi), Langwira (Mbeya), Mabuki (Misungwi) na Kizota (Dodoma) ili kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za malisho. Katika mwaka 2012/2013, jumla ya tani 48 za mbegu bora za aina mbalimbali na marobota 497,611 ya hei yamezalishwa katika mashamba hayo na taasisi nyingine za umma. Aidha, sekta binafsi imeendelea kuhamasishwa kuwekeza katika uzalishaji wa hei ambapo jumla ya marobota 421,000 yamezalishwa. Pia, sekta binafsi imeendelea kuwekeza katika usindikaji wa vyakula vya mifugo ambapo uzalishaji wa vyakula vya mifugo ulifikia tani 905,000 mwaka 2012/2013. Vilevile, Wizara imefanya ukaguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo katika viwanda 15 vinavyosindika vyakula vya mifugo ili kuona kama vinakidhi viwango. Kaguzi hizo zilibaini upungufu wa protini na wanga na ushauri umetolewa ili kuondoa kasoro hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) inayotekelezwa na Halmashauri iliwezesha ujenzi wa malambo mapya 25, ukarabati wa malambo tisa (9) na uchimbaji wa visima virefu saba (7). Aidha, elimu ya matumizi bora ya ardhi imetolewa kwa watalaam 26 katika Halmashauri 12 za Igunga, Kalambo, Kaliua, Kakonko, Kasulu, Mlele, Mpanda, Nkasi, Sikonge, Sumbawanga, Urambo na Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya Langwira, Vikuge, Sao Hill, Mabuki, Kongwa, Kizota, Buhuri na Mivumoni kwa kuyapatia vitendea kazi na kuhamasisha sekta binafsi kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za malisho. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia uzalishaji na usindikaji wa vyakula bora vya mifugo nchini katika viwanda 80 vilivyopo

na vingine vitakavyojengwa na kuwajengea uwezo wakaguzi 45 wa vyakula vya mifugo. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalam 30 kuhusu usimamizi na matumizi ya maeneo ya malisho kutoka Halmashauri za Chunya, Ileje, Iringa, Kalambo, Kilolo, Mbarali, Mbozi, Momba, Nkasi na Sumbawanga ikiwa ni baadhi ya maeneo ambayo wafugaji wanahamia na kufikisha idadi ya watalaam 51 kutoka jumla ya Halmashauri 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa Kifuta Machozi kwa wafugaji. Zoezi la kutoa kifuta machozi kwa wafugaji waliopoteza mifugo yao yote katika Wilaya za Longido (kaya 2,852), Monduli (kaya 1,484) na Ngorongoro (kaya 1,791) kutokana na ukame uliotokea mwaka 2008/2009 linaendelea kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Mpango huu unatarajiwa kusambaza ng'ombe katika Wilaya za Longido (14,260), Monduli (7,420) na Ngorongoro (8,508) zitakazogharimu jumla ya shilingi 12,109, 900,000. Hadi sasa, jumla ya ng'ombe 6,933 na mbuzi 1,740 wenye thamani ya shilingi 2,945,916,000 wamegawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, udhibiti wa magonjwa ya mifugo. Maeneo huru ya magonjwa ya mifugo. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imeendelea kujenga uwezo katika maeneo yaliyoainishwa kuwa huru na magonjwa ya mlipuko ya mifugo ya Sumbawanga na Nkasi kwa kutoa mafunzo kwa wadau na kuanzisha Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo Sumbawanga. Pia, uchunguzi wa sampuli 93 za nyati katika Hifadhi za Ruaha, Mikumi, Mkomazi na 155 za ng'ombe kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi hizo ulifanyika na uchunguzi wa kubaini aina ya virusi vya ugonjwa wa Miguu na Midomo unaendelea. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia Ugonjwa wa Miguu na Midomo *(FMD)* katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mlipuko. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko ya Mifugo unaotekelezwa katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini

mwa Afrika imewezesha mafunzo ya uzamili kwa wataalam 25 na 90 wamepata mafunzo ya muda mfupi. Aidha, vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mashine za "Fume hood na Lympholysing machine" kwa ajili ya maabara ya kisasa *Bio-Security Level 3* ya mifugo Temeke vimenunuliwa. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuandaa Mpango Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo nchini, kuunganisha vituo sita vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kwenye mdahalisi *(internet)* na kuvipatia kompyuta 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kugharimia mafunzo ya wataalam, ununuzi wa vitenganishi *(reagents and diagnostic kits)* na kuendeleza uchunguzi wa Ugonjwa wa Miguu na Midomo kwenye nyati na wanyama wafugwao nchini. Aidha, uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko utaendelea kwenye ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe katika maeneo mbalimbali nchini ili kubaini aina ya virusi na chanjo itakayosaidia kudhibiti ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege (HPAI), ambapo hadi sasa ugonjwa huo haujatokea nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imeandaa na kuchapisha nakala 1,000 za Mpango wa Tahadhari ya Mafua Makali ya Ndege wa Miaka Mitano (2012 – 2017) kwa ajili ya kusambazwa kwa wadau. Vilevile, Wizara imesambaza dozi milioni 5.4 za chanjo ya Mdondo kwa lengo la kuendelea kudhibiti ugonjwa hatari wa Mdondo wa kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kufuatilia mwenendo wa Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege na kudhibiti Mdondo na Homa ya Nguruwe pamoja na kukamilisha mikakati ya udhibiti wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya ng'ombe nchini kwa kununua chanjo dozi 300,000

ambazo zimewezesha kuchanja ng'ombe 285,000 katika Wilaya za Kiteto, Iringa, Kilindi, Nkasi na katika mashamba ya Kampuni ya Ranchi za Taifa. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itanunua chanjo dozi milioni tano (5) kupitia mradi wa "*SADC–TADs*" kwa ajili ya kuendeleza uchanjaji katika Mikoa ya Kagera na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa Sotoka ya mbuzi na kondoo umeendelea kudhibitiwa kwa kutoa chanjo katika Mikoa ya Arusha, Mtwara, Morogoro, Singida, Tanga, Rukwa na Mara. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na *FAO* imesambaza dozi 400,000 za chanjo katika Mikoa ya Arusha, Singida na Tanga. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *FAO - ECTAD* Nairobi imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Mlipuko wa Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kuratibu na kusimamia kampeni za chanjo katika Mikoa ya Arusha, Mara, Tanga na Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yanayoenezwa na kupe. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, imeendelea kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe kwa kukarabati majosho 20 na kujenga majosho mapya 14 kupitia DADPs. Aidha, Wizara imeendelea kutoa ruzuku ya asilimia 40 kwa dawa za kuogesha mifugo ambapo lita 92,323 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.5 zilinunuliwa na kusambazwa katika Mikoa yote nchini. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi ilichanja ng'ombe 140,438 dhidi ya Ndigana kali katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Pwani, Rukwa, Singida na Tanga. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na wadau mbalimbali katika kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo kupitia ujenzi wa majosho mapya, ukarabati wa majosho, matumizi sahihi ya dawa za ruzuku na kuhamasisha matumizi ya chanjo dhidi ya Ndigana kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbung'o na nagana. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati

wa Kudhibiti Mbung'o na Nagana kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha uchunguzi wa mtawanyiko wa mbung'o nchini ambapo matokeo yameonesha eneo linalokaliwa na mbung'o ni hekta 30,931,957.6 sawa na asilimia 32.8 ya eneo la nchi nzima

(ii) Kutega vyambo 9,286 vyenye viuatilifu aina ya pareto na kusambaza mitego 32, mabomba ya mkono 64, viuatilifu aina ya pareto lita 24, mabango 2,000 na vipeperushi 7,500 katika Wilaya za Urambo, Uvinza, Bagamoyo, Handeni, Pangani, Kisarawe, Mpanda na Mbulu; na

(iii) Kujenga uwezo wa wataalam 18, watatu kwa kila Wilaya za Kilombero, Kondoa, Manyoni, Mbulu, Nanyumbu na Ulanga walijengewa uwezo wa mbinu shirikishi za udhibiti wa mbung'o na Nagana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kudhibiti Mbung'o na Nagana katika Halmashauri za Kibondo, Kasulu, Meatu, Maswa, Karatu, Kiteto, Ngorongoro na Serengeti. Aidha, itanunua na kusambaza vitambaa vya vyambo mita 50,000, mitego 500 na viuatilifu vya pareto lita 110 katika Halmashauri za Ngorongoro, Kiteto, Mpanda, Nkasi, Kaliua na Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu, kichaa cha mbwa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Taasisi ya *Bill & Melinda Gates Foundation* chini ya Uratibu wa Shirika la Afya Duniani imeendelea kutekeleza Mradi wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara na Pwani. Kupitia mradi huo, dozi 200,000 za chanjo zimenunuliwa na kusambazwa ambapo jumla ya mbwa 189,890 na paka 9,160 walichanjwa. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na sekta binafsi

itaendelea kudhibiti Kichaa cha Mbwa kwa kununua dozi 250,000 za chanjo dhidi ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, homa ya Bonde la Ufa, katika mwaka 2012/2013, jumla ya dozi 400,000 zilinunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri za Longido, Ngorongoro, Babati, Handeni, Mkuranga, Karagwe, Ngara, Geita, Chamwino, Bahi na Mpwapwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeandaa na kusambaza nakala 1,000 za Mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa wa Miaka Mitano (2007/2008 – 2012/2013). Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuhamasisha udhibiti wa ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kununua chanjo dozi 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa kutupa mimba na kifua kikuu, katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kupima kiwango cha maambukizi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba (*Brucellosis*) ambapo sampuli 2,910 (ng'ombe 2,856 na mbuzi 54) kutoka Wilaya za Kiteto, Manyoni, Singida, Iramba, Kondoa, Urambo, Mbeya, Iringa, Lushoto, Muheza, Mufindi na Nanyumbu zilipimwa. Jumla ya ng'ombe 69 waligundulika kuwa na maambukizi na kuchinjwa chini ya usimamizi. Vile vile, sampuli 1,403 za ng'ombe kutoka Wilaya za Iramba, Manyoni, Singida, Mbeya, Mufindi na Iringa zilipimwa ambapo sampuli tano zilibainika kuwa na vimelea vya Kifua Kikuu cha ng'ombe na kuteketezwa. Pia, wataalam 6 walipata mafunzo ya muda mfupi ya udhibiti wa magonjwa hayo. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kupima kiwango cha maambukizi ya magonjwa ya Kutupa Mimba na Kifua Kikuu cha ng'ombe nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa mifugo na mazao yake, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kufanya ukaguzi wa mifugo na mazao yake ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa na kulinda afya ya walaji. Katika mwaka 2012/2013 jumla ya ng'ombe milioni 1.85, mbuzi 870,150, kondoo 216,304, kuku milioni 4.2 na nguruwe 144,260 walikaguliwa katika machinjio mbalimbali. Aidha,

wakaguzi 60 walipata mafunzo ya matumizi ya teknonojia ya kalamu ya dijitali na udhibiti wa ubora wa ngozi na nyama kutoka Halmashauri 23 katika Mikoa ya Arusha, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Mtwara na Rukwa. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa mifugo na mazao yake nchini ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa, kulinda afya ya walaji na kukuza soko la mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuimarisha Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo kwa kutoa mafunzo kuhusu Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Sura 184 na Kanuni zake kwa wataalam 20 kutoka Halmashauri za Bagamoyo, Handeni, Lushoto, Mbeya, Mvomero, Njombe na Rungwe. Aidha, kupitia ufadhili wa *FAO* ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo unaendelea. Pia, Wizara imenunua vifaa vya utambuzi ikiwa ni pamoja na tufe za tumboni 5,000 na hereni 5,000. Vilevile, wafugaji 2,428 walisajiliwa na ng'ombe 50,534 walipigwa chapa ya moto kuwatambua katika Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo katika Halmashauri. Pia, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalam 100 na kuhamasisha umma kuhusu mfumo huu. Vilevile, Wizara itakamilisha ujenzi wa mfumo wa utambuzi na kushirikiana na Halmashauri kufanya utambuzi wa ng'ombe 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa sekta ya uvuvi. *Uvuvi wa samaki na uuzaji wa mazao ya uvuvi.* Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuratibu na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini. Katika mwaka 2012/2013, idadi ya wavuvi ilikuwa 182,741 na vyombo vya uvuvi 56,985. Nguvu hii ya uvuvi imewezesha kuvunwa tani 365,023.38 za mazao ya uvuvi yenye thamani ya shilingi trilioni 1.3. Aidha, Wizara imeendelea

kuratibu na kusimamia uuzaji wa samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi ambapo jumla ya leseni 97 za kuuza nje ya nchi samaki na mazao ya uvuvi zimetolewa na tani 41,394.3 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 45,550 wenye thamani ya shilingi bilioni 254.9 waliuzwa nje ya nchi na kuiingizia Serikali mapato ya shilingi bilioni 6.8. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na *FAO* imekamilisha kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji *(Pelagic Fisheries Management Plan)* ili kuwa na uvuvi endelevu wa samaki wanaopatikana katika tabaka hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kuhamasisha wadau kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya uvuvi yakiwemo ujenzi wa boti bora za uvuvi na viwanda vya uvuvi ili kuongeza uzalishaji na thamani kwenye mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wavuvi wadogo. Wizara imeendelea kuwawezesha wavuvi wadogo kwa kuboresha miundombinu ya uvuvi. Katika mwaka 2012/2013, ujenzi wa mialo ya Kibirizi (Kigoma Ujiji), Muyobozi (Uvinza), Ikola (Mpanda) na Kirango (Nkasi) katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika umeanza. Aidha, ujenzi wa boma la karakana ya kutengeneza boti ya Mbamba Bay umekamilika. Pia, Wizara imesambaza nakala 595 za kitabu cha Kanuni Bora za Uvuvi na Ufugaji wa Samaki na vipeperushi 700 na kuhamasisha uanzishaji wa Vyama 23 vya Msingi vya Ushirika wa Wavuvi katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mradi wa MACEMP uliokamilika Mwezi Februari, 2013, inakamilisha ujenzi wa ghala la mwani katika kijiji cha Jibondo Mafia; ujenzi wa mialo ya Nyamisati (Rufiji), Kilwa-Masoko na Kilindoni (Mafia) na kuweka mitambo ya barafu na majokofu kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya uvuvi; imeandaa filamu ya tathmini ya kazi zilizofanywa na Mradi wa MACEMP; kukamilisha ununuzi wa maboya 63 ya kuweka mipaka ya Hifadhi za Bahari ya

Mafia, Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma na Maeneo Tengefu ya Dar es Salaam na Maziwe (Pangani). Aidha, Wizara imepokea taarifa ya uchunguzi kuhusu mtandao wa vyanzo, usambazaji na masoko ya mabomu yanayotumika katika uvuvi haramu na madhara yake katika maeneo ya mradi na inaifanyia kazi kwa kushirikiana na vyombo husika. Baada ya *MACEMP* kukamilika, mradi mpya unaandaliwa wa *Southwest Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Programme -SWIOFish* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia ambao utatekelezwa kuanzia mwaka 2014/2015 katika nchi za Afrika zinazopakana na Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itakamilisha ujenzi wa karakana ya kutengeneza boti ya Mbamba Bay na itaendelea kuhamasisha wavuvi wadogo kuanzisha vyama vya ushirika na *SACCOS*; na kutoa elimu kuhusu fursa za uwekezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Wizara imeendelea kuratibu shughuli za ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki, ajira na kipato kwa wananchi. Katika mwaka 2012/2013, vituo vya kuzalisha vifaranga vya samaki wa maji baridi vya Kingolwira (Morogoro), Luhira (Songea), Mtama (Lindi), Nyamirembe (Chato) na Mwamapuli (Igunga) vimeimarishwa kwa kupewa wataalam na vitendea kazi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kujenga na kuimarisha vituo vya ukuzaji wa viumbe kwenye maji vya Chongoleani (Tanga), Nyamirembe (Chato), Mbegani, Kingolwira, Ruhila (Songea), Mtama, Bukoba, Mwanza, Musoma na Karanga (Moshi) na kuanzisha vituo vipya vya Chihiko (Mtwara), Mwamapuli (Igunga) na Kibirizi (Kigoma) kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa vifaranga kwa wafugaji wa samaki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, katika kusambaza teknolojia ya kufuga viumbe kwenye maji, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imetoa mafunzo kwa wadau 1,547 kuhusu ufugaji wa samaki na kuwezesha

kuanzishwa kwa vikundi 64 vya ukuzaji viumbe kwenye maji. Aidha, vifaranga 2,066,620 aina ya perege vimezalishwa na kusambazwa kwa wadau. Pia, Kampuni ya *Alphakrust* iliyopo Mafia imezalisha na kusambaza vifaranga 11,520,000 vya kambamiti na imevuna tani 270 za kambamiti zenye thamani ya shilingi bilioni 2.16. Tani 384.75 za mwani zenye thamani ya shilingi 153,900,000/= zimevunwa na wakulima wa mwani na kuuzwa nje ya nchi. Vilevile, Kikundi cha Msichoke katika Wilaya ya Bagamoyo kimetengeneza na kuuza miche 4,500 ya sabuni za mwani na kikundi cha Mngoji katika Wilaya ya Mtwara kimekuza na kuvuna vipande 762 vya lulu na kutengeneza jozi 120 za hereni. Vilevile, jumla ya mabwawa 696 ya kufugia samaki yamechimbwa na kupandikizwa samaki katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kuhamasisha wananchi kuhusu ukuzaji viumbe kwenye maji kwa kutoa elimu, kuzalisha na kusambaza vifaranga vya samaki milioni 10 pamoja na uongezaji thamani ya mazao yakuzwayo kwenye maji. Baadhi ya vifaranga hivyo vitapandikizwa kwenye mabwawa ya asili ya Bulenya (Igunga), Nara (Kilosa) na Msenda (Namtumbo). Aidha, maafisa ugani 40 watapatiwa mafunzo ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti, mafunzo na ugani wa mifugo na uvuvi. Wizara imeendelea kusimamia na kuwezesha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (*TALIRI)* na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)*; Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) na Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania (TVLA) ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(TALIRI)*. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba uanzishwaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania umekamilika chini ya Sheria Na. 4 ya mwaka 2012 na Taasisi

imeanza kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka 2012/ 2013, Wizara imeendelea kuimarisha vituo vya utafiti vya *TALIRI* vya Kongwa, Mabuki, Mpwapwa, Naliendele, Tanga, Uyole na *West Kilimanjaro* kwa kuvipatia vitendea kazi na kukarabati miundombinu. Aidha, Taasisi imeendelea kutekeleza miradi ya utafiti wa mifugo ya kuboresha uzalishaji wa ng'ombe wa nyama na maziwa, nguruwe; kuku, malisho na masoko ya mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuhifadhi koosafu za asili, katika mwaka 2012/2013, Taasisi imetathmini na kusambaza mifugo yenye tija vijijini ambapo ng'ombe 1,353 wa aina ya Mpwapwa na 339 aina ya *Friesian* na chotara wa ng'ombe hao waliendelea kufanyiwa utafiti na kusambazwa kwa wafugaji walioomba na kuuziwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Pwani, Singida na Tanga. Aidha, Taasisi imetathmini ng'ombe 20 aina ya Maasai, mbuzi wa asili 1,136 aina za Buha, Red Maasai, Pare White, Red Sonjo, Newala na Gogo White; aina tatu za kondoo za Red Maasai, Dorper na *Black Head Persian (BHP);* nguruwe 48; kuku wa asili 1,278 aina za Kuchi, Sasamala, Kawaida, Mtewa, Kishingo, Bukini, Kisunzu, Kuza, Sukuma, Msumbiji, Katewa, Mandendenga na Njachama; na vinasaba 200 vya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti kuhusu malisho ya mifugo zimeendelea ambapo ekari 543 za majaribio zimepandwa malisho aina ya *Rhodes* na Nyakachimbu (*Cenchrus ciliaris*) na kuzalisha marobota 78,600 ya hei. Aidha, kilo 1,100 za mbegu za nyasi zimevunwa na kusambazwa kwa wafugaji katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Mtwara na Pwani na kilo 40 ziligawiwa kwa watafiti wa mifugo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Vilevile, jumla ya kilo 37 za mbegu za mikunde na 65 za mabingobingo zilisambazwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya matokeo ya tafiti hizo yameonesha ng'ombe jike chotara anayetokana na ng'ombe dume aina ya Mpwapwa na jike aina ya Zebu ameongeza uzalishaji wa maziwa kufikia lita sita (6)

ikilinganishwa na uzalishaji wa lita moja (1) hadi mbili (2) kwa siku. Aidha, chotara jike anayetokana na kupandisha dume la *Fresian* na ng'ombe wa asili ameonesha uwezo wa kuzaa mara ya kwanza katika umri mdogo wa miaka 2 -3 ikilinganishwa na miaka 4 - 5 kwa Zebu. Matokeo hayo yamesambazwa kwa wafugaji 764 kupitia mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itakamilisha kuandaa miundo ya utumishi, kanuni za fedha na utumishi na miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania. Aidha, Taasisi itaendelea kutekeleza miradi ya utafiti wa mifugo ya kuboresha uzalishaji wa ng'ombe wa nyama na maziwa; mbuzi, kondoo, nguruwe; kuku wa asili na malisho pamoja na utafiti wa masoko ya mifugo na mazao ya mifugo. Vilevile, Taasisi itatathmini kosaafu ya ng'ombe wa asili aina ya Sukuma; itasambaza madume 150 ya ng'ombe aina ya Mpwapwa na mbuzi 120 aina ya Malya kwa wafugaji kwa lengo la kuboresha mifugo ya asili; na kusambaza kilo 1,000 za mbegu za nyasi na kilo 500 za mikunde. Pia, Taasisi itaendelea na ujenzi wa maabara za sayansi ya nyama (Mabuki), uhawilishaji kiinitete (embryo transfer) - Mpwapwa, teknolojia ya maziwa (Uyole), lishe ya mifugo (Mpwapwa, Tanga na West Kilimanjaro) pamoja na ujenzi na ukarabati wa nyumba za watumishi na ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti Uvuvi Tanzania *(TAFIRI).* Wizara imeendelea kujenga uwezo wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) ili kuongeza tija katika utafiti wa uvuvi. Katika mwaka 2012/2013, Taasisi imekarabati maabara na jengo la utawala la kituo cha Kigoma; imefunga vifaa vya uvuvi na utafiti katika meli ya RV Kiboko inayotumika kwa utafiti katika Bahari ya Hindi; imejenga matenki ya kufanyia majaribio ya vyakula vya samaki katika kituo cha *TAFIRI* Dar es Salaam; imesimika *wind mill* ya kuvuta maji kutoka ziwani na kukarabati mabwawa ya kufanyia utafiti katika kituo cha Mwanza. Pia, Taasisi

imenunua vitendea kazi vikiwemo gari, kompyuta, Printer na vifaa vya utafiti kwa ajili ya kuboresha utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Taasisi imeendelea kufanya tafiti ili kubaini wingi na mtawanyiko wa Potwe (*whale shark*) katika Bahari ya Hindi na kutathmini uchumi-jamii wa samaki aina ya Jodari (Tuna) katika pwani ya Bahari ya Hindi kwa kushirikiana na *World Wide Fund for Nature (WWF).* Aidha, Taasisi imefanya utafiti kuhusu bioanuwai ya uvuvi katika Mto Ruvu, Mto Ruvuma na Ziwa Rukwa na matokeo ya awali yanaonesha uwepo wa bioanuwai kubwa. Pia, imefanya utafiti wa kutengeneza vyakula vya samaki kwa kutumia malighafi zipatikanazo karibu na wafugaji katika vituo vya Kunduchi na Mwanza; kuzalisha mbegu bora za samaki kituo cha Kunduchi na Mwanza; kufuga samaki kwa mfumo unaojumuisha samaki, kilimo cha mbogamboga na kuku huko Kingolwira-Morogoro; kupunguza uharibifu wa mazao ya samaki baada ya uvunaji kwa kutumia kifaa cha kukaushia samaki kinachotumia mionzi ya jua kwenye Kituo cha Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, *TAFIRI* kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea na utafiti wa samaki na mazingira katika maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), maziwa madogo, mito na Bahari ya Hindi; kufanya utafiti wa ufugaji samaki; kuimarisha miundombinu ya Taasisi kwa kujenga na kukarabati ofisi na maabara na kununua vitendea kazi kwa vituo vya Dar es Salaam, Sota (Rorya), Kyela na Mwanza. Aidha, Taasisi itasambaza taarifa za kitafiti kwa wadau mbalimbali wa uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (*Tanzania Veterinary Laboratory Agency-TVLA)*. Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imeendelea na majukumu yake ya kufanya tafiti, uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo. Katika mwaka 2012/2013, Wakala imezalisha na kusambaza dozi milioni 5.4 za chanjo ya Mdondo, dozi 77,500 za Kimeta na dozi 36,900 za Chambavu; imefanya uchunguzi wa sampuli 416 za vyakula

vya mifugo ambapo sampuli 333 zilibainika kuwa na upungufu wa nguvu na protini; kuendelea kufuga mbung'o 10,760 kwa ajili ya tafiti za teknolojia za kudhibiti mbung'o na ugonjwa wa Nagana katika Kituo cha Utafiti wa Mbung'o na Ndorobo Tanga; kufanya utambuzi wa magonjwa ya wanyama kwa sampuli 10,800 kutoka kwa wafugaji na vituo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo ambapo sampuli 8,600 zilibainika kuwa na magonjwa mbalimbali; na kuanzisha kitengo cha *cell culture* katika maabara. Aidha, Wakala inaendelea kufanya tafiti za kudhibiti mbung'o na ndorobo katika maeneo ya Mikoa ya Lindi, Pwani na Mtwara ambapo mbung'o aina ya *Glossina morsitans morsitans* na *Glossina pallidipes* wamepungua. Pia, Wakala imeendelea kutafiti chanjo ya I-2 ya kuzuia Mdondo katika maeneo ya Rorya, Rufiji, Same na Singida; na kufanya tathmini za kimaabara kwa chanjo za Homa ya Bonde la Ufa, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Kimeta, Ugonjwa wa Kutupa Mimba na Ndui ya Kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wakala itaimarisha kitengo cha *Cell culture* kwa kuweka vifaa katika maabara; itaendeleza tathmini ya aina tatu za chanjo za magonjwa ya mifugo ya Homa ya Bonde la Ufa, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe na Ndui ya Kuku ili ziweze kutumika. Aidha, Wakala itazalisha, kuuza na kusambaza chanjo za Mdondo dozi milioni 100, Kimeta dozi 500,000, Chambavu dozi 500,000 na dozi 250,000 za Ugonjwa wa Kutupa Mimba. Pia, itafanya tafiti na kusambaza teknolojia mbalimbali kwa ajili ya kutambua na kudhibiti magonjwa ya Ndigana Kali, Nagana na Malale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi *(Fisheries Education and Training Agency - FETA).* Wizara imeendelea kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi ili kukidhi mahitaji ya wataalam katika fani hiyo. Katika mwaka 2012/2013, Wakala imeongeza udahili wa wanafunzi katika Kampasi za Nyegezi na Mbegani kufikia 943 ikilinganishwa na 714 mwaka 2011/2012. Pia, imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wanafunzi 272 wakiwemo 56 kutoka nchi za *SADC*. Aidha, vyuo hivi vimeimarishwa kwa

kupatiwa wataalam na vitendea kazi. Pia, ukarabati wa Kampasi ya Kigoma umekamilika na mafunzo tarajali kwa wataalam wa ugani 20 kutoka kanda ya Ziwa Tanganyika yametolewa na maandalizi ya kuanzisha kozi za astashahada katika Kampasi hiyo yanaendelea. Vilevile, Meli ya MV Mafunzo imefanyiwa ukarabati mkubwa katika Chelezo cha Zanzibar na taratibu za kuanzisha Kampasi ya Mikindani na Kituo cha Kurasini zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuimarisha Wakala kwa kukarabati Kampasi za Mikindani na Kigoma; na Vituo vya *Mwanza South* na Kurasini na kuvipatia vifaa ili kuwezesha Wakala kudahili jumla ya wanachuo 1,500. Aidha, Wakala itaanzisha vituo vipya vya Mbamba Bay na Gabimori (Rorya), kufanya tafiti tumika na kutoa huduma za ushauri zinazohusu uvuvi na ufugaji wa viumbe majini. Pia, kuendelea kuzalisha chakula na vifaranga bora vya samaki wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo *(Livestock Training Agency - LITA).* Wizara imeendelea kuimarisha Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo ili kutoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada na Astashahada katika Kampasi zake za Tengeru, Mpwapwa, Morogoro, Madaba, Buhuri na Temeke. Katika mwaka 2012/2013 jumla ya wanafunzi 1,720 walidahiliwa na kati ya hao, 689 wa mwaka wa pili watamaliza mafunzo yao mwezi Juni 2013. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na wadau imetoa mafunzo ya ufugaji bora kwa wafugaji 118, watengenezaji mitambo ya biogesi 22 na kilimo biashara kwa maafisa ugani 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wakala imeendelea kujiimarisha kwa kuongeza wataalam na vitendea kazi; kujenga, kukarabati majengo na miundombinu katika Kampasi zake na kuanzisha kituo cha Mabuki. Aidha, Wakala imenunua ng'ombe bora 50 wa maziwa na kuboresha hekta 120 za malisho kwa ajili ya mafunzo na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wakala itatoa mafunzo kwa wanafunzi 2,000 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada na mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji na wakulima; kujenga, kukarabati na kuzipatia vifaa Kampasi na Makao Makuu ya *LITA.* Aidha, itaboresha uzalishaji wa mifugo na mazao ya kilimo katika Kampasi zake, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri zinazohusu afya na uzalishaji wa mifugo. Aidha, Wakala itaanzisha kituo kipya cha Kikulula (Karagwe).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri iliendelea kupeleka teknolojia za kisasa kwa kutoa mafunzo maalum kwa wafugaji 2,140, wavuvi 1,789 na wagani 20. Pia, wafugaji 10 kutoka Halmashauri za Bagamoyo, Mvomero na Njombe walikwenda Naivasha - Kenya kwa ziara ya mafunzo ya wiki moja kupitia Programu ya *Eastern Africa Agricultural Productivity Programme (EAAPP).* Wizara ilitayarisha na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya runinga vilivyohusu ufugaji na uvuvi. Aidha, vipeperushi 7,000 kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa vimesambazwa kwa wadau. Vilevile, Wizara imeendelea kukarabati vituo vya mafunzo ya wafugaji na wavuvi vya Gabimori na Kikulula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itatayarisha na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya runinga. Aidha, itatoa mafunzo elekezi kwa wataalam wa Halmashauri 25 kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi katika ufugaji wa samaki na kuwezesha wataalam wa ugani 30 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia ubora wa mazao ya mifugo na uvuvi pamoja na huduma za kitaalam kupitia Bodi ya Nyama, Bodi ya Maziwa na Baraza la Veterinari Tanzania, Kitengo cha Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi na Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi-Nyegezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Nyama Tanzania kwa

kuipatia wataalam na vitendea kazi. Aidha, Bodi imeendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sheria ya Nyama, Sura ya 421 na kusambaza nakala 1,200 za vipeperushi vya tafsiri ya sheria hiyo. Pia, Bodi imetekeleza mfumo wa ubia wa kiushindani ambapo wadau 297 wa mnyororo wa thamani wa nyama ya kuku katika Mkoa wa Dar es Salaam wametambuliwa. Vilevile, Bodi imeandaa mwongozo wa usajili wa wadau wa tasnia ya nyama, imeandaa Mpango Mkakati wa Bodi wa miaka mitano (2013/14 – 2017/18) na kuwawezesha Wajumbe wa Bodi kupata mafunzo kuhusu Utawala Bora. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa za Kanda ya Ziwa imewezesha kuanzishwa na kusajiliwa kwa Chama cha Wafugaji Kanda ya Ziwa (CHAWAKAZI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuiimarisha na kuiwezesha Bodi ya Nyama kwa kuipatia wataalam na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake. Aidha, Bodi itasajili wadau 200 wa tasnia ya nyama na vyama vyao; kuendelea kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Nyama, Sura ya 421 na kusimamia ubora wa nyama na bidhaa zake. Pia, itahamasisha na kuwezesha uundaji wa Chama cha Wafugaji Kitaifa na kuimarisha Vyama vya Wadau vya Wafanyabiashara wa Mifugo na Nyama Tanzania *(TALIMETA)* na Chama cha Wasindikaji wa Nyama Tanzania *(TAMEPA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Maziwa kwa kuipatia wataalam na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka 2012/2013, Bodi imetoa elimu kwa wadau 400 ili kutekeleza Sheria ya Maziwa Sura 262 na Kanuni zake katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Morogoro, Rukwa na Ruvuma. Aidha, Bodi imeratibu Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Unywaji wa Maziwa Shuleni Duniani yaliyofanyika Njombe Mjini na Wiki ya Maziwa iliyofanyika katika Manispaa ya Moshi. Vilevile, Bodi imeandaa Taratibu za Ukaguzi wa Maziwa *(Code of Milk Hygiene);* na kuwezesha mafunzo kwa watumishi tisa wa Bodi kuhusu taratibu na kanuni za utumishi wa umma. Pia, Bodi imeendelea kuratibu Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni

ambapo wanafunzi 66,528 kutoka shule 144 wamenufaika na mpango huo .

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuiimarisha Bodi ya Maziwa kwa kuipatia wataalam na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake. Aidha, itaimarisha ukaguzi wa maziwa kwa kuteua na kuwajengea uwezo wakaguzi wa maziwa; kuanzisha mfumo wa takwimu; kuendelea kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza Mpango wa Unywaji wa Maziwa Shuleni; na kuratibu Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yatakayofanyika kitaifa katika Manispaa ya Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Veterinari limeendelea kusimamia viwango na kuandaa miongozo juu ya utoaji huduma za mifugo nchini. Katika mwaka 2012/2013, Baraza limesajili Madaktari wa Mifugo 21; vituo vya huduma 62; kuorodhesha na kuandikisha wataalam wasaidizi 227; kutoa leseni kwa wakaguzi wa nyama 27, wahimilishaji 18 na fundi sanifu wa maabara 13. Aidha, Baraza limetoa mafunzo kwa wataalam 198 na wadau 124 na limekagua vituo vya huduma za mifugo 201 katika Halmashauri za Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Geita, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Njombe, Ruvuma, Shinyanga na Simiyu ambapo vituo 51 vilifungwa na kuelekezwa maboresho. Pia, Baraza kwa kushirikiana na *NACTE* limehakiki matumizi ya mitaala ya Astashahada na Stashahada ya Afya na Uzalishaji Mifugo katika vyuo 11 vikiwemo 4 vya sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Baraza litasajili madaktari wa mifugo 30, kuandikisha, kuorodhesha na kuwapatia miongozo wataalam 700 na kusajili vituo vya huduma za mifugo 350. Vilevile, Baraza litatoa leseni kwa wakaguzi wa nyama 50, wahimilishaji 40 na mafundi sanifu wa maabara 20; kuhakiki viwango vya taaluma ya veterinari katika vyuo 10 na makampuni 30 yanayotoa huduma za mifugo. Aidha, Baraza litaratibu Siku ya Veterinari Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhakiki

viwango vya ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi. Katika mwaka 2012/2013, wadau 40 walioteuliwa na Halmashauri kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Kagera, Kigoma, Mbeya, Mwanza, Pwani na Tanga, wamehamasishwa kuwekeza kwenye viwanda vya uvuvi ambapo viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi vimeongezeka kutoka 34 mwaka 2011/2012 hadi 43 mwaka 2012/2013. Aidha, kaguzi 618 za viwanda na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi na 1,979 za kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao yake kabla ya kusafirishwa kwenye masoko ya nje ya nchi zilifanyika. Matokeo ya kaguzi hizo yalionesha kukidhi viwango vya ubora. Pia, Wizara imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia sahihi ya uandaaji, uchakataji na uhifadhi wa samaki na mazao yake kwa wadau wa uvuvi 331 na wakaguzi 34 katika ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itafanya kaguzi 3,600 za kuhakiki ubora na viwango kwenye viwanda vya kuchakata na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi. Aidha, itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kuhifadhi mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kuratibu miundombinu ya masoko ya uvuvi kwa kufanya kaguzi 195 kwenye masoko makubwa ya Samaki ya Magogoni - Dar es Salaam, Kirumba - Mwanza na masoko madogo katika maeneo ya mijini na katika mialo ya Ziwa Victoria, Tanganyika, Rukwa na Nyasa, maziwa madogo na mito. Aidha, masoko matatu ya samaki yamejengwa katika Halmashauri za Babati, Iringa na Kyela kupitia *DADPs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuratibu usafi wa masoko na mialo na kuhimiza uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuimarisha Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi - Nyegezi kwa kuipatia vitenganishi *(reagents)* na kutoa mafunzo kwa wataalam wa maabara na kukamilisha uandaaji wa miongozo ya uendeshaji. Aidha, Wizara imeandaa taratibu za awali za kupata ithibati ya uchunguzi wa kemikali, imechunguza sampuli 1,474 ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi na imechunguza sampuli 1,135 za samaki, maji, vyakula vya samaki na udongo. Pia, Maabara ya Viuatilifu ya Dar es Salaam imeimarishwa kwa kuipatia vitenganishi na vituo vya ukaguzi wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi vya Bukoba, Dar es Salaam, Kigoma, Kilwa, Mafia, Musoma, Mwanza na Tanga vimeimarishwa kwa kuvipatia wataalam na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuimarisha na kuwezesha Maabara ya Samaki – Nyegezi, Maabara ya Viuatilifu ya Dar es Salaam na vituo vya ukaguzi pamoja na kufanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli 800 za minofu ya samaki na majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Halmashauri imeendelea kusimamia rasilimali za uvuvi, hususan udhibiti wa uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeimarisha vituo vya doria katika Ziwa Victoria (7), Ziwa Tanganyika (4), Ziwa Nyasa (3) na Bahari ya Hindi (6) kwa kuvikarabati na kuvipatia wataalam na vitendea kazi. Pia, doria zenye siku - kazi 2,999 zimefanyika na kuwezesha kukamatwa kwa nyavu za aina mbalimbali 58,191, mabomu 866, tambi za kulipua mabomu 269, vifaa vya kuzamia jozi 164, mikuki 69, bunduki za kienyeji 49, kasia 2,543, katuli 314, ndoano 94, miwani ya kuogelea 129, mitumbwi 505, injini za boti 15, magari 18, pikipiki 7 na baiskeli 9. Pia, kilo 37,112 za

samaki wachanga, 2,613 za samaki wabichi, 1,752 za samaki wakavu, 4,768 za dagaa wakavu, 1,997 za samaki waliovuliwa kwa mabomu, 312 za jongoo bahari na 264 za makombe zilikamatwa. Vilevile, watuhumiwa 294 walikamatwa kwa kujihusisha na uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi ambapo kesi 27 zilifunguliwa mahakamani. Aidha, Wizara imekagua maduka ya nyavu 44 katika maeneo mbalimbali nchini ambapo maduka manne yalikutwa na nyavu haramu na wamiliki walifikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuimarisha vituo 21 vya doria, kushirikiana na Halmashauri pamoja na wadau wengine kufanya doria zenye siku - kazi 24,000 na kuendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu athari za uvuvi haramu. Aidha, Wizara itapendekeza kuanzisha mamlaka maalum ya kudhibiti uvuvi haramu chini ya Sheria ya Uvuvi Sura 279 inayofanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imewezesha kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi *(Beach Management Units - BMUs)* 20 na kufanya idadi ya *BMUs* kote nchini kufikia 739. Pia, *BMUs* 16 zimesajiliwa na nane kuwezeshwa kutunga sheria ndogo. Aidha, wadau 754 wameelimishwa kuhusu athari za uvuvi haramu na usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira. Pia, Wizara imeendelea kuzielekeza Halmashauri kuimarisha ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itawezesha uanzishwaji na uimarishaji wa *BMUs* na kuendeleza utekelezaji wa mtandao wa vikundi hivyo. Pia, itaendelea kuhamasisha wadau kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia rasilimali za uvuvi kwenye maeneo ya uvuvi, kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(MPRU).* Katika mwaka 2012/2013, Kitengo kimefanya doria zenye siku

- kazi 213 ili kudhibiti wavuvi haramu ambapo nyavu haramu 140, mbao za mikoko 200, mabomu 18, mitumbwi 14, michinji 43 na maboya 44 yalikamatwa. Aidha, Kitengo kimetangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kupitia maonesho ya Karibu (Arusha), Indaba (Afrika Kusini), Sabasaba na Nanenane; na kuchapisha na kusambaza nakala 10,000 za vipeperushi kwa wadau. Pia, Kitengo kimeimarishwa kwa kupatiwa wataalam na vitendea kazi vikiwemo magari matatu, pikipiki sita, boti la kioo na kujenga nyumba tatu za kuishi watumishi katika Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi - Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Kitengo kitaandaa kanuni za usimamizi wa maeneo na kuanzisha mchakato wa kutangaza maeneo mapya ya uhifadhi, kufanya doria za siku kazi 400 kudhibiti uvuvi haramu kwenye maeneo ya hifadhi na kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa uvuvi katika bahari kuu. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inasimamia uvuvi katika Bahari Kuu kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority – DSFA).* Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Mei, 2013, Mamlaka imetoa leseni za uvuvi 38 ambazo ziliingiza Dola za Kimarekani 1,335.810. Wavuvi wakubwa hao wameanza kutekeleza Sheria ya *Deep Sea Fishing Authority*, Sura ya 388 na Kanuni zake kwa kuleta meli zao ili zikaguliwe kwenye bandari zetu na kuchukua wataalam wa uvuvi kama waangalizi wa shughuli za uvuvi kwenye meli. Pia, ilifanya doria za saa 180 za anga na maji kwa kushirikiana na Jeshi la Wanamaji, Polisi na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) ili kudhibiti uvuvi haramu. Vilevile, Mamlaka imesasisha *(update)* mfumo wa kudhibiti nyendo za meli Bahari Kuu kwa kuweka kifaa cha kuangalia mienendo ya vyombo vya uvuvi katika Bahari Kuu *(Vessel Monitoring System - VMS)* na kuwezesha kufuatilia meli 51 zilizopata leseni. Mamlaka kwa kushirikiana na Mpango wa *FISH-i Africa* chini ya *NEPAD* ilibaini meli mbili zikiendesha uvuvi

haramu na taarifa kuhusu suala hili imetolewa *Indian Ocean Tuna Commission (IOTC)* ili ifanye uhakiki ili tuweze kuchukua hatua stahiki. Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia taarifa ya kuwepo kwa meli kumi za uvuvi ambazo zimevua katika maji yetu kwa kutumia leseni za kughushi. Pia, Mamlaka kwa kushirikiana na *TAFIRI, IOTC* na *South West Indian Ocean Fisheries Project (SWIOFP),* imefanya tathmini ya uvuvi wa kibiashara kwa kutumia vifaa sita vya kuvutia samaki *(Fish Aggregating Devices - FADs)* na kuonesha ongezeko la aina mbalimbali za samaki katika maeneo hayo. Vilevile, Wizara imeanza kupitia Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu, Sura ya 388 na Kanuni zake ili kuandaa mapendekezo ya kuiwezesha Sheria hiyo kutekelezwa ipasavyo katika mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itakamilisha mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu, Sura ya 388 na Kanuni zake. Aidha, Mamlaka itanunua meli moja ya doria na kuongeza vifaa vya kuvutia samaki *(FADs)* baharini. Vilevile, itaendelea kuhamasisha wavuvi Watanzania kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu, kushirikiana na nchi wanachama wa *IOTC* kufanya doria ya pamoja na kushirikiana na *World Wide Fund for Nature (WWF)* kufanya tathmini ya mnyororo wa thamani ya samaki aina ya Jodari na jamii zake. Pia, Mamlaka itatoa mafunzo kwa wavuvi 50 na watumishi wake wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili watumishi waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo, wanahitaji kujengewa uwezo wa kiutendaji pamoja na kuendelea kukua katika taaluma zao. Katika mwaka 2012/2013, Wizara na Taasisi zake imeajiri watumishi 20, kupandisha vyeo watumishi 234 na 50 kuthibitishwa kazini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 61, muda mfupi 143 na 166 wanaendelea na masomo ya muda mrefu. Pia, Wizara imewezesha kikao cha Baraza la Wafanyakazi, kuelimisha watumishi 601 kuhusu Mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wazi *(OPRAS),* kuwezesha watumishi 52 kushiriki katika michezo ya SHIMIWI na kuendelea

kufanya mapitio ya miundo ya utumishi wa kada za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma itawezesha ajira ya maafisa ugani wa mifugo na uvuvi 2,500 watakaoajiriwa katika Halmashauri. Halmashauri zinahimizwa zijiandae kuwapokea, kuwapangia kazi na kuwapatia vitendea kazi watumishi hao. Aidha, itapandisha vyeo watumishi 191, kuthibitisha kazini 54, kuajiri 432 wa kada mbalimbali, kuwezesha mafunzo kwa watumishi 176 na kuwezesha watumishi 50 kushiriki katika michezo mbalimbali inayoratibiwa na SHIMIWI. Pia, Wizara itaendelea kuwezesha majukumu ya matawi ya vyama vya wafanyakazi (TUGHE na RAAWU) Wizarani na Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala bora, jinsia na UKIMWI kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu na kuwaelimisha watumishi juu ya uadilifu, maadili, wajibu na haki zao;

(ii) Kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu namna ya kuferejisha masuala ya jinsia katika mipango ya Wizara;

(iii) Kuelimisha watumishi kuhusu kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa;

(iv) Kufanya mapitio, kuchapisha na kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja;

(v) Kuendelea kutoa elimu kuhusu UKIMWI na huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU na wanaougua UKIMWI; na

(vi) Kuanzisha dawati la malalamiko na kufanyia kazi malalamiko yanayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014,

Wizara itaendelea kuhimiza watumishi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi, kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa na kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Aidha, Wizara itaimarisha Dawati la Jinsia na Dawati la Malalamiko, kuhamasisha watumishi kuhusu umuhimu wa kupima afya zao kwa hiari na kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU na wanaougua UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutayarisha na kusambaza taarifa za matukio mbalimbali kuhusu sekta za mifugo na uvuvi kupitia vyombo vya habari. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeandaa na kurusha hewani vipindi vya runinga 5 na redio 20 kuhusu sera, mikakati na mipango ya kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Pia, Wizara imendaa na kusambaza nakala 1,000 za kalenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaimarisha maktaba ya Wizara na kuipatia vifaa muhimu; kukamilisha na kuchapisha Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara; kuandaa na kurusha hewani vipindi vinne vya runinga na kumi vya redio kutangaza mafanikio ya sekta ya mifugo na uvuvi; na kuandaa na kusambaza nakala 1,000 za kalenda ya mwaka 2014 na 1,000 za vipeperushi juu ya utekelezaji ya majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeandaa Mkakati wa kutekeleza Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya Wizara na kuimarisha mfumo wa TEHAMA. Pia, imeboresha tovuti ya Wizara na kuiunganisha na mitandao ya vituo vya Mpwapwa, *TAFIRI* na Nyegezi, kwa lengo la kuweka msingi wa kutumia simu za mdahalisi *(internet)* na kuwezesha kutumia mfumo wa mikutano ya masafa *(video and teleconferencing).* Aidha, Wizara imeimarisha Kitengo cha TEHAMA kwa kukipatia watumishi na vitendea kazi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itajenga mfumo wa kompyuta wa kuhifadhi kumbukumbu na kufuatilia mzunguko wa majalada na kuendelea kuboresha tovuti ya Wizara kwa lengo la kuwawezesha wadau kupata taarifa mbalimbali za sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA),* imeendelea kutoa taarifa kwa wafugaji na wavuvi kuhusu upatikanaji wa maji na malisho na hali ya bahari na maziwa na kutoa maelekezo stahiki. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Mradi wa Taifa wa Biogesi, imebainisha maeneo yatakayojengwa mitambo ya mfano ya biogesi inayozingatia hali ya ukame katika mazingira ya ufugaji wa asili katika Wilaya za Arusha, Babati, Longido, Monduli, Hanang, Mbulu, Korogwe, Handeni, Dodoma, Kongwa, Bahi, Kondoa, Singida, Manyoni, Mwanga, Same na Arumeru. Vilevile, wadau 126 kutoka kwenye vikundi vya wavuvi wa Wilaya za Muheza, Bagamoyo, Mkinga na Rufiji wamehamasishwa kutumia teknolojia ya kukausha samaki kwa nishati ya jua. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza sekta binafsi kuwekeza katika matumizi ya boti za *fibre glass* ili kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza mitumbwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutekeleza mfumo wa utoaji tahadhari kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa wafugaji na wavuvi na kuhamasisha matumizi ya teknolojia zinazozingatia hifadhi ya mazingira na matumizi ya nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho na makongamano muhimu katika sekta za mifugo na uvuvi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuandaa na kushiriki katika maadhimisho na makongamano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa yakiwemo:-

(i) Siku ya Chakula Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 16 Oktoba kila mwaka. Katika mwaka 2012 maadhimisho na sherehe hizo zilifanyika katika Wilaya ya Kigoma yakiwa na "kaulimbiu ya Ushirika katika Kilimo;"

(ii) Siku ya Mvuvi Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 21 Novemba kila mwaka. Katika mwaka 2012 maadhimisho na sherehe hizo zilifanyika katika Wilaya ya Lindi yakiwa na kaulimbiu ya "Matumizi ya teknolojia sahihi katika

uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji, kuongeza uzalishaji, lishe, kipato na kupunguza kasi ya uvuvi kwenye maji ya asili;"

(iii) Maadhimisho ya Nanenane hufanyika tarehe 8 Agosti kila mwaka. Katika mwaka 2012 maadhimisho hayo yalifanyika Dodoma yakiwa na kaulimbiu ya "KILIMO KWANZA - Zalisha Kisayansi na Kiteknolojia Kukidhi Mahitaji ya Ongezeko la Idadi ya Watu;"

(iv) Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani ambayo iliadhimishwa kitaifa katika Manispaa ya Temeke tarehe 28 Septemba, 2012. Kaulimbiu ilikuwa ni Tushirikiane Kufanya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa kuwa Historia;

(v) Siku ya Wanyama Duniani ambayo iliadhimishwa tarehe 4 Oktoba, 2012 Kitunda, Dar es Salaam na kaulimbiu ilikuwa Tuwapende na Kuwathamini Wanyama Wetu;

(vi) Siku ya Veterinari Duniani iliyoadhimishwa tarehe 27 Aprili, 2013 ilikuwa na kaulimbiu "Chanja ili kulinda na kuzuia;"

(vii) Siku ya Maziwa Shuleni Duniani ilifanyika Mkoani Njombe tarehe 26 Septemba, 2012 ikiwa na kaulimbiu "Maziwa kwa Mtoto ni Afya na Chachu ya Mahudhurio;"

(viii) Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa Duniani iliyoadhimishwa tarehe 29 Mei - 1 Juni, 2013 katika Manispaa ya Songea ambapo kaulimbiu ilikuwa ni 'Fuga Ng'ombe wa Maziwa Boresha Kipato na Lishe';

(ix) Mkutano wa mwaka wa Wataalam wa Uzalishaji Mifugo *(Tanzania Society of Animal Production)* uliofanyika tarehe 23 - 26 Oktoba, 2012 katika Jiji la Arusha. Maudhui ya mkutano huo yalikuwa "Teknolojia Mpya za Kuongeza Tija Uzalishaji wa Mifugo na Uvuvi ili Kufikia Malengo ya Milenia;" na

(x) Mkutano wa mwaka wa Madaktari wa Mifugo

*(Tanzania Veterinary Association Scientific Conference)* uliofanyika tarehe 11 - 13 Desemba, 2012 katika Jiji la Arusha. Maudhui ya mkutano yalikuwa ni "Mchango wa Taaluma ya Veterinari katika Kuboresha Afya ya Jamii".

Katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuandaa na kushiriki katika maadhimisho na makongamano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Napenda kuzitambua na kuzishukuru nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC),* Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU),* Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya *Czech,* Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Jamhuri ya Watu wa China, Israel, Korea Kusini, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *FAO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO* na *WHO* na Mifuko ya Kimataifa ya *GEF* na *IFAD* kwa kuchangia katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nazishukuru Taasisi za Kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika; Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japan *(JICA),* Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea *(KOICA),* Shirika la Misaada la Ireland *(Irish Aid),* Shirika la Misaada la Marekani *(USAID),* Shirika la Misaada la Australia *(AUSAID),* Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza *(DfID),* Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika *(AU/IBAR),* Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE),* Shirika la Maendeleo la Uswisi *(SDC),* Shirika la Ushirikiano la Ujerumani *(GTZ), United Nations University (UNU),* Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA)* na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden *(SIDA),* kwa michango yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Pia, nayashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation, Association for*

*Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), The New Partnership for African's Development (NEPAD), International Livestock Research Institute (ILRI), World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFAM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute for Security Studies (ISS-Africa), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish* na *Marine Stewardship Council (MSC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani zangu za pekee kwa Wananchi wote, hususan wafugaji, wavuvi na wadau wengine kwa michango yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Nachukua nafasi hii kuwaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Jimbo la Kiteto na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukurani zangu kwa Katibu Mkuu - Dokta Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu - Dokta Yohana Budeba, Wakuu wa Idara na Vitengo, Taasisi na Watumishi wote wa Wizara, kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa na kufanikisha maandalizi ya bajeti hii. Vilevile, napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Same Magharibi kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Pia, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo ninapotekeleza majukumu ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi 47,180,225,000.00 kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi 38,206,909,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi 16,339,267,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi *(PE);* na shilingi 21,867,642,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC);* na

(ii) Shilingi 8,973,316,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 3,488,270,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 5,485,046,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani: *www.mifugouvuvi.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imekwisha kuungwa mkono, tunaingia sasa hatua inayofuata. Nitaomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua makadirio haya, lakini kwa niaba yake ninamwona Mheshimiwa Amina Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum,

Mjumbe wa Kamati na anakwenda kusoma Taarifa ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti na kwa niaba ya Kamati hiyo.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam tarehe 28 Machi na 2 Aprili, 2013. Katika vikao hivyo, Waziri alitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, changamoto za utekelezaji, malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati imeridhika kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni ya Kamati, isipokuwa kwa maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na bajeti ndogo na ucheleweshaji wa fedha pamoja na sababu mbalimbali za kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo katika kufikia malengo iliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

Moja, kushindwa kufikia malengo yaliyotarajiwa kutokana na kuchelewa kupata fedha zikiwemo fedha za

maendeleo za ndani na nje kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, fedha hutolewa kidogo kidogo kiasi kwamba, haziendani na mpango kazi. Kwa mfano, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2013 jumla ya Shilingi 22,422,553,000.95 tu zimetolewa, sawa na asilimia 56.04 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa upande wa fedha za maendeleo ni Shilingi 4,609,833,000 tu, sawa na asilimia 33.3 zimetolewa.

Mbili, uwekezaji mdogo wa Sekta za Mifugo na Uvuvi hasa katika usindikaji wa mazao ya mifugo na uvuvi na katika Bahari Kuu kunaathiri mchango wa sekta katika Pato la Taifa. Katika mwaka 2012, sekta za mifugo na uvuvi zilikua kwa asilimia 3.1 na 2.9 sawia na kuchangia asilimia 4.6 na 1.4 sawia katika Pato la Taifa.

Tatu, kasi ndogo ya Halmashauri katika kuainisha, kupima na kumilikisha maeneo ya ufugaji ili yawe endelevu, jambo ambalo limesababisha kwa kiwango kikubwa kuhamahama kwa mifugo na hivyo kusababisha migogoro mingi baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na hasa wakulima.

Nne, kuenea kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo, hususan magonjwa ya milipuko kutokana na ufugaji wa kuhamahama na usiozingatia uwezo wa malisho kuhimili wingi wa mifugo. Magonjwa hayo ni pamoja na homa ya mapafu, mdondo, mapele ya ngozi, kichaa cha mbwa, mafua makali ya ndege na kadhalika.

Tano, kutopatikana kwa mikopo ya kutosha na yenye masharti nafuu kwa shughuli za ufugaji na uvuvi ikilinganishwa na mahitaji yao. Aidha, gharama za pembejeo na zana kwa ajili ya ufugaji na uvuvi ni kubwa na kufanya wafugaji na wavuvi kushindwa kuzinunua.

Sita, uhaba wa Maafisa Ugani wa Mifugo na Uvuvi ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam hao katika Halmashauri. Kwa mfano, mahitaji ya wagani wa mifugo na

uvuvi kwa nchi nzima ni 17,525 na 16,000 sawia, ikilinganishwa na wagani wa mifugo na uvuvi waliopo 5,197 na 436 sawia.

Saba, ukosefu wa mbegu bora za mifugo na samaki, pembejeo na huduma hafifu ya uhamilishaji *(Artificial insemination*).

Nane, ukosefu wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi na hasa katika maeneo ya vijijini.

Tisa, ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi. Hali hii imesababisha kupungua kwa samaki katika bahari, maziwa na mito, uharibifu wa mazalia ya samaki na uharibifu wa mazingira kwa ujumla.

Kumi, elimu duni ya ufugaji bora, ufugaji usio wa kibiashara na matumizi duni ya teknolojia za kisasa kwa wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, ili kutekeleza majukumu yake, Wizara chini ya Fungu 99, inaomba jumla ya Shilingi 47,180,225,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 38,206,909,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 8,973,316,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, Shilingi 3,488,270,000 ni fedha za ndani na Shilingi 5,485,046,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki kilichotengwa ni kidogo na hakiwezi kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa majukumu muhimu ya Wizara ili kuwezesha kufikia malengo ya utoaji wa huduma kwa wafugaji na wavuvi kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010 ya Chama cha Mapinduzi na maelekezo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikipata bajeti ndogo na bajeti hiyo imekuwa ikipungua mwaka hadi

mwaka na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, Kamati imebaini kuwa mchango wa Washiriki wa Maendeleo *(DPs)* kwa mwaka 2013/2014, umepungua kutoka Shilingi 9,439,483,000 mwaka 2012/2013 hadi Shilingi 5,485,046,000. Hii imetokana na kukamilika kwa Mradi wa *MACEMP* na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP).* Hata hivyo, Kamati imeridhika na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuandaa miradi na programu mbadala kufuatia kukamilika kwa miradi na programu tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za ndani za Maendeleo, Kamati imebaini kuwa, bajeti iliyotengwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2013/2014 ni Shilingi 3,484,270,000, ikilinganishwa na Shilingi 4,000,000,000 mwaka 2012/2013. Aidha, Kamati imebaini kuwa fedha za Maendeleo kwa mwaka 2013/2014 ni tegemezi kwa asilimia 61, yaani Shilingi 5,485,046,000. Kiasi hiki kilichotengwa ni kidogo na hakiwezi kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa majukumu muhimu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa, pamoja na fedha ndogo zinazotengwa, fedha hizo hazitolewi kama ilivyopangwa na kwamba zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri wa Kamati uliotolewa mwaka jana kuhusu umuhimu wa Wizara hii kuongezewa fedha, Kamati imesikitishwa kuona kwamba, Bajeti ya Wizara imeshuka zaidi kutoka Shilingi 54,566,124,000 mwaka 2012/2013 hadi Shilingi 47,180,225,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Wizara iliomba Shilingi bilioni 163 ili kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi, kwa kasi inayoendana na Kaulimbiu ya KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu wa

Bajeti ya Wizara hii, Kamati inaishauri Serikali iongeze Bajeti ya Wizara kiasi cha Shilingi 40,000,000,000 na kufikia Shilingi 87,180,225,000 kwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele muhimu kama vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali. Maeneo yanayoombewa fedha ni yale ambayo Kamati inaona yatakuwa na matokeo ya haraka katika kuboresha maisha ya wafugaji na wavuvi na hivyo kuongeza Pato la Taifa kwa ujumla. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo:-

Moja, kuwezesha Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)*, kuongeza idadi ya mifugo, kupanua programu ya unenepeshaji, kupanua machinjio ya Dodoma na kukamilisha ujenzi wa machinjio ya Ruvu. Shilingi 5,000,000,000.

Mbili, kuendeleza kuboresha miundombinu ya mifugo na uvuvi kwa kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Mbegani - Bagamoyo. Hii itawezesha kujenga bandari ambayo itakuza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika Pato la Taifa, kuvutia wawekezaji, kukuza ajira na kipato cha wavuvi kwa ujumla. Shilingi 11,000,000,000.

Tatu, kuanzisha mfumo wa ruzuku kwa wavuvi na wafugaji. Kwa upande wa mifugo, ruzuku hii itatumika kwa ununuzi wa madawa ya kuogeshea na chanjo za mifugo na hivyo kupunguza vifo vya mifugo vitokanavyo na magojwa yaenezwayo na kupe hususan Ndigana Kali *(ECF).* Kwa upande wa uvuvi, ruzuku itatumika kwa ununuzi wa zana za uvuvi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa boti, injini za boti, nyavu na mishipi na ruzuku ya uzalishaji wa chakula bora cha samaki na vifaranga. Aidha, Mfumo huu utawawezesha wavuvi wadogo wadogo kuvua kwenye maji ya kina kirefu na *Exclusive Economic Zone (EEZ)* na kutoa ajira kwa vijana na kuboresha maisha ya jamii za wavuvi. Shilingi 4,000,000,000.

Nne, katika eneo la Utafiti na Mafunzo yafutayo yatatekelezwa: Kuimarisha utafiti wa mifugo na uvuvi kwa kuboresha miundombinu ya *TAFIRI, TALIRI* na maabara za *TVLA;* Kufanya utafiti wa magonjwa ya mifugo na

kutengeneza chanjo zake na Kusomesha watafiti wa kutosha kwa ajili ya Taasisi za utafiti. Shilingi 9,500,000,000.

Tano, kudhibiti uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi, kwa kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa meli baharini na katika maziwa (*Vessel Monitoring*) na kudhibiti meli za kimataifa zinazoiba samaki kwenye eneo letu la Bahari Kuu *(EEZ).* Shilingi 5,505,000,000.

Sita, kuimarisha usimamizi, ukaguzi na udhibiti wa huduma za mazao ya mifugo na uvuvi kwa kuimarisha Bodi za Mazao ya Mifugo na Uvuvi, Baraza la Veterinari Tanzania na wakaguzi wa mazao ya mifugo na uvuvi. Shilingi 5,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutafuta kiasi cha Shilingi 40,000,000,000 kinachoombwa ili kuboresha huduma za sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya kuzalisha vifaranga wa samaki na kununua mitambo ya kuzalisha vyakula bora vya samaki. Kamati inaishauri Serikali kujenga na kuboresha miundombinu ya kuzalisha vifaranga vya samaki kwa kuanzia na vituo vitano vya Ruhila (Songea Manispaa), Mwamapuli (Igunga), Mtama (Lindi), Kibirizi (Kigoma) na Nyamirembe (Chato). Hii itasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa vifaranga na kuongeza uzalishaji kutoka vifaranga 5,000,000 (2012/2013) hadi 16,000,000 (2014/2015).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kujenga malambo makubwa ya maji kwenye maeneo ya wafugaji yakiwemo maeneo ya Mbangala (Chunya), Miteja (Kilwa), Mji Mwema (Lindi), Mbondo (Nachingwea) na Kwamaliga (Kilindi). Aidha, Wizara ianzishe vituo vipya vya kuzalisha mbegu bora za malisho. Hatua hizi zitasaidia kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali

kuimarisha huduma za uhamilishaji wa mifugo kwa kuendeleza ujenzi wa Kituo cha uhamilishaji cha Sao Hill - Iringa na vituo vipya vitano vya uhamilishaji vya Tabora, Kagera, Tanga, Manyara na Katavi na kuimarisha *National Artificial Insemination Centre (NAIC)*, kilichoko Arusha na mashamba matano ya kuzalisha mitamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji imekuwa sugu na kila siku migogoro mipya inaibuka na kusababisha maafa makubwa. Kamati inashauri yafuatayo:-

Serikali ipeleke huduma muhimu katika maeneo ya wafugaji; Serikali iharakishe zoezi la upimaji vijiji na kutenga maeneo ya ufugaji; na Kwa kuwa suala hili ni mtambuka, Wizara ishirikiane na Wizara nyingine kama Ardhi, Kilimo, Maliasili, Maji na TAMISEMI ili washirikiane kutatua migogoro inayojitokeza kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa bajeti ya Wizara hii, Sekta ya Mifugo na Uvuvi haijaweza kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa na kuboresha maisha ya Wafugaji na Wavuvi licha ya kuwa na rasilimali kubwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla - Mwenyekiti, Mheshimiwa Said J. Nkumba - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Abdusalaam Selemani Amer, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma, Mhesheshimiwa Moshi Selemani

Kakoso, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka na Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ya Shilingi 47,180,225,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 38,206,909,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 8,973,316,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, Shilingi 3,484,270,000 ni fedha za ndani na Shilingi 5,485,046,000 ni fedha za nje, ikiwa ni pamoja na nyongeza iliyoombwa ya Shilingi 40,000,000,000 ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuleta tija kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Amina Makilagi, kwa kuwasilisha taarifa kwa niaba ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, hatua inayofuata sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hiyo na ninamwona Mheshimiwa Rose Kamili, atatoa maoni ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. ROSE K. SUKUM (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Hotuba hii iingie kwenye Hansard kama nilivyowasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba hii inatolewa chini

ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha kuwa, rasilimali za mifugo na uvuvi zinaendelezwa na kutunzwa katika mazingira endelevu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya Wananchi. Aidha, dira inalenga kuhamasisha ufugaji wa kisasa na uvuvi endelevu ili kujenga uchumi endelevu kwa jamii nzima ya wafugaji na wavuvi na taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya ukweli kwamba, wafugaji na wavuvi wana mchango mkubwa katika uchumi wetu, Serikali hii ya CCM imeshindwa kuwapatia maeneo maalum kwa ajili ya malisho kwa maendeleo ya mifugo yao. Wafugaji wamekuwa wakihamishwa na au wakifukuzwa kutoka eneo moja la nchi hadi eneo lingine kama vile hawana haki ya kufanya shughuli za kiuchumi kama ufugaji katika nchi yao. Ni aibu kwa Serikali kushindwa kuwapatia wafugaji mahitaji muhimu ambayo yangepelekea ufugaji wao kuwa wa kisasa, kibiashara na endelevu kama ilivyobainisha katika dira ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, haioni sababu ya Serikali kutowapatia wafugaji maeneo ya kufugia kwa kuwa wafugaji wangeweza kuingia ubia na mashamba makubwa ya mifugo ambayo yalikuwa yanamilikiwa na Ranchi za Taifa; lakini kutokana na ubinafsi na ufisadi uliofichwa kwenye kivuli cha cha sera ya ubinafsishaji, Serikali ya CCM imesimamia zoezi la Viongozi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi wakigawiana ranchi hizo na kuwaacha wafugaji wakifukuzwa ovyo na kupewa jina la wachungaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wavuvi, hali ni hiyo hiyo, kwani mapato mengi ya Serikali yanayokusanywa kutoka katika Sekta ya Uvuvi yanatokana na wavuvi wadogo ambao mara zote wao ndiyo waathirika wa mfumo kandamizi wa Serikali. Zana za uvuvi zinapokamatwa, wao

ndiyo wanapata hasara, lakini wauzaji wa zana hizo za uvuvi wala hawaulizwi na wala hakuna hatua zinazochukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayozikabili sekta hizi za ufugaji na uvuvi ni kwamba, sekta zote mbili hazina bima dhidi ya majanga ambayo yanaweza kutokea. Katika mazingira kama haya, dhana ya kuwa sekta za kisasa au kibiashara na endelevu inakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, iliainisha upungufu mkubwa wa kiutendaji na kiuwajibikaji kwa Wizara hii na kuitaka Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

Moja, kuwajibika kwa uzembe wa kuitelekeza meli ya uvuvi ya Tawariq iliyokamatwa ikifanya uvuvi haramu katika ukanda wa bahari ya hindi hadi meli hiyo kuharibika kabisa na kuanza kuzama bila faida yoyote?

Mbili, kuchukua hatua dhidi ya mwekazaji wa *Kagera Sugar* kwa kushindwa kuendeleza shamba la ukubwa wa hekta 45,000 (sawa na ekari 112,500) kinyume na mkataba.

Tatu, kueleza sababu za kuwapa mashamba makubwa wawekezaji wa kigeni na kuwanyanyapaa wafugaji wa asili kinyume cha sheria.

Nne, kutatua migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji ambayo mara kadhaa imesababisha uvunjifu wa amani na umwagaji damu miongoni mwa Wananchi.

Tano, kujenga viwanda vya kusindika nyama katika mikoa ya wafugaji ili kuongeza thamani ya bidhaa ya nyama na hivyo kukuza uchumi.

Sita, kuweka wazi kiasi cha fedha kinachopatika kama mrabaha kutokana na uvuvi katika Bahari Kuu, pamoja

na fedha za leseni kwa meli zinazofanya uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo ina nafasi kubwa katika kujenga uchumi imara wa Taifa, kuongeza kipato kwa Watanzania wanaotegemea mifugo na kutoa fursa za ajira sanjari na kuhifadhi rasilimali za Taifa. Sera ya Mifugo inaeleza nia ya Serikali na wadau wengine katika kukabiliana na changamoto zinazokabili Sekta ya Mifugo. Lengo kubwa ni kujenga mazingira mazuri yatakayotoa fursa za kuongeza kipato na ajira kwa wafugaji wadogo, kufuga kibiashara na kuongeza ajira. Ili kufikia haya, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutekeleza malengo makuu matatu ya kisera kama ifuatavyo:-

Moja, kuendeleza Sekta ya Mifugo itakayokuwa na mwelekeo wa kibiashara, yenye ufanisi na itakayohimili ushindani wa kimataifa;

Mbili, kuibua mifumo bora ya uzalishaji itakayoongeza tija miongoni mwa wafugaji wadogo na wa asili; na

Tatu, kuhifadhi rasilimali za mifugo na kuunda sera na taasisi zitakazosimamia maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali hizo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera hiyo ya Mifugo imeweka wazi azma ya Serikali ya kuboresha Sekta hii ya Mifugo, lakini kutokuwepo na mkakati madhubuti wa kufanikisha yale yote yanayohitajika kufanyika na Sera hii ya Mifugo ya mwaka 2006, kunaendeleza matatizo katika Sekta hii mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo hapa nchini ina nafasi kubwa katika ujenzi wa uchumi wa Taifa. Kwanza, kwa kuthamanisha kiwango cha nyama kinachotumika kila siku hapa nchini ikiwa kiwango hicho kingekuwa kinaagizwa toka nje ya nchi. Pili ni kuongeza kipato kwa Watanzania wanaotegemea mifugo na kutoa fursa za ajira sanjari na kuhifadhi rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba makubwa ya mifugo yana uwezo wa kuongeza viwango vya uzalishaji na uuzaji wa mifugo na mazao yake nje ya nchi, ajira na kuboresha maisha ya wafanyakazi wake. Mkakati umetumika wa kugawa mashamba makubwa ya Kampuni ya Ranchi za Taifa KARATA (*NARCO*) na yale yaliyokuwa chini ya Kampuni ya Ng'ombe wa Maziwa (*DAFCO*) kuwa mashamba yenye ukubwa wa kati kwa ajili ya ufugaji wa kibiashara unaolenga kutekeleza dhana hii. Mkakati huu umeongeza upeo wa umilikaji mashamba na pia kuwawezesha Watanzania kuingia katika ufugaji wa kibiashara. Maeneo ya Ranchi za KARATA (*NARCO*) yaliyobaki, yataendelea kutumika kama ranchi za mfano na maeneo yasiyo na magonjwa ya mifugo kwa ajili ya soko la nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM ya mwaka 2005 – 2010, aya ya 32 inasema kwamba: "Pamoja na kwamba, Tanzania ina mifugo mingi sana, mchango wa mifugo kwenye Uchumi wa Taifa ni mdogo. Kwa lengo la kuendeleza Sekta ya Mifugo ili ichangie zaidi ukuaji wa Uchumi wa Taifa na kuwaongezea kipato wafugaji, Serikali za CCM zitaendeleza kwa msisitizo zaidi lengo la kuzingatia zaidi ubora kuliko wingi pekee katika ufugaji. Ili kufikia lengo hilo, hatua zifuatazo zitachukuliwa katika kipindi cha 2005 - 2010:-

- Kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongezea thamani mazao ya mifugo kama vile ukataji nyama, usindikaji wa maziwa, utengenezaji wa bidhaa za ngozi na kadhalika. Huu ni usemi wa Sera ya CCM.

- Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015, aya ya 38 inasema kwamba: "Katika kipindi cha Ilani hii ya miaka 2010 - 2015, Chama cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kuiendeleza Sekta ya Mifugo kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi ili kuiwezesha kutoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

- Serikali iandae Programu Kabambe ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo na Ufugaji. Programu hiyo

ijumuishe pamoja na mambo mengine, masuala ya uendelezaji wa maeneo ya malisho, kuchimba na kujenga malambo, mabwawa, majosho na huduma za ugani ili hatimaye wafugaji waondokane na ufugaji wa kuhamahama.

- Benki ya Kilimo itakayoanzishwa iwe pia Benki ya Mifugo ili iweze pia kutoa mikopo kwa wasomi wenye nia ya kufuga na kuwawezesha kuingia kwa wingi katika ufugaji wa kisasa.

- Kuelimisha wafugaji uwiano kati ya idadi ya mifugo na eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuonesha kuwa CCM yale wanayoyaandika siyo wanayosimamia, katika kuinua Sekta ya Ufugaji hasa wa asilia ambao unachangia zaidi ya asilimia 85 ya ufugaji wote. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza kwa mkakati huo wa CCM dhidi ya wafugaji na ufugaji ni kwa vipi ufugaji unaweza kuwa endelevu na wa kisasa wakati wafugaji wanaporwa maeneo ya kulishia mifugo yao, hawapewi maeneo ya malisho, hawapati huduma za ugani, hawapati mikopo na hawana soko la uhakika wa bidhaa zinazotokana na mifugo.

Kambi Rasmi ya Upinzani, inauliza kwa makati huo wa CCM dhidi ya wafugaji na ufugaji ni kwa vipi ufugaji unaweza kuwa endelevu na wa kisasa wakati wafugaji wanaporwa maeneo ya kulishia mifugo yao, hawapewi maeneo ya malisho, hawapati huduma za ugani, hawapati mikopo na hawana soko la uhakika? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa kauli juu ya ni wapi wafugaji wa asili watafugia mifugo yao ili kuwa endelevu na ya kisasa?

Kwa mfano, wafugaji na wakulima wa vijiji vinne vya Makuyuni, Loikisale, Naiti na Mswakini katika Wilaya ya Monduli, wanatishiwa kuhamishwa kutokana na mkakati mahususi ulioasisiwa na Mheshimiwa Waziri Kagasheki wa kutangaza maeneo hayo kuwa ni *Wildlife Management Area (WMA*). Uhakika ni kwamba, *WMA* hiyo ni hewa haipo na

ukweli ni kwamba, eneo hilo linapewa kikundi kinachoitwa ELEWANA AFRIKA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza Wafugaji hao ni wapi wanakokwenda na mifugo yao. Aidha, kwa kuwa utaratibu wa kuanzisha *WMA* huwa inaanzishwa kwa kupata ridhaa za wanavijiji ambao kwa hiari yao wanatoa maeneo ya vijiji vyao kuwa *WMA* na ndipo kazi ya Waziri husika inafuata ya kutoa idhini ya uanzishwaji wa hiyo *WMA*. Kwa kuwa huo ndiyo utaratibu wa kuanzisha *WMA*; je, ni kwa nini vijiji hivyo havikupewa fursa hiyo ambapo ni sawa na Loliondo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa ardhi katika eneo la Loliondo ni taswira nyingine ya jinsi ambavyo Serikali ya CCM imekiuka haki za Wafugaji wa Kimaasai kwa manufaa ya wawekezaji wa kigeni katika Sekta ya Uwindaji wa Kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa Loliondo bado haujapatiwa ufumbuzi na sasa umeanzishwa mgogoro mwingine Wilaya ya Monduli. Hii ni kwa makusudi kuhakikisha wafugaji wa asili wanakwisha kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo kabla ya uhuru Serikali ilitenga eneo la zaidi ya hekta 18,000, sawa na ekari 45,000, Wilayani Maswa, lililojulikana kama *SHISHIYU Holding Ground* kwa ajili ya kunenepesha mifugo kabla ya kusafirishwa kwenye kiwanda cha Nyama cha *Tanganyika Packers*, ambacho kimekufa. Cha ajabu ni kwamba, katika eneo hilo bado hadi sasa Wafanyakazi wa Idara ya Mifugo wapo pale lakini mifugo haineneрeshwi. Je, hii siyo hujuma kwa Sekta ya Mifugo na Wafugaji hasa wa Wilaya ya Maswa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, bali pale Ipala Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora, kuna kituo cha treni kilichokuwa kikitumika kupakia ng'ombe kwenda Dar es Salaam. Eneo hilo lilikuwa limetengwa rasmi kwa ajili ya mifugo na kuna miundombinu ya kupakia mifugo kwenye treni. Jambo la ajabu ni kwamba, Serikali imeligeuza eneo

lile kuwa hifadhi ya misitu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa wafugaji wanaoishi eneo hilo waachiwe eneo litumike kwa malisho na miundombinu iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kitendo kinachofanywa na Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kuwahamisha wafugaji kwa nguvu katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwa kuwalipisha mamilioni ya fedha wafugaji hao. Kwa mfano, mfugaji mmoja wa Mikumi alitozwa faini ya shilingi milioni 42.78 kwa kukamatwa ng'ombe wake na mwingine ni mfugaji wa Chunya zaidi ya shilingi milioni 19 na kadhalika, nao ni ushahidi wa dhahiri kwamba, Serikali hii ya CCM haina dhamira ya dhati katika kuhakikisha wafugaji na ufugaji unakuwa na tija katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wa asili ya Kisukuma, Kimasai, Wairaq na Wabarbaig katika Wilaya za Kilombero, Ulanga, Kilosa, Mbarali, Chunya, Kilindi, Handeni, Mpanda, Rufiji na kadhalika, wamepata matatizo makubwa sana na wengine wameuawa na Vyombo vya Dola. Kosa lao kubwa ni kuwa na mifugo mingi iliyosababisha wahame toka Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini kwa sababu za malisho. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge, je, kosa la ndugu zetu hao ni kuwa na utajiri wa mifugo mingi au nini hadi wanadharauliwa na kunyanyaswa na kufanywa kuwa Watanzania wa daraja la nne katika nchi yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kwamba, Wizara imeshindwa kuwatetea na kuwalinda wafugaji wa asili; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wafugaji ni Wizara gani itakayosikiliza na kutatua matatizo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imekuwa ikitokea katika maeneo ya Ranchi zilizokuwa za Mkoa wa Kagera, Rukwa, Morogoro, Tanga na Pwani, watu waliopewa ekari 4,000 au ekari 10,000 za maeneo ya Ranchi za Taifa kama wawekezaji, watu hao wameshindwa kuziendeleza

ranchi hizo kwa vile wengine hawana hata mifugo ya kuweka katika maeneo hayo. Kukosa mifugo ya kuendeleza eneo hilo, kwa makusudi watu hao huona kuwa mbadala unaobakia ni kupangisha maeneo hayo kwa wawekezaji kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa ni jambo la busara kama ushirika wa wafugaji au mwekezaji mmoja mmoja kupewa ekari 1,000 ikiwa eneo lote la ekari 10,000 lingegawanywa ili kurahisisha uwekezaji wake na kufanya kuwa endelelevu. Kwa eneo dogo uwezekano wa kupata mkopo toshelezo kwa uwekezaji toka benki zetu na asasi zingine za fedha ni rahisi kwani hata *investment risk* inakuwa ni ndogo na inakuwa imesambaa kwa wawekezaji wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri akijibu swali namba 26 kuhusu maeneo ya Ranchi za Mkoa wa Kagera; je, kwa nini Serikali isiyarudishe maeneo hayo kwani waliopewa wanayakodisha kwa wafugaji toka nchi jirani? Je, ni Watanzania gani kwa majina waliogawiwa maeneo kwenye ranchi hizo? Orodha ya majina ya Wawekezaji Watanzania waliogawiwa maeneo hayo ya Ranchi ipo, nitaomba kukutana na Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa ili nimkabidhi orodha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa hivi majina hayo ya wamiliki, Waziri ameshindwa kuyatoa kama alivyoahidi ndani ya Bunge. Hoja ni kwamba, kama kweli wamiliki ni Watanzania; kwa nini wanashindwa kuweka majina hadharani? Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri kutoa kwa Wabunge majina hayo ya wamiliki na uraia wao hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuiwezesha Sekta ya Mifugo kutoa mchango stahiki kwa Taifa hili ni lazima uboreshaji katika Sekta ya Mifugo ufanyike kwani wanachokosa wafugaji wetu ni ardhi na elimu ya ufugaji yenye mafanikio kutokana na kutumia mbinu za zamani za kuzalisha mifugo.

Changamoto kubwa katika Sekta hii ni kukosekana kwa mbinu za kisasa, vifaa na madawa ya uhakika kuhudumia wanyama. Aidha, mifugo mingi inatunzwa kienyeji na matokeo yake kukosa soko la kimataifa kama zilivyo nchi nyingine. Kama elimu ya kutosha itatolewa na kuruhusu wawekezaji wa ndani katika Sekta ya Mifugo, changamoto hizo zitapungua kwa kiasi kikubwa na hivyo kutoa nafasi ya ongezeko la bidhaa zitokanazo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema wawekezaji wa ndani, kwa maana kwamba, wafugaji wa asili wao mtaji wao mkubwa ni mifugo na *NARCO* wao mtaji wao ni utaalam na miundombinu iliyopo tayari. Hivyo basi, ni rahisi ubia huo kati ya wafugaji wa asili na *NARCO* kuleta tija zaidi kuliko mwekezaji toka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, kipato na ukuaji wa miji kwa nchi zinazoendelea Duniani, Tanzania ikiwa ni mojawapo, mahitaji ya bidhaa za mifugo nayo yamekuwa yakiongezeka pia. Takwimu zinaonesha kuwa, Tanzania pekee itaongeza mahitaji mara nne kwa mwaka 2030. Hivyo, ni jukumu la Serikali sasa kulieleza Bunge hili ni kwa vipi Wizara imejipanga kukabiliana na changamoto ya ongezeko hilo la mahitaji ya nyama kwa muda huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ni asilimia mbili tu ya mifugo yote inayozalishwa na kufugwa kibiashara, hivi sasa Tanzania ina machinjio ya kisasa manne ambayo hayatoshelezi kwani mahitaji ya nyama safi na salama yanaongezeka kila siku. Aidha, inaonesha kuwa, chini ya asilimia moja ya nyama yote iliyosindikwa ndiyo inazalishwa hapa nchini na sehemu yote iliyobaki inaagizwa na kuingizwa nchini kutoka Kenya. Vilevile taarifa hiyo inaonesha kuwa zaidi ya tani 700 ya nyama safi inaaagizwa toka nje ya nchi kila mwaka wakati mahitaji ya nyama ndani ya nchi na Kanda yetu ya ushirikiano yanazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya pili nyuma ya Ethiopia kwa kuwa na mifugo mingi katika Bara la

Afrika. Sasa kwa hali ya kawaida tu; inakuwaje nchi yetu inaagiza nyama kutoka nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina rasilimali kubwa ya maliasili ikiwemo ardhi, malisho na idadi kubwa ya mifugo. Kati ya jumla ya hekta milioni 94 za rasilimali ya ardhi, hekta milioni 60 ni nyanda za malisho zinazofaa kwa ufugaji. Kwa sasa kuna ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15.2 na kondoo milioni 6.4. Mifugo mingine ni pamoja na nguruwe milioni 1.9 na kuku wa asili milioni 58.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2013/2014, Kiambatanisho Na. 3 kinaonesha kuwa, kwa mikoa 21, wilaya 69 na vijiji vilivyopimwa 479, eneo la malisho ambalo linasadikiwa kuwa limetengwa kwa ajili ya wafugaji kuwa ni hekta milioni 1.28. Hii ni sawa na asilimia 2.13 ya hekta milioni 60 za nyanda za malisho katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri awaeleze wafugaji kwa ng'ombe milioni 21.3 na mbuzi na kondoo milioni 21.5 wanatakiwa wachungwe kwenye eneo la ukubwa gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mifugo umegawanyika katika mifumo mikuu miwili ambayo ni ufugaji huria na ufugaji shadidi. Mfumo wa ufugaji shadidi japo siyo mkubwa nchini, unatiliwa mkazo zaidi katika kuendeleza ufugaji na uwekezaji kwani unachangia zaidi kwenye uchumi wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, mfumo wa ufugaji huria ambao hufanywa na wakulima-wachungaji na wachungaji-wahamaji, ni mfumo unaotegemea upatikanaji wa malisho na maji kwa msimu na matokeo yake husababisha wafugaji kuhamahama. Mfumo huu unakabiliwa na matatizo ya utunzaji duni wa mifugo, matumizi duni ya teknolojia za kisasa, kuhodhi mifugo

wengi zaidi ya uwezo wa ardhi na ukosefu wa mazingira mazuri ya masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Asasi ya Kiraia ya *Tanzania Pastoralists, Hunters and Gatherers Organization* (*TAPHGO*), kuhusu mfumo wa biashara ya mifugo Tanzania, inaonesha kwamba, Sekta ya Ufugaji Tanzania inachangia asilimia 18 ya Pato la Taifa, uzalishaji wa nyama kwa mwaka unakadiriwa kuwa ni tani 259,800, kwa mifugo inayofugwa kwa ajili ya nyama pekee huchangia tani 181,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mchango wa wafugaji ambao pia ni wakulima huchangia asilimia 98 ya uhitaji wote wa nyama hapa nchini, huku asilimia mbili hutoka kwenye Ranchi za Taifa. Wakati mbuzi na kondoo huchangia tani 75,800. Thamani ya nyama inayozalishwa inakadiriwa kuwa ni shilingi bilioni 727.44, kati ya hizo shilingi bilioni 537.94 zinachangiwa na nyama ya ng'ombe na zilizobaki shilingi bilioni 189.5 ni kwa mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa kufungua mkutano wa uwekezaji kwa shabaha ya kuibua maendeleo ya Mkoa wa Mara, kwa kutumia rasilimali na utajiri uliopo mkoani Mara, lazima tuanze kutekeleza misingi ya ufugaji wa kisasa na tujipange vizuri kwa uwekezaji kwenye sekta hii.

Naomba tutenge maeneo maalum ya ufugaji wa kisasa. Kwa mfano, tukigawa maeneo ya ukubwa wa hekta 2,000 kila moja na tukawagawia watu kwa ajili ya kufuga kisasa, watakaopewa maeneo hayo wahimizwe na kusaidiwa wayaendeleze kwa malisho na huduma muhimu za maji, majosho, pamoja na za matibabu kwa mifugo. Maeneo hayo yakitumiwa kunenepesha ng'ombe wa nyama, tunawezesha kuwepo kiwanda cha nyama kitakachonunua toka kwao mifugo ya kuchinja. Kiwanda hicho kitatengeneza soko la uhakika kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hiyo ya Mheshimiwa

Rais imekuja muda ambao tayari maeneo mengi mazuri yaliyokuwa yanamilikiwa na Serikali yamekwishachukuliwa. Kama utaratibu ambao tumejaribu kuutolea maelezo kwa kuangalia Ranchi za Mkoa wa Kagera jinsi gani migogoro iliyopo haimaliziki kutokana na ukweli kwamba wahusika wakuu katika migogoro hiyo ni Watendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayoikabili tasnia ya mifugo ni namna ya kufikia viwango vya ubora wa mifugo na mazao yake vitakavyokidhi mahitaji ya soko la kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuonesha kuwa watendaji wanashindwa kutenganisha kati ya machinjio ya kisasa na viwanda vya kusindika ni pale Waziri alipokuwa anajibu swali namba 27 kwa mujibu wa *Hansard; "Je, hivi sasa kuna viwanda vingapi vya nyama na vinasindika kiasi gani cha nyama?"* Jibu la Waziri lilikuwa: "Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inahitaji viwanda ama machinjio makubwa takribani 16, yenye uwezo wa kuzalisha nyama tani 133 kwa siku kwa kila kiwanda au kila machinjio."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza tena ni kwa njia zipi utekelezaji wa Ilani unaweza kufikiwa kama tafsiri ya kiwanda cha kusindika nyama na machinjio inaonekana kuwa ni kitu kimoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida, ng'ombe wa asili hutoa maziwa lita 0.5 kwa siku wakati yule wa kisasa anatoa kati ya lita 7 – 30 kwa siku kutegemeana na matunzo na elimu ya ufugaji aliyonayo mfugaji. Hivyo basi, ili mfugaji wa ng'ombe wa asili aweze kupata lita 30 za maziwa kwa siku, atahitaji kuwa na ng'ombe 15. Mbali na mambo hayo yote ambayo yataenda na uwiano huo, lakini jambo la muhimu kwa mfugaji wa asili ni kwamba, madawa yanayohitajika kwa chanjo, kuosha na kutibu magonjwa ni zile zile kwa ng'ombe wote wa asili na wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sekta hii ya mifugo iweze kuleta tija inayokusudiwa, huduma ya ugani ni muhimu sana,

lakini kwa mtindo wa utendaji kazi kwa watoa huduma hiyo ulivyo ni dhahiri tija inayotegemewa ni vigumu kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na watoa huduma kutokuwa na idadi maalum ya wafugaji wanaowahudumia, eneo maalum na hivyo kuweza kuwajibika kwa matokeo yatakayopatikana katika eneo husika ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa ni vyema kama kila afisa ugani atakuwa na orodha kamili ya wafugaji anaofanya nao kazi katika eneo maalum, kwani utaratibu huo utarahisisha upatikanaji wa kumbukumbu sahihi na pia kuweza kupima utendaji wa afisa huyo.

Kwa mfano, kwa maafisa ugani wanaofanya kazi Mkoa wa Kagera, ambao ni Watumishi wa Serikali (Ndg. Patrick, Ndg. Kashankoro, Ndg. Kanyambo na Ndg. Mutabazi), hawa wote wanamiliki Vitalu vya Ranchi. Hoja ni je, utaratibu wa watendaji wa Serikali kujimilikisha mali za Wananchi unaendelea hata kwenye ngazi ya chini? Je, mgongano wa masilahi katika suala hili unashughulikiwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri Kivuli wa Fedha akiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kwenye Muswada wa Fedha, tarehe 16 Agosti, 2012 alisema yafuatayo: “Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 12 cha Muswada, Serikali inatoa pendekezo la kufanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mauzo ya Nje ya Nchi, Sura ya 196, kwa kuweka jedwali jipya ambalo linaongeza viwango vya tozo kwenye ngozi ghafi inayosafirishwa kwenda nje ya nchi. Kama Serikali ina mpango madhubuti wa kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini na kuleta tija kiuchumi ni dhahiri kuwa inatakiwa kusitisha uamuzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yetu ya bajeti tulipendekeza kuwa, Serikali izuie kabisa ngozi ghafi kusafirishwa nje ya nchi na badala yake, ijikite kutafuta uwezekano wa kuitumia ngozi hiyo hapa nchini na kuanzisha viwanda vya kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi hiyo.

Hata Kamati ya Fedha na Uchumi ilikuwa na mapendekezo hayahaya. Hii ni kutokana na manufaa makubwa ya kiuchumi wanayopata wenzetu hasa nchi ya Ethiopia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, wenzetu wa Uganda na Rwanda nao wamezuia ngozi ghafi kuuzwa nje ya nchi. Mapendekezo haya ya Serikali yakibaki kama yalivyo, hayataifanya Serikali kupata mapato yanayostahili kwa sababu wafanyabiashara wengi wanatoa takwimu zisizo sahihi kuhusu mauzo halisi watakayokuwa wanauza nje ya nchi *(under invoicing).*

Mapato ambayo Serikali inahofia kuyapoteza kwa kupiga marufuku uuzaji wa ngozi ghafi nje ya nchi, yatapatikana tena kwa kiasi kikubwa kutokana na ajira zitakazopatikana katika viwanda vya kusindika ngozi, kodi ya mapato kama vile *PAYE* na kadhalika. Sasa ni wakati mwafaka tuchukue hatua hii kwani hata nchi ya Pakistani ambao ndiyo wanunuzi wa ngozi yetu, wamepiga marufuku kabisa uuzaji wa ngozi ghafi nje ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Sekta ya Maziwa. Taarifa ya uwezo wa viwanda na hali halisi ilivyo sasa hivi inayonesha kuwa hadi sasa kuna viwanda 35 vyenye uwezo wa kusindika zaidi ya lita 1,000 kwa siku kwa kila kimoja. Kati ya hivyo, ni viwanda 28 tu ambavyo vinazalisha hadi sasa na vingine saba ama vimefungwa au kusimamisha uzalishaji. Kuna baadhi ya viwanda vinatumia hadi zaidi ya asilimia 80 ya uwezo wake na vingine chini ya asilimia 16. Kwa vile kuna viwanda visivyozalisha kabisa, wastani wa matumizi ya uwezo wa kusindika ni asilimia 12 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa jumla wa viwanda vyote ni kusindika lita 428,500 kwa siku, lakini hali halisi ni kusindika lita 52,330 kwa siku. Hali hii inaonesha kuwa, juhudi kubwa zinahitajika ili kuwezesha Sekta ya Viwanda vya Maziwa kuwa na uwezo wa ushindani na kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayovikabili

viwanda vya maziwa ni mengi na yanahitaji uchunguzi wa kina katika kila kiwanda ili kutoa ushauri kwa kila kiwanda husika, lakini matatizo yaliyotajwa na viwanda vyote ni kama yafuatayo:-

- Ukosefu wa maziwa ya kutosha. Ingawa Tanzania inakadiriwa kuzalisha lita 1,400 milioni za maziwa kila mwaka, kiasi cha maziwa yanayopatikana kwa ajili ya kusindika ni kidogo sana. Hali hii inatokana na maziwa mengi kuzalishwa na wafugaji wa jadi, ambayo kiasi kikubwa kinatumika na wafugaji wenyewe, uzalishaji ni wa msimu na ukusanyaji ni mgumu. Wafugaji hawa ndiyo huzalisha asilimia 70 ya maziwa yote nchini.

- Upungufu wa maziwa ya kusindika ambao huwa zaidi wakati wa kiangazi unachangiwa na sababu nyingi ambazo ni gharama kubwa na ugumu wa kukusanya maziwa ya wafugaji waliosambaa maeneo ya mbali; ushindani na wachuuzi wadogo wadogo; faida ndogo kutokana na matumizi kidogo ya uwezo wa viwanda; na uzalishaji wa msimu ambapo maziwa mengi hupatikana msimu wa mvua na kidogo sana wakati wa kiangazi na hivyo kushindwa kutosheleza

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa viwanda vya maziwa vilivyopo vinapata maziwa ya kutosha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba, maziwa yanayozalishwa na wafugaji wadogo au wa asili yanauzwa kwenye vituo maalum vya kukusanyia maziwa na pia maziwa yasiuzwe kwa wanunuzi bila ya kuyasindika. Kufanya hivyo kutaondoa kwanza matatizo ambayo yanaweza kutokana na magonjwa ya kuambukizwa kati ya mifugo na binadamu *(zoonotic deseases).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia liwe ni jukumu la Halmashauri kulinda soko la maziwa yaliyosindikwa na kwa njia hiyo wafugaji wadogo na wale wa asili, maziwa yao yatakuwa na uhakika wa soko badala ya sasa ambapo wakati wa msimu wa mvua maziwa yanakosa soko na hivyo kumwagwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maziwa kuuzwa moja kwa moja na wafugaji wadogo na wakubwa ni upotevu wa mapato; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa, liwe ni jukumu la Halmashauri kutunga kanuni ndogo za kuhakikisha viwanda vya maziwa vinalindwa kwa kupata maziwa muda wote ili kiwanda kiweze kulipa kodi kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na matatizo ya kimfumo na sera, pia katika kundi hili kuna matatizo ya urasimu katika vyombo vya kudhibiti ubora kama *TBS*, kuwa na vyombo vingi vya udhibiti, wadau kutoshirikishwa katika maandalizi ya sera na migogoro kati ya wafugaji na wasindikaji na vyama vya wadau visivyo imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwepo uwajibikaji kwenye vyombo vya udhibiti na vyombo hivi madhumuni yake yawe ni kuwezesha na siyo kukwamisha. Inapendekezwa kuwa, shughuli zote za udhibiti wa Sekta ya Maziwa zifanywe na Bodi ya Maziwa, tofauti na sasa ambapo vyombo vingi hufanya hivyo. Aidha, Bodi ya Maziwa iliyoanzishwa kisheria, iwezeshwe kufunya shughuli zake kwa kupewa rasilimali zinazotakiwa tofauti na sasa ambapo Bodi ipo kwa jina tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wadau washirikishwe katika utayarishaji wa Sera zinazohusu Sekta ya Maziwa, kwani sasa wanaohusishwa ni wale wenye viwanda vya maziwa. Je, wafugaji wa asili wanahusishwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengine ni kama kipato kidogo cha Wananchi, wawekezaji kuwa na miradi mingi kwa pamoja, Sekta ya Maziwa kutokuwa na mvuto kwa wawekezaji, ukosefu wa vyombo vya mikopo ya muda mrefu na riba ndogo na kutokuwa na maeneo maalum, yenye miundombinu ya kutosha ya kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi Upinzani inaitaka pia Serikali itafute njia ya kuimarisha Vyama vya Kitaifa vya Wadau *(TAMPA, TAMPRODA)*, ili viwe kweli vya

Kitaifa na vyenye uwezo wa kushirkiana na Serikali kundeleza sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo ya 7 aya ya 7.2.3 ya KILIMO KWANZA inayosema kwamba; "Kuainisha na kuimarisha uwezo unaohitajika kwa kuendeleza Sekta ya Mifugo, kwa mwaka 2010 Serikali pamoja na *TPSF,* ilitakiwa kukarabati viwanda vyote vya maziwa vilivyopo nchini na kuanzisha vituo vya kukusanyia maziwa." Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge na wadau kwenye Sekta hii ya Maziwa utekelezaji wa nguzo hii ya KILIMO KWANZA imetimizwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano inaonesha ili Sekta ya Mifugo iweze kuleta tija tarajiwa, ilitakiwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ipewe shilingi bilioni 275.98 kama fedha za maendeleo. Kwa masikitiko makubwa, mwaka huu wa fedha Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 8.97.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwa nini imeshindwa kutekeleza matakwa ya Mpango wa Maendeleo ambao ulipitishwa na Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inamiliki maeneo makubwa ya maji ambapo rasilimali za uvuvi hupatikana kwa wingi. Maeneo hayo ni pamoja na Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Mabwawa (Nyumba ya Mungu, Mtera na mengine mengi ya asili), Mito (Rufiji, Ruvu, Kilombero na kadhalika), malambo na maeneo oevu ambayo yana fursa kubwa ya uvuvi hapa nchini. Aidha, kuna Bahari ya Hindi ambayo ina maeneo mawili ya Bahari ya Taifa *(Territory Sea)* na Ukanda wa Uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic Zone - EEZ).*

Sekta ya Uvuvi inatoa mchango mkubwa katika kuwapatia Wananchi ajira, lishe, kipato na kuiingizia nchi fedha za kigeni. Uvuvi nchini huendeshwa na wavuvi wadogo takriban 200,000 ambao huvua asilimia zaidi ya 90 ya samaki wote wanaovuliwa nchini. Zaidi ya Wananchi 4,000,000

hujishughulisha na kujikimu kutokana na shughuli zinazoendana na uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uharibifu uliopo katika uvuvi umesababisha kuwepo kwa upungufu mkubwa wa rasilimali ya uvuvi, hususan katika Ziwa Victoria, ambalo huongoza kwa upatikanaji wa samaki aina ya Sangara ambao wamepungua kutoka tani 676,000 mwaka 2006 hadi tani 331,000 mwaka 2009. Hali hii imetokana na sababu zifuatazo:-

- Ongezeko la kasi ya matumizi ya zana haramu pamoja na ongezeko la idadi ya wavuvi kutoka 92,529 mwaka 2000 hadi 105,016 mwaka 2008;

- Ongezeko la vyombo vya kuvulia samaki kutoka vyombo 30,171 (2000) hadi vyombo 52,174 (2008);

- Ongezeko kubwa la mahitaji ya samaki na mazao yake katika soko la samaki ndani na nje ya nchi na hivyo kuwa kichocheo kikubwa cha samaki wachanga kuvuliwa. Kwa upande wa Bahari ya Hindi, mathalani rasilimali ya kambamiti imepungua kiasi cha kusababisha uvuvi wake kwa meli kubwa kufungwa hadi sasa. Aidha, rasilimali ya Kambamiti *(Prawns)* imepungua kutoka tani 1,320 kwa mwaka 2003 hadi kufikia tani 205 mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo wa ongezeko la mahitaji ya samaki na mazao yake katika soko, wavuvi wamekuwa wakiilalamikia Serikali kuwa inakwamisha au kuwahujumu kwa uchomaji wa nyavu za wavuvi ambao hata hawaelewi ni kwa nini wanauziwa nyavu zisizostahili kwa mujibu wa Watendaji.

Ukweli ni kuwa, nyavu zote kustahili au kutostahili inategemea unavua samaki wa aina gani na nyavu hizo zinatumika namna gani; hivyo basi, kitendo cha kuchoma nyavu za wavuvi (zana za uvuvi) bila ya kuhakiki matumizi yake na bila ya kutoa nyavu (zana mbadala) ni hujuma kwa sekta hii ya uvuvi na wavuvi wenyewe. Kumekuwepo na tabia

ya kufunga ziwa au kusitisha shughuli za uvuvi kiholela, bila taarifa au sababu za kisayansi zinazotolewa kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa tabia hii yenye kujenga hisia ya chuki za Wananchi kwa Serikali yao ni Ziwa Basotu. Hili Ziwa limeingizwa kwenye mitego, chambo na chuki au ulipizaji visasi vya kisiasa tu. Kumewekupo na shinikizo la ulipazaji kisasi wa kisiasa kwa kufungiwa Ziwa mara kwa mara ili wataabike, wasipate kitoweo na kipato na kuvuruga mfumo wao wa maisha ya kila siku, lakini siyo ukweli wa hali halisi kuwa kuna uvuvi usiofaa.

Je, haya ndiyo maendeleo ya Sekta ya Uvuvi? Hivi jambo la kisayansi linaendeshwaje kisiasa? Nadhani haya siyo maendeleo tuliyotarajia kwa mujibu wa Ilani za CCM za mwaka 2005 - 2010 na 2010 - 2015 bali ni hujuma na upandikizwaji wa mbegu mbaya za chuki za kisiasa tu.

Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri awaeleze Wananchi wa Basotu kwanza ni nani mwenye mamlaka ya kusitisha uvuvi katika Ziwa na hatua zipi ambazo pia zinashirikisha wadau zinapaswa kufuatwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za ufugaji wa samaki hufanywa na wafugaji wadogo. Hata hivyo, ufugaji wa samaki lazima ushindane na shughuli zingine za vijijini kwa eneo la ardhi, maji, nguvu kazi na vyakula. Hali hii hupelekea umuhimu wa kutathmini gharama na faida ya ufugaji samaki na mchango wake kwa maisha ya wakazi wa vijijini kulingana na shughuli zao zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, ufugaji wa samaki hukabiliwa na matatizo na changamoto zingine kama ukosefu wa sera thabiti ya ufugaji samaki; mabadiliko katika sera za uchumi; ukosefu wa teknolojia bora; upungufu wa vifaranga bora; miundombinu duni ya usafiri; utafiti usiokidhi mahitaji; ukosefu wa takwimu za uzalishaji; na upungufu wa taarifa sahihi za utunzaji wa bwawa la samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na uwezo wa

kufanya shughuli kwa mafanikio, ni muhimu kuwa na takwimu ya utendaji na shughuli husika. Vivyo hivyo, ili kuendesha shughuli za ufugaji samaki kibiashara, mfugaji analazimika kuchukua na kutunza takwimu kwa hatua zote au shughuli yoyote anayoifanya ikiwemo ya kutunza matumizi na mapato ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Sekta ya Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ilitakiwa itengewe jumla ya shilingi bilioni 60.896 ili sekta nzima ya uvuvi iweze kuleta tija stahili. Pamoja na faida zingine ni kwamba, kama uwekezaji kwa mujibu wa mpango hadi 2015, makusanyo ya Serikali kwa mwaka katika sekta hii yalifanikiwa kukua kutoka shilingi bilioni 6.58 hadi shilingi bilioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni kwa nini Serikali imekinzana na Mpango wa Maendeleo uliopitishwa na Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwenendo wa Bajeti ya Wizara kwa miaka minne inayoonesha kuwa Bajeti ambayo imekuwa ikitolewa kwa Wizara hii imekuwa ikishuka, Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 zilitengwa shilingi bilioni 58.8, mwaka 2011/2012 zilitengwa shilingi bilioni 57.2, mwaka 2012/2013 zilitengwa shilingi bilioni 54.6 na kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa shilingi bilioni 47.18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa tafsiri ya kupungua huko kwamba ni fundisho kwa watendaji wa Wizara, kuangalia fursa za mapato ambazo zipo katika Wizara hiyo, zifanyiwe kazi na ziweze kuwekezwa kwa maendeleo ya sekta hizi mbili (Mifugo na Uvuvi); na kwamba, kutokana na ukweli uliopo wa fursa hizo, Wizara imelala na hata kusimamia sheria na kanuni zilizopo za kuhakisha mirabaha ya uvuvi inalipwa au imeshindwa na wajanja wanaovuna rasilimali yetu bila nguvu yoyote ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, inasema kwamba, Wizara hii kwa kipindi kirefu imekuwa kama nyumba isiyokuwa na msimamizi, kiasi kwamba, rasilimali za nchi hii zimekuwa zikigawiwa, zikivunwa na kutumiwa bila kufuatwa kwa sheria na kanuni. Mfano mmojawapo ni ugawaji wa mashamba ya Ranchi za Taifa na kilichofuata ni nchi kuingia kwenye migogoro mikubwa kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuonesha kuwa Serikali imeshindwa kuthamini Sekta ya Mifugo kwa ujumla, mwaka 1981, Mwasisi wa nchi hii, Marehemu Mwalimu J. K. Nyerere, akiwa Morogoro alisema: "Tumetenga kwa mfano, maeneo maalum kwa ajili ya mazao kama pamba, kahawa, tumbaku na katani, lakini hatujatenga maeneo kama hayo kwa ajili ya mifugo. Tumetenga maeneo maalum kwa ajili ya pundamilia (Hifadhi za Taifa), lakini wafugaji wananing'inia hewani tu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kama kungekuwa na umakini katika Serikali hii ya CCM ni dhahiri kuwa, makosa ambayo yalikuwa yanatendeka huko nyuma, ulikuwa ni muda mwafaka wa kurekebisha makosa katika Sekta hii ya Mifugo na hivyo yanapelekea wafugaji kuwa wahamiaji au watu wasiohitajika katika nchi yao kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Menyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni shukurani kwa wanachama na wapenzi wote wa CHADEMA nchi nzima na hasa Wilaya ya Hanang, kwa kushirikiana na mimi, kwa kazi zote tunazozifanya bega kwa bega kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru. Waheshimiwa Wabunge, bila kupoteza muda, ninaomba nimwite mchangiaji wetu wa kwanza, ambaye ni Mheshimiwa Charles Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, kama

muda wetu utatosha, lakini ninaomba hawa wawili angalau wapate nafasi.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa. Nimelazimika kurudi, nilikuwa kwenye majukumu mazito ya kitaifa, lakini na hili la Wizara ya Mifugo na Uvuvi linanihusu. Nisije nikafanana na mtu aliyelisha watoto wa kwale, watoto wa kuku wakafa njaa. Nimelazimika kurudi ili nizungumzie suala la mgogoro wa *NARCO* na Serikali kwa upande mmoja na Wananchi wangu wa Kata ya Lutoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze binafsi mimi nakula nyama. Napenda ng'ombe na ninafuga; ninafuga Dar es Salaam na ninafuga kijijini kwangu Ilogero. Sina uhasama na mtu anayefuga. Jitihada za ufugaji katika Ranchi ya *NARCO*, zilipelekea maafa ya unyama dhidi ya utu. Ninaishauri Serikali yangu na ndiyo maana ninasema sijui niseme namna gani; ninaishauri Serikali yangu, kiasi cha pesa kilichotengwa cha shilingi bilioni 47, kwa kazi niliyonayo hakitoshi. Mimi nina kazi kubwa, shughui za mifugo zimeleta matendo mabovu dhidi ya ubinadamu.

Nakwenda zaidi; katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri sijaona kitu. Mimi ninafikiria maridhiano, ninaishukuru Serikali, ninaishukuru Wizara na hasa hasa Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, wamekuwa mstari wa mbele kufuatilia ule mgogoro wa Lutoro wanautatua. Serikali na Wizara hii wako mstari wa mbele sina matatizo nao. Tatizo langu ni wale watekelezaji wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefanyika unyama. Waziri hakufanya unyama kule. Waziri hajambambika mtu kesi. Waliobambika kesi baada ya kumaliza mgogoro wenu huu inabidi mfanye maridhiano. Mfanye maridhiano kama watu wa South Africa. Katika Kata yangu ya Lutoro akionekana Polisi watu wanakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninakuja hapa mahususi kuomba pesa zaidi ziongezwe ili zielekezwe katika

kutatua migogoro hiyo ambayo Wananchi na Wabunge mnaisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mwakyusa, Mheshmiwa Waride, Mheshimiwa Dkt. Kamani, kwa kutaja baadhi, ni watu ambao walifika Kashenamboni katika Kata yangu ya Lutoro. Mheshimiwa Waride alilia na mimi nillia. Kwa hiyo, mtu yeyote anayezunguka nchi hii akisema Mheshimiwa Mwijage anachochea, hajui uchungu wa mwana. Niko Bungeni kwa sababu nilichaguliwa na Wananchi, *full stop*. Kwa hiyo, mtu anayeingilia mchezo huu, jitihada zangu kwa kubeba Ilani ya Chama ni kwamba, sisi tunatetea Wananchi na suala hili nimelipeleka juu mpaka ofisi ya juu kabisa na Mwenyekiti wa Chama changu alinihakikikishia, Naibu Waziri alikuwepo kwamba, maslahi ya Chama cha Mapinduzi ni Wananchi na siyo ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pesa ziongezwe, migogoro ya Lutoro iishe, migogoro iliyoko Misenyi iishe, tuanze ukurasa mpya. Zaidi ambacho ninakielekeza kwa Serikali na hasa Waziri wa Mambo ya Ndani, kuna haja ya maridhiano.

Mtoto wa Lutoro, ukimwambia Polisi anakuja hata angelikuwa ana miezi mitatu utamlaza kwenye umande na hawezi kulia. Kwa hiyo, Wananchi wamejenga hofu kwa Watendaji wa Serikali hasa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi ya Marekani, kuzungumza suala lililoko Mahakamani siyo tatizo, Tanzania ninasikia inazuiwa. Ndugu zangu mlioko ndani kwa kesi za kubambikizwa, mnakufa, mnateswa, lakini mateso yenu yatawakomboa ndugu zenu wa Lutoro na mimi niko nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza suala la Lutoro, ninaomba niishauri Serikali yangu kama ilivyozungumzwa katika bajeti zenu, mwombe pesa zaidi tuwekeze kwenye *Pasture Management.* Tuwahimize Wananchi wetu kuwa na *Pasture.* Sisi tunazo hifadhi nyingi, asilimia 28 ya nchi yetu ni Hifadhi, wakati umefika sasa wa

kupunguza Hifadhi na kutengeneza *Ranching Association* ili Wananchi wetu hao ambao mnasema wanatangatanga, hawatangitangi, wanatafuta malisho; mtengeneze *Ranching Association* ili tuwaweke. Ningelipenda Wananchi wapewe maeneo waweze kufuga katika maeneo ambayo wanaangaliwa.

Mheshimiwa Mwneyekiti, ninarudia, sitafuni maneno; nisingelipenda kulisha watoto wa kwale, wakati watoto wa kuku wanakufa. Wako ndugu zangu Wasukuma wamekuja kwangu, lakini wameburuzwa, wamepigwa risasi; lakini anapotokea mtu kutoka atokako kule nje ya nchi yangu, anapoguswa Polisi nywele zinawasimama na Viongozi wote wanaanza kusema Mwijage anachochea migogoro. Sichochei migogoro, ninataka kulisha watoto wa kuku wanenepe, mimi Msukuma ni ndugu yangu, kwanza, tutosheke sisi kabla ya kuwakaribisha wengine. Anayewakaribisha kama ana masilahi yake atajijua mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la samaki. Samaki katika Ziwa Victoria wamekuwa wana mahitaji makubwa. Kuna uvuvi kupita kiasi. Sisi watu wa Kerebe, Gospa, Makibo, Kinagi na Bumbile, maisha yetu ni samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza na Mheshimiwa Waziri na ndiyo maana ninamwombea pesa. Kwamba, Wananchi wale mwangalie namna ya kuwawezesha, muwape zana za kisasa na muwaelekeze namna ya kuvua kitaalam na ndiyo maana ninaomba pesa zaidi kwa ajili ya watu hawa. Ninaomba pesa kwa ajili ya Wizara hii ili waweze kupata pesa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majilio ya mahitaji makubwa ya samaki, yamepelekea Wananchi kwenda kufuga. Kwetu sisi tumekwenda mbele zaidi, Wizara inajua, Mheshimiwa Dkt. Charles anajua, J & B, Kituo cha Ufugaji Samaki cha Ruanda, kimeshakwenda mbele na ninaishukuru Serikali imewapeleka watu wangu, wapambanaji wangu Vietnam. Tunachoomba,

Taasisi za pesa ziende kasi, panapoonekana kwamba mtu anakopesheka, urasimu upungue.

Mheshimiwa Mwenyeiti, ninaomba niwaeleze kitu kimoja; kuna jambo huwa ninalisema kila siku la *allocation advantage.* Nchi za Magharibi mwa Tanzania hasa Congo, nchi ambazo zinajengwa sana, wanahitaji samaki. Huwezi kuamini, samaki wanapita kwenye makontena wakitoka katika nchi za Uajemi, wakitoka Mashariki ya Mbali, wanasafirishwa kwenda katika nchi za Congo ambako uchumi unakua kwa kasi. Sisi tunayo mito, hata nisipoitaja mnaijua; mito yetu sisi ikiandaliwa vizuri, tukapewa mitambo hiyo ya kisasa kama waliyoomba watu wa J & B, watu wote wakafuga, tutaondoa umaskini, tutapata lishe na tutaweza kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari, ninasimama hapa kuiomba Serikali angalieni, wanasema jungu kuu halikosi ukoko, siridhiki mimi; mipangilio ninaiunga mkono, hasa lile la kumaliza migogoro, lakini pesa shilingi bilioni 47 zilizotengwa, ninaomba chondechonde tuangalie. Unaweza ukawa wewe unashabikia kutafuta umeme katika nyumba yako, lakini wenzako Urutoro na wapi, wanateketea kwa mateso kwa sababu ya migogoro. Ninaomba pesa ziongezwe ili Wizara ya Mifugo waweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba zaidi, Wananchi wengi wako kwenye ufugaji. Wizara ya Mifugo na Uvuvi iwezeshwe, kusudi vyuo vyao vya Mifugo viweze kufundisha wanafunzi wa miaka miwili, wa mwaka mmoja na hata wa miezi mitatu. Wafundisheni wafugaji wetu waweze kujua ku-*handle* mambo haya. Itawezekana kwa kuwa na Vituo vidogo vidogo vya kuwawezesha Wananchi kwenda Kisasa. *Pasture Management* itafundishwa kwa vipindi vifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaomba niseme ninaishawishi Serikali yangu, Serikali Kuu, kwenye Fuko Kuu, mwongeze pesa kwenye Wizara hii, ili Wizara hii iende kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaendelea na majukumu yenu mliyonipa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mwijage, ninafikiri kule Lutoro wamekusikia. Sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa niwe mchangiaji wa mwisho mchana huu. Kwanza, naipongeza safu ya Wizara, mmekaa vizuri mmetulia, tatizo lenu hamna Bajeti ya kutosha kutekeleza majukumu. *(Makofi)*

Mna Sera ya Mifugo nzuri ya mwaka 2006. Mna Programu ya Kuendeleza Mifugo ya 2001, imekaa vizuri kabisa na Programu ya Kuendeleza Uvuvi. Mnafanya kazi nzuri, endeleeni na mimi niungane mkono na Wabunge wenzangu, akiwemo Mheshimiwa Charles Mwijage, aliyemaliza kuongea sasa, Wizara iongezewe fedha. Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo, imeomba Serikali iongeze shilingi bilioni 40; mimi ninaunga mkono hilo lifanyike. *(Makofi)*

Kwa sababu unapoweka shilingi bilioni nne kwa sekta kama hii, kwa ajili ya Maendeleo ya Sekta, shilingi bilioni nne fedha za ndani, huitendei haki Sekta hii. Sekta muhimu ambayo ni mboga na kitoweo. Nchi yetu ni ya pili katika Afrika kwa wingi wa mifugo, baada ya Sudan kugawanyika tulikuwa wa tatu, sasa tumekuwa wa pili, baada ya Ethiopia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilikuwa imeomba shilingi bilioni 163 wamepewa 47. Ninarudia, fedha hizi chonde chonde ziongezwe. La pili, Wananchi wa kutoka Jimbo la Magu, Wafugaji ambao sasa wanaitwa Wachungaji, wameenea maeneo mengi na Mheshimiwa Mwijage amenisaidia kusema katika Jimbo lake la Muleba Kaskazini wapo Wasukuma; Wasukuma wale wengi wanatoka Mwanza, wanatoka Magu. Mkoa wa Mwanza ni wa pili kwa idadi kubwa ya watu katika nchi hii baada ya Dar es Salaam;

kwa hiyo, hakuna mahali pa kulisha mifugo, hakuna mahali pa kuchungia na ndiyo maana sasa inabidi waende mahali pengine wanaitwa wahamiaji; na hawako Kagera tu; wapo Mpanda, wapo Morogoro, wapo Kigoma, wapo Lindi na sehemu mbalimbali. Wengine walikwenda mpaka Ihefu na wamepoteza mali nyingi wakati wanahama kwenda Lindi, mpaka Zambia wengine wanajaribu kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nipendekeze; hatuwezi kukaa tunalialia kama vile sisi ni maskini. Tanzania siyo maskini hata kidogo. Tanzania eneo lake, ujumlishe Kenya, ujumlishe Uganda, ujumlishe Rwanda, ujumlishe Burundi, ujumlishe Comoro, ujumlishe Shelisheli, zote. *(Makofi)*

Tunalo eneo kubwa la kutosha, kufanya mambo yetu na kupanga mambo yetu vizuri. Tumefanya uamuzi mzuri, lakini siyo wa busara sana; asilimia 25 ya eneo letu tumeweka Hifadhi za Taifa ambazo ziko 13. Mapori ya Akiba ambayo yako 29 na maeneo yaliyodhibitiwa *(Controlled and Protected Areas 40).* Jumla haya yote yanakula asilimia 25 ya eneo letu. Asilimia 25 unaweka kwa ajili ya wanyamapori, lakini usawa wa wanyama uko wapi; unapendelea wanyama wa porini, hawa wanyama wanaofugwa na binadamu huwapi stahili yao, hiyo siyo sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lililotengwa kwa ajili ya Hifadhi, ni sawa sawa linakaribia na eneo na Uganda yote. Uganda nzima imetengwa kwa ajili ya Hifadhi ya Wanyamapori; hiyo siyo sawa sawa. *(Makofi)*

Ninaomba hili eneo lililohifadhiwa limegwe asilimia 25, libaki asilimia 75 ili asilimia 25 ambayo ni kilometa za mraba 60,000, ambayo ni karibia hekta milioni sita, wagagiwe wafugaji. Lengo la kutenga haya mapori lilikuwa ni zuri na sipingani na uhifadhi, naomba nieleweke. Unapokuwa una matatizo ya idadi ya watu, migogoro ya wafugaji na wakulima na Serikali, huwezi kuendelea kushikilia eneo hili kwa Hifadhi ya Wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuvunje angalau Hifadhi mbili. Ninapendekeza kwa Serikali, iangalie Hifadhi mbili au tatu zivunjwe tubaki na Hifadhi kumi ama tumege maeneo katika Hifadhi zetu ili turuhusu wafugaji. Kule Serengeti yatafutwe maeneo ili wapewe wakulima. Kule *Maswa Game Reserve* nako yatafutwe maeneo wapewe wakulima na kwenye maeneo mengine kwenye Ranchi zetu zote, kwenye Hifadhi zetu zote, hili lifanyike, asilimia 25 na eneo hili likitengwa asilimia 25 ni sawa sawa na Mikoa ya Dodoma na Mkoa wa Kilimanjaro kwa pamoja. Kwa hiyo, tuwatengee wafugaji wa Mkoa wa Dodoma, eneo linalolingana na Mkoa wa Dodoma, ujumlishe na Mkoa wa Kilimanjaro ili tuwatengenezee utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa jinsi watu wanavyohangaika. Bangladesh, nimesoma kule mwaka mmoja; ina eneo asilimia 16 ya eneo la Tanzania. Asilimia 16 nchi hiyo ya Bangladesh. Tanzania, idadi ya watu ni asilimia 28 peke yake, lakini wamejitosheleza kwa chakula na umaskini umepungua kwa asilimia 25 toka miaka ya 90. Wana shida na wamejibana. Tusione tu kama sisi haya matatizo hayatugusi. Migogoro hii lazima majibu yake tuyapate na ninapendekeza hilo lifanyike. Tuweke vichwa vyetu pamoja, siyo matumbo yetu pamoja, tuthubutu, tufanye maamuzi magumu. *(Makofi)*

Tuangalie maeneo ambayo tutaongeza ili wakafundishwe kule kufuga kisasa na kufanya kama wanavyofanya nchi nyingine. Wote hapa tunatembea, tunafanya ziara kwenda Botswana, tunakwenda Argentina, kote ambako wameendelea, tunaona jinsi wanavyofanya; kwa nini sisi hatufanyi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba, Serikali itasikia kilio cha wafugaji na kilichotokea Ifakara kwa wafugaji, kwenye lile Bonde ambako tunahifadhi mnyama anayeitwa Sheshe, lakini watu wamepata maumivu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine tuyafanye

lakini tuwe na moyo wa kibinadamu. Ninashukuru angalau baadhi ya wakulima wamerudishiwa mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaomba nikushukuru sana. Ninaamini Serikali itasikia kilio cha Wabunge, kwamba Bajeti ya Wizara hii iongezwe ili wakachape kazi na kuleta maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Limbu.

Waheshimiwa Wabunge, uwiano wa kuchangia leo ni Wabunge 15 ambao wanatoka Kambi ya Chama Tawala, Wabunge watatu kutoka CHADEMA na Wabunge wawili kutoka *CUF.* Ninawashukuru sana Ma-*Chieef Whip;* Mheshimiwa Halima Mdee, ameshanipa orodha na utaratibu wa kuchangia kwa Wabunge wa CHADEMA; na *Chief Whip* wa Chama cha *CUF,* naye ameshanipa utaratibu kutoka Chama cha *CUF*; na Chama cha Mapinduzi pia orodha tayari iko hapa mezani. Kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote, wawasiliane na Ma-*Chief Whip* wao, wajue utaratibu wa kwao wa kuchangia leo.

Niwataje wale watakaoanza mara tutakapoingia hapa saa 11.00 jioni. Tutamsikiliza Mbunge wa tatu wa Kambi ya Chama Tawala, Mheshimiwa Lekule Laizer, halafu tutampa nafasi Mbunge wa CHADEMA, Mheshimiwa Shibuda na baadaye tutaendelea kama nilivyosema, uwiano wote wa vyama kadiri ya Ma-*Whip* walivyowasilisha majina hapa Mezani, tuweze kukamilisha uchangiaji wetu ndani ya Bunge kwa siku hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema utaratibu huo, ninaomba nisitishe shughuli hizi za Bunge na tutaonana tena ndani ya Ukumbi wa Bunge saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee na shughuli za leo na Mkutano wetu ni wa Kumi na Moja, Kikao cha Thelathini na Tisa na Wizara iliyo mbele yetu ni Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu kama ilivyotamkwa na Katibu na kama nilivyosema majadiliano yanaendelea. Wakati nasitisha kikao saa saba mchana nilisema tutakaporejea tena Bungeni jioni hii, msemaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Lekule Laizer atafuatiwa na Mheshimiwa Magalle Shibuda. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Laizer na Mheshimiwa Shibuda ajiandae. Mheshimiwa Laizer!

**MHE. MICHAEL L. LEKULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru sana Serikali kwa kuona kwamba mwaka 2009 mifugo ilikufa sana katika Majimbo yetu katika Wilaya ya Longido, Ngorongoro na Monduli na wakatupa mifugo kwa ajili ya kifuta machozi. Nawashukuru sana kwani hali ilikuwa mbaya sana, kulikuwa na watu ambao hawakubakiwa na ng'ombe hata mmoja, lakini Waswahili wao wakimwona Mmasai wanadhani kwamba, kila Mmasai ana ng'ombe lakini wakati huo hawakuwa na ng'ombe kabisa.

Kwa hiyo, walipaswa kupewa ng'ombe kama walivyopewa na Serikali. Namshukuru sana Rais kwa kuona hilo na kutupa mifugo na mifugo bado inaendelea kugawanywa kulingana na fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia bajeti ya Wizara hii, Wizara hii ndiyo wafugaji wote Tanzania wanaitegemea, na nadhani wafugaji ni wengi kweli, nadhani kwa sensa hii, sikujua wafugaji watakuwa wangapi, lakini nadhani wako zaidi ya 30% na wanategemea bajeti hii, lakini

Wizara hii imepewa fedha kidogo sana na inapunguzwa kila mwaka. Kila bajeti wanapunguza na wanapopunguza ndiyo wanadidimiza kabisa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo tulitegemea watuchimbie mabwawa, miaka yote iliyopita hatuna mabwawa yaliyochimbwa kutokana na ufinyu wa bajeti. Wizara hii ndiyo tulitegemea itupatie majosho kwa vijiji ambavyo havina majosho, lakini bado kila siku ni kilio. Wizara hii ndiyo tunategemea itupatie madawa, kama alivyosema Waziri katika bajeti yake *foot and mouth disease, ECF* hayo ni magonjwa sugu ambayo yanamaliza mifugo na kufanya wafugaji kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa kwa sasa ya *ECF* dozi ya ndama mmoja ni sh. 8,000/= na mkubwa ni sh. 12,000/=, sasa kama ni wafugaji ndiyo wananunua na kutafuta madawa haya wengine wanashindwa kuchanja. Kwa hiyo, naona hali hii, sijui kwa nini Wizara imeundwa ambayo ina jina la mifugo, lakini hakuna huduma ya mifugo. Hilo kwa kweli ni jambo la mshangao, nataka Serikali iangalie kwa bajeti hii na hatukubali fedha kidogo kama hizi, tunataka fedha za kutosha kwa ajili ya hayo niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu minada. Wilaya yangu iko mpakani nadhani nategemea katika idadi ya ng'ombe waliouzwa ambao Waziri alitaja kwenye bajeti yake ng'ombe wa Longido hawapo na sisi tunauza ng'ombe, lakini hatuuzi Tanzania tunauza Kenya na ng'ombe wa Longido ndiyo ng'ombe bora Tanzania lakini hatuna masoko wala hatuna viwanda kuanzia Tarime, Ngorongoro, Longido na hata Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe wote wanauzwa Kenya na kwa sababu hakuna masoko ya kutosheleza mifugo, tunaomba Serikali hii na narudia kila bajeti kuomba fedha kwa ajili ya kujenga soko mpakani kwa sababu wenzetu wanafaidi sana mapato ya mifugo kutoka maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya hawana ng'ombe bali wapo Tanzania, lakini wanajivunia kwamba wao ndiyo wanauza nyama nyingi nchi za nje, wao ndiyo wanauza ngozi lakini ni za ng'ombe wa Tanzania na nyama ni ng'ombe wa Tanzania, lakini pia wanarudisha nyama za ng'ombe wa Tanzania kuleta Dar es Salaam. Napenda Serikali isikilize kilio chetu kwa sababu kila siku tunalia kwamba hali ni mbaya. Kwa wiki ng'ombe wanaouzwa Bisi ni 3,000 kutoka Tanzania, sasa utapiga hesabu kwa mwaka watakuwa wameuza ng'ombe wangapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hali ni mbaya, pamoja na soko la ngozi, ngozi zinakwenda huko huko. Napenda Serikali iangalie sasa hali hii kwa sababu ni mbaya, kule ndiyo wanapata ruzuku na kodi ya mifugo na Tanzania hawapati kodi ya mifugo kwa ajili ya ng'ombe wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni migogoro ya wakulima na wafugaji. Kwanza nawapongeza wafugaji na wakulima wa Wilaya yangu ya Longido kwa sababu wao hawana mgogoro, pamoja na kwamba wapo wakulima na wafugaji, lakini hawapigani. Nawashukuru sana na hawa wafugaji na wakulima waige mfano wa maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro uliopo huku ni unyanyasaji wa wafugaji kuvamiwa katika maeneo yao, popote pale ambapo wafugaji wapo, wakulima wanakwenda na kuweka maboma na kuanza kuwavamia. Kwa hiyo, naomba hali hiyo iangaliwe, pamoja na masuala ya maeneo ya wanyamapori. Maeneo ya wanyamapori yaangaliwe kwa sababu eneo lote la wanyamapori katika Longido, Ngorongoro na Loliondo ni eneo la vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 hakuna *game control area* itakayokuwa ndani ya vijiji, lakini bado wanang'ang'aniza. Naomba ionekane kwamba, hayo maeneo ni maeneo ya vijiji na ni eneo la malisho ya vijiji. Hatuchukii wanyama wakiwa ndani ya maeneo hayo ya malisho, lakini lisije likaonekana kwamba ni eneo la wanyamapori na siyo eneo la wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kusema ni kwamba, Serikali iangalie kuboresha mashamba ya *NARCO*. Serikali iipe *NARCO* fedha kwa ajili ya kuboresha mashamba hayo ili Tanzania ianze nayo kuuza nyama nje. Tuna mashamba makubwa tumeanza sasa kuyabinafsisha, ni afadhali tuanze kuyafufua kuliko kuyabinafsisha kwa sababu bado Serikali ina uwezo wa kusimamia na Tanzania kuwa na soko la nyama katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema kwamba, kuna mgogoro mkubwa wa wakulima na wafugaji. Ukiangalia katika maeneo ya wafugaji yanavamiwa kila siku, ukienda Kiteto wakulima ambao hawapo katika maeneo yale wametoka Dar es Salaam na kila mahali na kwenda kwenye maeneo ya wafugaji au malisho na kwenda kufungua mashamba makubwa na bado inasemekana eti wenye haki ni wale wakulima walioacha maeneo yao na kuja kufungua mashamba. Bado hilo ni tatizo na ndivyo ilivyo katika maeneo yote. Naomba Serikali imalize mgogoro wa wafugaji na wakulima kwa sababu inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Laizer, lakini kabla sijamwita Mheshimiwa Shibuda ningeomba wahudumu wa Ukumbi wa Bunge mahali popote walipo, warejee ndani ya ukumbi haraka kwani hatuna mtu wa kutuhudumia humu ndani. Kwa hiyo, naomba sana wahudumu wetu wa Ukumbi wa Bunge mahali popote walipo, nadhani wananisikia warejee ndani ya ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Shibuda!

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia mawazo katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana naomba kuwasilisha mawazo na maono ya wafugaji ambao wako katika hali ngumu na ya matatizo makubwa sana baada ya kuwa wafugaji wengi wanauawa na mifugo inauawa, dhuluma zilizopo, rushwa iliyopo na yote haya hayana mahali pa kimbilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuihimiza Wizara hii na napenda kuwapa tu chemsha bongo ya kwamba, bila ninyi muelewe wazi ya kwamba maslahi ya wafugaj hayana mtetezi na hayana msemaji. Kwa hiyo, naomba Serikali pia itambue ya kwamba, mwisho wa ubaya wowote wa dhuluma ambao unatendwa na watumishi ni aibu kwa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, mwisho wa ubaya wowote unaofanywa na watumishi wa Serikali ni aibu na itarejea kwenye Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, naomba Chama cha Mapinduzi ambacho ndiyo Chama Tawala mwamke na mzinduke, muwe macho na muwe masikio na muwe midomo ya sauti ya wokovu na wokovu kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina deni kubwa sana na napenda kupongeza juhudi za Bunge hili. Napongeza Bunge kwa juhudi zake za kuandaa Kamati ya kwenda kufuatilia matatizo ya gesi Mtwara pamoja na matatizo yanayowakabili wananchi wote wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, naomba, mtazamo huo huo ambao umetumika na ukafikia kufanyiwa uamuzi kwamba tukatazame matatizo, vifo na mauaji yaliyotokea kule, vivyo hivyo napenda kutambulisha Bunge hili na kuomba umwambie Mheshimwa Spika kwamba na sisi wafugaji tunahitaji Kamati iende ikachunguze mauaji ya wafugaji yanayotendwa na Askari wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo tunataka tutambue mauaji ya mifugo yetu, rushwa na dhuluma ambazo zinatendeka kule. Vivyo hivyo, naomba kueleza

kwamba, damu ya wafugaji iliyomwagika katika Mikoa mbalimbali ni zaidi ya wananchi wengi ambao wamepata madhara Rukwa pamoja na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kusisitiza kwamba, Kamati ya Bunge ambayo imekwenda Mtwara, basi na mfumo huohuo ufanyike kuwa ni sauti ya ukombozi na Bunge lisitafsirike kwamba lina tabia za ubaguzi kwamba kuna maeneo bora zaidi ya kwenda kuchunguzwa na kuna maeneo bora zaidi ya kwenda kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wanalia na naomba ieleweke wazi kwamba, wafugaji ni kabila kubwa sana, ambao ni Wasukuma. Sasa upole wa Wasukuma usichukuliwe kwamba ni malighafi ya uhondo wa viongozi wa kisiasa pamoja na Serikali. Naomba kusema kwamba, upole wetu utambuliwe na upewe heshima ya ustaarabu, lakini naomba kusema kwamba mdai chake kwa mdaiwa huambiwa kwamba ni mtu mbaya. Sisi itafikia pahali tutakachodai mwaka 2015 asiyejua maana haambiwi maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo uliweke na wewe ni Mjumbe wa Kamati Kuu, naomba salamu hizi wapelekee pia na Kamati kuu. Ukimya wa CCM, mifugo inauawa, wafugaji wanauawa, dhuluma na rushwa, hakuna kikosikazi kinachokwenda kutafsiri na kuangalia matatizo ya wafugaji, hili ni tatizo ambalo linaleta taarifa kwamba, kuna ubaguzi na matabaka ya kuhudumia matatizo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la gesi Mtwara, viwanda vinamiminika kwenda kule, lakini sisi wafugaji Viwanda vya Kusindika Nyama hakuna, Viwanda vya Maziwa hakuna, ukiangalia Viwanda vya Ngozi vilibinafsishwa, hivi mnataka Wasukuma na sisi tufanye nini? Naomba majibu toka kwa Mheshimiwa Waziri na naomba ushauri wa Bunge uzingatie masuala haya. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbusha

historia ya Tanganyika, bila wafugaji kuunga mkono kura za maoni za kudai uhuru wa Tanganyika wakulima na wafugaji, Gavana asingeruhusu na asingemwambia Watanganyika tupo tayari kujitawala. Lakini baada ya kujitawala wafugaji leo tunaambiwa ni wafugaji haramuna wahamiaji haramu, je na wale wafanyabiashara waliotoka mikoa asilia ya kwao wakaenda mikoa mingine na wenyewe ni wafanyabiashara wahamiaji haramu? Je, kwa nini nchi hii kama mnaona ardhi ni ndogo, wakimbizi mnawapa ardhi wakati wafugaji hamuwapi ardhi yao? Naomba suala hilo mlitazame na Serikali mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwaka 1978, wendawazimu wa Iddi Amini ulipomega eneo la Kagera, wafugaji walitoa kitoweo kwa majeshi yetu yote, hapo wakaambiwa ni wazalendo na waaminifu. Baada ya vita leo mnawaambia wafugaji ni haramu, wahamiaji haramu, Wakuu wa Mikoa wanawatesa na Ma-*DC* wanawatesa, tuliondoa ukaburu, tuliondoa ubeberu na ukoloni, huu sasa ni ubeberu na ukoloni mamboleo wa Kiafrika, lakini CCM imekaa kimya, naomba mje mtueleze mwaka 2015. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba kusema hayo kwa sababu nina masikitiko makubwa sana. Wakati wa Baba wa Taifa alizungumza na Marehemu Bomani na Hayati Mnanka, akawaambia waambieni wafugaji na Wasukuma wote na wakulima wote muunge mkono kura ya maoni. Gavana akasema kweli sasa mnadai uhuru, mmeungwa na Kanda ya Ziwa, lakini leo heshima ya wafugaji iko wapi? Leo heshima hata ya wakulima wafugaji na yenyewe iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiko la dhuluma ni Wizara ya Maliasili. Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu, Wizara ya Maliasili ndiyo dhulumati wakubwa kupitia kikosikazi cha wanyamapori. Kikosi cha Wanyamapori wanadhulumu, wanaua ndiyo kitengo cha rushwa. Wizara ya Mifugo na yenyewe mmekaa kimya, hivi ukimya huu tuuelewe vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwende huko

mkazungumze na hao watu, kama kuna sheria hatarishi ambazo zimevamia maeneo ya wakulima na wafugaji, wakati umefika Wizara ya Wafugaji, hakikisheni viongozi wa Wizara hii mnakwenda kudai sheria ambazo ni hatarisho ambazo haziboreshi utulivu wa fikra za wafugaji na wakulima, tunaomba tuelewe kwamba sasa tunatengewa maeneo ya hifadhi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa wanyamapori wanapozaliana mnasema ni kuongezeka kwa uchumi, lakini mifugo ikiongezeka mnasema ni uharibifu wa mazingira, kwa nini viwanda vinapoongeza uzalishaji mnavipongeza, lakini mifugo ikiongezeka tusipongezane? Kwa kweli nasikitika sana na kama mnaona kwamba wanyamapori wanaendelea kuzaliana wataleta fujo, basi anzisheni uzazi wa mpango kwa wanyamapori. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba viwanda ambavyo vitakwenda sambamba na mahitaji ya mifugo zaidi ya milioni 20 na mbuzi zaidi ya milioni 15. Serikali imeserereka, haisemi ni nini wanafanya kuhusiana na kwenda sambamba, lakini ajira kwenye Viwanda vya Kusindika Nyama ingekuwa ni kubwa sana na tungepunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji Tanzania ni yatima na wanaishi maisha ya ghadhabu kwa sababu hawana mtu wa kuwasaidia. Leo mtambo wa kuzalisha fitina na hila hizi ni Wizara ya Maliasili. Wizara ya Maliasili wanazungumza kila siku kwamba sheria, sheria, sasa kama sheria haina uhai kwa maslahi ya utulivu wa Watanzania ni sheria gani hiyo? Tulikataa ukaburu na ubeberu, lakini leo mnaurudisha kinyumenyume na kusema kwamba, wafugaji ni wavamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, mporomoko wa viwanda uliotendeka Tanzania na kubinafsishwa, kwa kweli ni janga kwa maslahi ya Watanzania wote. Naomba kusema kwamba, viwanda viongezwe haraka sana na viende sawasawa, wanyamapori

kuongezeka ni neema, lakini mifugo mnailaani, kwa hiyo naomba na wafugaji pia mhakikishe kwamba, wanapewa neema ya uhuru wa Tanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukidadisi maisha ya wafugaji utakuta kwamba ni kamali ya rushwa, hakuna kikosikazi cha kuwasikiliza, hakuna sikio sikivu, Wizara hii na yenyewe siyo sikio sikivu, kwa hiyo wafugaji wanaishi maisha taabani sana. Nawaomba wafugaji wote mkae macho, kura zenu ndiyo ukombozi wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya Wizara hii najua imedumaa, imedorora, naomba Wizara hii sasa muamke na mhakikishe kwamba, mnakuwa watu ambao mnahakikisha utiifu bila shurti wala rushwa unaondoka kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo wa moto ni chehe, cheche za Mtwara ni cheche zinazowaka hovyo hovyo, lakini napenda kuwaambia cheche za wafugaji ni za kimya kimya. Amkeni, zindukeni, la sivyo majuto ni mjukuu. Hitilafu ya kukosekana imani na amani kwa wafugaji inasababishwa na Serikali. Dhahama ya Serikali mjue ndiyo mchwa unaoitafuna CCM, wala msigombane na Vyama vya Upinzani, ninyi ndiyo mnaozalisha *agenda* kwa sababu ya uwajibikaji wenu ambao hamtaki kuwa sikio la wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, CCM na Serikali yake hivi sasa mmepokonya haki za wafugaji. *TANU* ilikuwa tulizo la wafugaji, lakini leo hatuna utulivu. *TANU* ilikuwa ngao na usalama wa wafugaji, leo hakuna chama ambacho ni ngao na usalama wa wafugaji. Nawaomba, ukombozi dhidi ya wafugaji na mtambue kwamba nyie wafugaji ndiyo ngome kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nasema kwamba, CCM na Serikali yake kaeni... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili. Tunakushukuru Mheshimiwa Shibuda kwa mchango wako, ingawa leo umetunyima raha yetu Wabunge ya nahau za Kiswahili, lakini tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea na narudi tena kwenye Kambi ya Chama Tawala. Nitamwita Mheshimiwa Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Abuu Jumaa na atafuatiwa na Mheshimiwa Ole – Telele.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote sitaunga mkono hoja hii mpaka pale tutakapokuwa tumeongezewa zile fedha zilizoombwa na Kamati, shilingi bilioni 40. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana kwani inahudumia wananchi ambao ni wengi kwa maana ya wakulima na wafugaji. Bajeti ya Serikali kwa Wizara hii imekuwa ikishuka mara kwa mara. Asilimia kubwa ya bajeti hii ni ya mishahara tu ya wafanyakazi, fedha za maendeleo hakuna. Wizara nzima imetengewa shilingi bilioni nane tu, sijui Wizara hii inafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kama kweli tumedhamiria kutatua matatizo ya wafugaji na wavuvi, ni vyema basi, ikatenga fedha tulizoomba ambazo Kamati imependekeza ili tuweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa sana kwenye sekta hii; tatizo la kwanza, wakulima au wafugaji walio wengi wanahamahama kwa sababu hawajapata huduma iliyo nzuri katika maeneo yao. Hatuwezi kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji kama Serikali haijawajengea mabwawa, majosho ya mifugo na kutenga maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali ikaangalia upya, kuna maeneo mengi sana ambayo imeyaacha kwa ajili ya matumizi, *either* ni hifadhi za misitu au ni hifadhi za Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa wakaangalia umuhimu wa wananchi ambao wanatangatanga katika nchi yao na wanaonekana kama wakimbizi kwa sababu hakujawa na miundombinu ya kuwasaidia wafugaji hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu kuna wafugaji wengi sana ambao wametoka Mikoa ya Shinyanga na Mwanza. Sababu kubwa ni kwamba, kule hakuna miundombinu. Kama wangekuwa wamejengewa mabwawa, majosho na huduma nyingine kama vile maeneo ya kulishia mifugo, hawa wananchi wa kutoka mikoa hiyo wasingefika kwenye maeneo ya kwetu. Sasa ni lazima Serikali ijipange kuhakikisha inaandaa miundombinu ili kuwasaidia wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu inayohitajika katika maeneo ya wafugaji. Wafugaji wajengewe Viwanda vya Kusindika Nyama. Kama viwanda vitajengwa katika maeneo hayo, ni vigumu sana kuwaona wafugaji wanatangatanga na kupeleka mifugo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kama kutakuwa na ujengaji wa Viwanda vya Ngozi tutakuwa tumezalisha ajira nyingi ambazo zitatoka kwenye sekta hii. Niiombe Serikali watilie mkazo na umuhimu katika maeneo haya ili kuweza kuondoa migogoro isiyokuwa na ulazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi. Sekta hii ni eneo ambalo halijafanyiwa kazi na Serikali, kwani imeshindwa kuwekeza kwenye sekta hii ambayo ingekuza uchumi wa Taifa hili. Tuna maeneo makubwa sana katika nchi hii; mwambao wa bahari ambao ni mrefu kuzidi maeneo mengine katika nchi za Afrika hasa katika Bahari hii ya Hindi, ukianzia maeneo ya Mtwara mpaka kule Tanga. Eneo hili ni la uvuvi ambalo kama lingewekezwa lingeweza kutoa ajira nyingi kwa Watanzania, lakini kwa bahati mbaya hakuna kitu ambacho kimewekezwa katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia meli nyingi za nje zikija kuvua katika ukanda wa bahari yetu kama vile wako nyumbani kwao. Inasikitisha sana na nitaomba maelezo ya Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze. Wenzetu wa nchi ya Msumbiji walipokamata meli iliyokuwa inaiba katika mwambao wa Bahari ya Hindi ambapo na sisi tulikamata meli, ile meli wenzetu waliitumia vizuri. Mara walipoikamata waliitaifisha na ikaanza kufanya doria kwa ajili ya kusimamia wale wavuvi haramu katika maeneo husika ya nchi ya Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ile meli tuliichukua na kuiweka kama kielelezo cha Mahakama. Leo hii ile meli haipo na iliishazama. Tunaomba maelezo ya Serikali ni kwa nini tusingeitumia ile meli ikafanya shughuli za doria kwa ajili ya kutafuta wale ambao wanafanya uharibifu kwenye mwambao wa bahari yetu ya Hindi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la uvuvi liko Ziwa Victoria. Eneo hili limekuwa likivuliwa samaki na wanaonufaika sana ni nchi za Uganda na Kenya. Ukiangalia katika ramani mmiliki wa Ziwa Victoria kwa asilimia kubwa ni nchi yetu ya Tanzania. Bahati mbaya hakuna kitu chochote ambacho tumekiwekeza kwa ajili ya kusimamia uvuvi wa maeneo haya. Hatuna mafuta ya kufanya doria ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake Waganda na Wakenya, wanavua kwa wingi katika maeneo ya kwetu na hata wale wafanyakazi ambao wapo na wangeweza wakalinda zile rasilimali tulizonazo wanashindwa kwa sababu hawana vitendea kazi. Naomba Serikali iangalie na ihakikishe inawatengea Wizara fedha zile zilizoombwa, wapewe ili waweze kwenda kufanya kazi na hatimaye tutaona matunda ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika hakuna uwekezaji wa aina yoyote uliofanywa na Serikali. Wenzetu wa Zambia wana

eneo dogo sana la Ziwa Tanganyika, lakini samaki wote wanaovuliwa upande wa Tanzania wanakwenda kuuzwa Zambia kwa sababu wenzetu wana miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona kila mahali ambapo sisi tuna eneo la ziwa kama vile Tanganyika na Nyasa, wanaonufaika ni nchi jirani ambazo tumepakana nazo. Sisi Watanzania tuna ugonjwa gani ambao hauna tiba? Ni vizuri tukaangalia na tukaona jinsi ya kuwasaidia wananchi wa maeneo haya wanaoishi kando kando na maziwa haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshaji. Hakuna maeneo ambayo wamewasaidia wavuvi wadogo wadogo. Katika eneo hili, ili tuweze kuwasaidia wananchi, ni lazima Serikali iandae mpango kazi maalum wa kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo ambao wakisaidiwa watatoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivyo, tutakuwa tukizishuhudia kwa macho rasilimali zote zikibebwa na wajanja wachache ambao wanatumia fursa tulizonazo. Ni lazima tupeleke viwanda kwenye maeneo ya Ziwa Tanganyika ili kuhakikisha mazao yanayozalishwa katika maeneo hayo yanaweza kusindikwa na hatimaye kuuzwa nje na kusaidia jamii zinazozunguka katika maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Nyasa ni Ziwa ambalo lina samaki wengi, lakini wanaonufaika ni Wamalawi na ndiyo maana Serikali ya Malawi inathubutu kusema lile ziwa lote ni mali yao kwa sababu Serikali ya Tanzania haijaweka mpango mzuri wa kuwasaidia wavuvi katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali na bahati mbaya Waziri wa Fedha hatujamwona leo hapa, angekuja na tamko la kuisaidia Wizara hii ili iweze kufanya kazi. Wizara hii wapatiwe fedha ambazo zitawasaidia kutekeleza majukumu yao, vinginevyo kila siku tutakuwa tunapiga kelele isiyokuwa na faida ya aina yoyote kwa sababu bajeti

inakuwa ndogo. Hii ni Wizara yenye migogoro mingi, lakini bahati mbaya ndiyo Wizara ambayo bajeti yake inashuka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono pale nitakapokuwa nimepata maelezo thabiti ya ongezeko.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalam wake wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya na jitihada ambazo wanaendeleza katika Wizara hii ili kuhakikisha sekta hizi za mifugo na uvuvi zinaendelea. Kwa kweli, jitihada wanazo, lakini tatizo kubwa ni fedha. Kila siku tunazungumzia masuala ya fedha hapa, mmeainisha mambo mengi mazuri, lakini tatizo kubwa ni fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii tu kuiomba Serikali iisaidie Wizara hii ili iweze kukidhi mahitaji ya wananchi wetu wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani miaka miwili au mitatu iliyopita, Mheshimiwa Rais alizindua ujenzi wa Kiwanda cha Machinjio pale Ruvu. Kiwanda hiki kimechukua muda mrefu na wakati ule Mheshimiwa Rais anazindua ujenzi wake, wananchi wengi walihamasishwa na wakahamasika kufuga ng'ombe wa kisasa kwa kuwanenepesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo halikutosha, wananchi wakahamasishwa na wakahamasika kutenga maeneo ya ufugaji na walifanya hivyo. Jambo la kusikitisha ni kwamba, licha ya fedha za wananchi kutumika pale mpaka sasa hakuna uendelezaji wowote uliofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukipita pale unakuta gofu, vifaa na vitu vingine vinaibiwa na limekuwa ni tatizo kubwa. Vijana takribani zaidi ya 1,000 waliahidiwa kupata ajira kutokana na kiwanda kile. Vijana wamezagaa tu pale Mlandizi, Jimboni kwangu, hawana kazi za kufanya kutokana na matumaini makubwa ambayo wameyapata kutokana na kujengwa kwa kiwanda kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati anakuja hapa, basi atupatie majibu kuhusiana na kiwanda kile kwani kimechukua muda mrefu, jambo ambalo ni sawa na kumtia aibu Mheshimiwa Rais, maana Mheshimiwa Rais alikwenda akafungua mradi ule, umechukua muda mrefu na hauna mategemeo yoyote. Kwa bahati mbaya katika kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona hata sehemu moja ambayo inazungumzia suala zima la kiwanda kile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndiyo mahali husika pa kuomba. Nichukue fursa hii kumwomba tena Mheshimiwa Waziri, pamoja na matatizo ya kifedha, naamini Serikali itasikia kilio cha Wabunge, upo uwezekano mkubwa wa kuongezewa fedha. Naomba Mheshimiwa Waziri atambue kwamba, Jimbo la Kibaha Vijijini vilevile ni la wafugaji kama maeneo mengine, tuna wafugaji wengi tu pale ambao wanafuga ng'ombe, mbuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atambue suala hili kwa sababu wananchi wangu wakati mwingine hata ukiwaambia kuna Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, hawaitambui. Inawezekana kutokuitambua huko ni kwa sababu Waziri hajapata muda wa kutembelea kule ili wananchi wajue kuna Wizara hii. Namwomba tu

Mheshimiwa Waziri, akipata muda wakati mwingine apitie katika Jimbo la Kibaha Vijijini ili aweze kuona kwamba, kuna wafugaji wengi tu pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kwamba, kwa sababu tuna wafugaji wengi na kiwanda kile kikikamilika maana yake tutaongeza pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunalalamika hatuna fedha, kwa sababu kiwanda kile kimekaa kwa muda mrefu. Kama tungeweza kujenga kiwanda kile na kukimaliza tungeweza kupata mapato na Taifa lingeweza kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ningependa kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa sababu tuna wafugaji na mifugo mingi pale, tuna maziwa mengi sana ya kutosha, lakini wafugaji wetu pale wanashindwa kupata soko la kuuzia maziwa. Nashauri kwamba, kwa sababu Dar es Salaam ilipo Wizara ni karibu sana na Kibaha Mjini, Waziri angejaribu kufikiria Jimbo la Kibaha Vijijini liwe mfano kwa kujenga kiwanda cha maziwa pale. Pia angehakikisha anatembelea pale mara kwa mara na kwa kuwa ndiyo njia kubwa ya Wabunge, basi wakipita wataona kwamba, Wizara yake inaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri tu Mheshimiwa Waziri kama upo uwezekano na akiongezewa fedha, afikirie suala la kujenga Kiwanda cha Maziwa pale. Pia nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba, tatizo kubwa linalowakabili wafugaji wangu ni elimu. Tumetenga maeneo ya wafugaji, lakini tatizo kubwa ni elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aweke utaratibu wa kuhakikisha wafugaji wetu hawa wanapata elimu ya kufuga kisasa ili kuondokana na migogoro mingi ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatenga maeneo, lakini tatizo kubwa ni kwamba, yale maeneo ambayo tunayatenga

yanakabiliwa na ukosefu wa huduma muhimu. Kwa mfano, tumetenga maeneo, lakini hakuna malambo, majosho, hilo ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, wakati tunatenga maeneo ni vyema kuhakikisha huduma muhimu zinafika kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile dawa za ruzuku ni tatizo kubwa na wananchi kule wanashindwa kupata dawa na haijulikani dawa zile zinaweza kufika kule kwa muda gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia suala la uvuvi na Wabunge wengi wamezungumzia kwamba, tuna mito, bahari, lakini mkumbuke tuna Mto Ruvu pale. Kama tunaweza kuutumia mto huu ni vizuri na tuna vijana wengi, tukiweka pale miundombinu, tukijenga mabwawa mengine tukaanza kufuga samaki, wakati huo huo tunaweza tukapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Telele atafuatiwa na Mheshimiwa Sanya.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Naomba Waheshimiwa Wabunge watakaopata nafasi ya kuchangia bajeti hii waendelee kama walivyoanza wengine kupigia kelele na kutetea sana bajeti hii ndogo ambayo kwa kweli hairuhusu kutekeleza miradi ya wafugaji na wavuvi. Tupigie kelele kama ambavyo tumepigia kelele bajeti ya Wizara ya Maji na baadaye Serikali ikaenda kutafuta shilingi bilioni 184 na ushehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kwamba, kutokana na kushuka kwa bajeti hii mwaka hadi mwaka ndani ya miaka mitano bajeti hii imeshuka kwa kiasi cha sh. 163,000,000,000; tangu mwaka 2009 hadi bajeti hii tunayoizungumzia leo. Kwa

hiyo, hiyo *graph* inakwenda chini tu, mwisho itafika sifuri na ikifika sifuri basi na mifugo kwa kweli itapotea kabisa, kwa sababu kuna maradhi mengi sana ya mifugo, tunataka kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kwamba, badala ya shilingi bilioni 40 ambayo Wizara hii imeomba kama nyongeza ili iweze kufanikisha shughuli zake kwa kweli waongezewe sh. 163,000,000,000 waliyopoteza ndani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hili linawezekana kwa sababu hata juzi hapa, Wizara hii imeongezewa siku mbili. Hii ni kwa sababu imeonekana kama alivyosema Mheshimiwa Lekule Laizer hapa Wizara hii inabeba Watanzania wengi sana sio chini ya asilimia 30 kama alivyosema na inaweza ikawa ni zaidi. Sasa kama wameweza kuongeza kwa siku mbili kwa nini washindwe kuongeza bajeti. Kama sio yote hiyo waliyopoteza kwa miaka mitano, basi wongezewe hiyo waliyoomba sh. 40,000,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamezungumzia kutenga maeneo ya wafugaji na sio kutenga tu Serikali itenge na isajili maeneo yale ipatikane hati ili wafugaji hawa waendelee kutulia katika maeneo yao. Wakishafanya hivyo lazima miundombinu ya uhakika iwekwe katika maeneo ya wafugaji kama vile kuchimba mabwawa kama walivyosema wenzangu wengi, majosho, wajenge viwanda, watafute masoko kwa ajili ya mazao ya mifugo, wakifanya hivyo angalau hii Wizara sasa inaweza ikavutia kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi mbalimbali wamekwenda ziara kule Botswana, wamekwenda Uganda wametembelea hata mashamba ya mifugo ya Mheshimiwa Rais, maana ni mfugaji yule. Sasa viongozi mbalimbali wanakwenda, lakini wakirudi hawapeleki walichokiona kwa wafugaji wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni wakati muafaka sasa na wafugaji wa kawaida nao watembelee, wapelekwe maana wanasema hasa ndugu zangu jamii yangu ninayotoka, wanasema jicho lililotoka nje likaona, likirudi linaweza kufanya na kuleta mabadiliko. Sasa badala ya kuwaacha tu katika hali yao ya kawaida na wenyewe watoke nje waone wenzetu wanafanya nini ili kuweza kuja kuanzisha mambo ambayo yataboresha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uwekezaji mdogo katika sekta hii. Ni uwekezaji mdogo kwa upande wa Serikali na uwekezaji mdogo kwa upande wa sekta binafsi. Hakuna masoko, hakuna mikopo kwa ajili ya kuendeleza hii sekta ya mifugo. Watu wengine wanasema lazima tufuge kulingana na uwezo wa eneo ambalo tunakusudia kufuga, wanaita *carrying capacity*, lakini ukifuga katika eneo dogo na hakuna miundombinu kama nilivyoeleza, kwa kweli itakuwa ni balaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nina matumaini kwa sababu sekta hii imepigiwa kelele muda mrefu na hakuna mabadiliko yoyote. Naamini katika mchakato wa Katiba mpya, wafugaji watakuwa wametoa maoni yao kuhusu mifugo yao itakuwaje ili Katiba mpya itamke kwamba, mifugo ni zao ambalo ni muhimu kama kilimo na kama tunasema Kilimo Kwanza isifanye sasa hali ya mifugo nayo ikapotea katika mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako magonjwa mengi sana ambayo yanasumbua mifugo. Magonjwa mengi yanasababishwa na kupe zaidi, kwa hiyo tukiweza kudhibiti kupe magonjwa mengi ya mifugo yanaweza kupungua. Lakini yako magonjwa mengine kama *foot and mouth* au miguu na midomo ambayo inahitaji chanjo tu, magonjwa kama na ndigana kali yanahitaji chanjo, magonjwa yanayoenezwa na mbung’o, tulielezwa katika hotuba ya Waziri kwamba hekta karibu 30,000 ambayo ni sawasawa na asilimia karibu 30 ya eneo la Tanzania limekabiliwa na mbung’o. Nimeona huko Serengeti wameweka vitambaa

vyeusi ambavyo mbu akipita pale, anavutwa, ananasa pale na kwa hiyo anafia palepale. Naomba utaalam huo uenezwe katika maeneo yote ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Brucellosis* nao ni ugonjwa ambao unapunguza sana idadi ya mifugo kwa sababu mitamba inatupa mimba kwa wingi kutokana na ugonjwa huu. Mabadiliko ya tabianchi yataathiri pia sana wafugaji kama ambavyo yataathiri wakulima. Kwa hiyo, ni lazima tutafute namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kuweza kuwanusuru wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la migogoro ya wakulima na wafugaji limedumu kwa muda mrefu, lakini vilevile kuna mgogoro unaozuka kati ya wafugaji na wawekezaji na wale wapiga picha ambao wako katika maeneo ya wafugaji. Tunaomba migogoro hii ishughulikiwe haraka na hao wawekezaji nao watambue wafugaji kwamba ni *good neighbours* katika suala zima la uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Telele. Kama nilivyosema, sasa nitamwita Mheshimiwa Sanya na baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Sanya tutampa nafasi Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza nasema, nitakuwepo kesho kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri, kwa sababu hii bajeti inaonekana kwamba *we are not committed, we are not serious,* hii ni Wizara ambayo ina sekta mbili muhimu sana kwa nchi yetu, sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi. Lakini sekta zote mbili hizo hazijafanyiwa kazi zikazalisha na zikasaidia nchi kiuchumi na zikawasaidia Watanzania. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli hatuoni kwamba, sisi Tanzania kama ingekuwa hatuna mifugo katika nchi hii tungetumia kiasi gani cha fedha kuagizia nyama kutoka nchi za nje. Hicho ni kigezo tosha kwamba, Mungu ametunusuru; tuna wanyama wa kutosha wa kuweza kula, lakini akatupa na ziada ya kuweza kuwasafirisha ama nchi za jirani ama nchi za nje, tunafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele zimekuwa nyingi baina ya wafugaji na wakulima, lakini huwezi ukambadilisha mkulima akageuka akawa mfugaji na mfugaji akawa mkulima, ni *two different subjects* hizo. Kilichobaki ni kujengewa mazingira mazuri, wakulima wakawa na maeneo yao na wafugaji wakawa na maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wafugaji wanatangatanga tu na ng'ombe nchi nzima, lakini tumewajengea miundombinu gani ya kuwasaidia. Wafugaji hawana majosho, vituo vya utafiti ni kidogo, maji kwa ajili ya wanyama wao hakuna, matokeo yake tunakuja na *data* hapa kwamba kila Mtanzania anakula kilo 12 kwa mwaka. Ina maana kwa mwezi Mtanzania ambaye anahesabiwa ana nyama nchi ya pili katika Afrika anakula kilo moja kwa mwezi, ina maana kila mtu anakula mshikaki mmoja kwa siku, ndiyo hesabu hii ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utasemaje wewe ni mtu wa pili Afrika, una ng'ombe wengi halafu Mtanzania anakula kilo 12 kwa mwaka, ina maana kwa mwezi ni kilo moja, ina maana hata huo mshikaki mmoja anagawana baina ya yeye na mama nyumbani, kila mmoja anapata vipande viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye mayai hivyo hivyo na hawa wafugaji kama hatukuwaangalia, tukawatengenezea mazingira mazuri siku watakayogoma kuchinja ng'ombe, basi tutamaliza mbuzi, sungura, kuku, mayai na mwisho tutakula kunguru nchi hii. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hawa wanaolisha nchi nyama. Kama wewe unapumzika baada ya kutoka hapa,

kutoka kazini ukahitaji nyama choma, ni hawa wafugaji. Ni hawa wanatoa maziwa, ni hawa wanatoa ngozi, ni hawa wanaweza wakazalisha maziwa zikatoa *products* nyingine siagi, jibini na mambo mengine chungu zima, matokeo yake maziwa hakuna. Mashule yetu tunawapikia uji watoto bila maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ajabu na haya ni maajabu makubwa duniani kwamba Tanzania ni nchi ya pili kuwa na mifugo lakini hatunywi maziwa. Kenya hawana mifugo kuliko sisi, lakini wana maziwa mpaka wanasafirisha wanatuletea Tanzania. Kwa nini tusitengeneze viwanda vikazalisha viroba vya maziwa badala ya viroba vya ulevi, tukawapa nafuu wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusifanye *insemination* baada ya kutoa kilo 200, ngombe akatoa kilo 500 na 600. Siku zote itakuwa hapa tunakuja tunazungumza masuala ya matatizo baina ya wakulima na wafugaji. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijijini pako Peramiho, kuna Kijiji kinaitwa Ngadinda, kama yeye hakielewei kuna matatizo kimevamiwa na wafugaji, kwa nini? Kwa sababu hatujatenga maeneo, hatuna *plan survey* ya *land* ya kuwafanyia watu wetu, hawa wafugaji huku simba na faru, huku mkulima na hii *reserve* ya *investment* hatuna, wenzetu wanazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nendeni Bostwana mkaone wanavyofanya, nendeni Malawi, Afrika ya Kusini, hadi hii leo tunaagizia maziwa, hadi hii leo tuvae viatu vya plastiki kutoka Thailand, hadi hii leo siagi itoke Kenya, *is quiet ridiculous*. Wamasai, Wasukuma, Wabarbaig wasaidiwe sasa wajisikie kwamba huu ndio uhuru wa Mtanzania katika kilimo cha kisasa na ufugaji wa kisasa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye uvuvi; anza Tanga njoo zako Dar es Salaam teremka chini, Lindi mpaka Mtwara tunafanya nini na samaki. *Lake Victoria dominated by three states* Kenya, Uganda na Tanzania ile *portion* ndogo

ya Tanzania, tunazalisha samaki wengi wakati katika *Lake Victoria* kuna *species* kidogo za samaki kuliko za bahari kuu na tunasafirisha *in billions* kupeleka Ulaya, ndege zinakuja zinachukua, lakini hakuna ndege hata moja inayokuja kuchukua hata dagaa Dar es Salaam. *It's quiet shame* na vijana wapo hawana kazi, wako Kilwa, Mtwara, Lindi, Tanga, Dar es Salaam, Pemba na Unguja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine za boti wala sio ghali. Karibu nakwenda kuzindua mradi wangu kule Jimboni kwangu, nimeagizia hizi mashine za Japan, *they are so cheap* na hakuna ushuru nchi hii. Haya mabilioni ya Mheshimiwa Kikwete kama yangetumika katika suala la uvuvi, basi vijana wengi wangepata ajira. Matokeo yake fedha zile ukienda ukizichunguza, hujui zimechukuliwa na nani zimefanyiwa miradi gani zimezalisha nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri watume wataalam waende Mauritania, Senegal, Namibia wakaone namna gani nchi zile zilivyojikita katika uvuvi wa kisasa. Wana *fishing ports,* sisi hatuna hata *fishing ports,* tumekamata meli moja la Magufuli itabakia historia na litakuwa kwenye *archieves* mpaka kiama ndio hilo hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda kudai ukubwa wa bahari mpaka kilo 1,200 wakati maji ya futi tunashindwa kuzoa hata chaza na chiwale. Kwa nini tusiwape watu wakaenda wakavua. Hii *deep sea fishing* kuna mameli yanavuna kule. Je, Serikali yetu inazo taarifa kwamba kuna meli ngapi zinavua tani ngapi? Ndiyo Namibia wanavyofanya, meli inaripoti bandarini inakwenda kuvua, baadaye inarudi ile *trawler* kuja kuonesha kwamba nimepakia kiasi gani cha samaki ili nchi ipate mapato kutokana na uwezo wa kile chombo na samaki iliyowabeba, sisi tunao mpango huo? Hatuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi *survey* ya baharini zinakwenda na ndege za kisasa, zinazochukua njia za *GPS* za *satellites* kuweza kujua meli ziko wapi. Halafu hii Wizara iwe na ndege yake au ndege zake, wanapo-*trace* kitu

kwenye hiyo *satellite,* wawe wanachukua ndege yao wanakwenda kuikamata ile meli na kwenda kuizunguka leo, hamna hata helikopta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwende mkakodi ndege *Airport* ya kibiashara hata wale wenyewe wakiiona ile ndege iwapo ni *Coaster*, *ZanAir* wataona *this is a commercial flights* hawatashtuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulikwenda mpaka Jordan tukaambiwa ndege zipo ambazo zina *camera* za kisasa, zinachukua *radius* kiasi gani ya bahari na bei yake ni *1.5 dollar million.* Hivyo kila mwaka kununua angalau ndege moja kwa miaka miwili tukawa na ndege mbili inashindikana, mnakuja kutuletea bajeti ya shilingi bilioni 47! Kama mngekuwa *serious* katika hili hata sisi Wabunge tungekuchukulieni mkopo *CRBD* mkafanya kazi. *Yes what is 47 billions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sio fedha za kujinadi kwamba nyie mnaweza kufanya kitu, hamuwezi kwa sababu mna sekta mbili katika nchi. Lakini sisi tuna tatizo moja Tanzania nimeligundua hilo, ukipata kipya kikuukuu kinakuwa kinyemi. Tumepata gesi tena mawazo yetu ohoo, gesi wee, utajiri huo unakuja, utakuja *for how long* wakati tunao kuku wanataga kila siku, wataka kumchinja kuku upate mayai yote siku moja huwezi. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujikite na haya mambo ambayo tunayo mkononi, ukulima yaani kilimo, ufugaji na uvuvi. Nakwambia unaweza ukachangia asilimia mpaka asilimia 65 ya bajeti ya Serikali ya Tanzania ukiachilia mbali utalii. Hizi *uranium, gold* sijui gesi acha ziende katika mfumo wake, lakini tukijikita huku kwenye uchumi halali, uchumi utakaotoa ajira, vijana sisi tunawafanya kama kofia ya Msikitini ukiingia unavaa ukisha kusali unaitupa. Tunawahitaji wakati wa kura tu, wakishapiga kura, basi miaka mitano tunangojea tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwajengee mazingira waipende nchi yao wafanye kazi, wazalishe. Mimi kwa hili bwana nitalisimamia mpaka dakika ya mwisho. Shilingi bilioni 47 kuletwa hapa Bungeni, bora mngekaa kwenye Kamati mkapanga matumizi yenu, hii ni mishahara tu. Kuna *excess* gani pale, kuna fedha kidogo ambazo zimetoka nje na fedha za ndani kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kesho tupo tunatoa shilingi, utarudi Dar es Salaam kwa miguu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Sanya kwa mchango wako na nafikiri Mheshimiwa Waziri amesikia na kile kilio cha wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho kule Ngadinda wanavyopata shida ya kuingiliwa na wafugaji. Kwa hiyo, atatuwekea mambo sawa huko.

Waheshimiwa Wabunge nilisema nitamwita Mheshimiwa Mangungu, atafutiwa na Mheshimiwa Kitandula na atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii muhimu na moja katika mihimili ya ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa mujibu wa kanuni ya 61(1) naomba ku-*declare interest* kwamba, yapo mengine ambayo nitayazungumzia naweza kwa maana moja au nyingine nina maslahi nayo binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya bajeti hii imedhihirisha ni jinsi gani ambavyo inakwenda ikishuka kila mwaka. Nimepiga hesabu za haraka haraka inaonesha kwamba kuna wastani wa shilingi zisizopungua bilioni 15 kila mwaka zinashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa *trend* hii tunayokwenda nayo, baada ya miaka mitatu inayokuja

Wizara hii itakuwa haina bajeti na inawezekana Waziri atalipwa mshahara kupitia Wizara nyingine, huko ndiko tunakoelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kuongeza bajeti hii kwa sababu hata ukienda kwenye cha bajeti ya *development* upande wa *fisheries* hakuna senti hata moja ambayo imepangwa na Waziri anakuja hapa kwenye Bunge kuja kuomba apitishiwe bajeti sijui kwa kazi ipi anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mpango wowote wa kuendeleza maeneo ya uvuvi na katika sekta ya uvuvi liko tatizo kubwa sana na Wizara imeamua kukaa kimya bila kutoa majibu yanayoeleweka. Kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita wamezuia uvuvi wa Kamba katika maeneo ya *Delta* na maeneo ya ukanda wa Kilwa bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu yao wanasema kwamba, wazaliane umri wa kamba tangu anazaliwa mpaka anazeeka hadi anakufa ni miezi tisa, hii miaka sita mnataka kamba hao wafanye kitu gani? Tunaomba tupate majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo katika uvuvi; wavuvi wadogo wadogo wananyanyaswa, wanateswa na mara nyingine hata jeshi huwa linatumika kwenda kuwakamata, kama vile katika eneo la ukanda wa Tanga, lakini vilevile katika maeneo mengine. Sasa najiuliza Wizara imewahi kufanya utafiti wa kujua sababu zinazopelekea watu wakafanya uvuvi wa haramu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa wananchi au wavuvi hawa hawajawezeshwa kuwa na vifaa kuweza kuvua vizuri. Ni jambo la kustaajabisha makampuni ya kigeni yanakuja yanapewa leseni na tumeambiwa *only* 1.3 milioni *Dollars* ndiyo iliyopatikana katika leseni zilizotolewa katika leseni za uvuvi ule wa bahari kuu. Samaki wanazaliwa mpaka wanakufa au mara nyingine kwa sababu ni *immigrated*

*species* wanakwenda kuvuliwa katika maeneo mengine, sisi huku tunawazalisha, wanazaliwa katika ukanda wetu wanakwenda kuvuliwa mahali pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka kuanzia hivi sasa licha ya leseni ambayo inachajiwa kwa mvuvi, tunahitaji tuwe tunalipwa *royalty* kama watu wa madini ambavyo wanalipwa, maeneo yote ya Ukanda wa Pwani na maeneo yote ya uvuvi ili pesa zile ziweze kusaidia sekta ya uvuvi kwa wavuvi wadogo. Sisi tunaotoka maeneo ya ukanda wa Pwani samaki ndiyo madini yetu, kwa hiyo na sisi tunataka tulipwe *royalty. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nizungumzie ni mbolea za kemikali katika kilimo. Tunahamasisha sana utumiaji wa mbolea za kemikali katika kilimo, lakini mbolea hizi baada ya kutumika zinakusanywa na mvua zinaingia kwenye mito, zinapelekwa baharini, samaki wanakufa, sasa tunataka nini? Tunataka kilimo sana au tunataka kufuga sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo inabidi tuliangalie kwa sababu unapotumia mbolea za kemikali unatengeneza green *algae* ambao wana–*suck* ile *oxygen* yote kwenye maji, matokeo yake yanakuwa ni *dead water,* samaki hawawezi ku- *survive*. Sasa hili tuliangalie na lazima tuweke namna ambayo tunaweza kusaidia wavuvi wetu tusilaumu tu kuwa tunavua bila kuwa na uvuvi endelevu lakini matatizo kama haya yapo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika eneo la mifugo, tumekuwa na migogoro mingi katika maeneo mengi nchini, lakini kwa nini Wizara zinazohusika Wizara ya Utalii, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi, msiweke mpango mkakati ili kuweza kuainisha maeneo ambayo yanafaa ufugaji na kuwapa *skills* wale wafugaji, jinsi ya kuweza kukuza nyasi, kuzalisha chakula kwa ajili ya mifugo yao na kuondokana na haya matatizo, maeneo yote bora wanapewa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwa kuwa wawekezaji wanao uwezo mkubwa ndiyo wapewe maeneo yasiyofaa ili waweke miundombinu wafuge mifugo yao na yale maeneo ambayo hayana miundombinu wapewe wafugaji wetu ambao hawana uwezo ili waweze kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu msamiati wa watu wanaohama, watu wanaofuga, sisi tumewapokea Wasukuma wengi sana sababu kubwa ni wanetu, lakini wapo wengine ambao wanakuja hapa wanahamasisha ukanda, hawa wakae Kanda hii na hawa wakae Kanda hii. Je, hao watu ambao wanahama leo kwenda mahali pengine, tukishaweka ukanda watu hawa wata-*move* vipi kwenda katika kila eneo? Tusilete kilio cha mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni masuala ya *genes Bank*, Tanzania bado hatujawa nazo, leo itafikia wakati hawa kuku ambao tunawatumia watakuja kupotea na tutagemea kuagiza kutoka nje, utaratibu huu Mheshimiwa Waziri unauelewa vizuri, tuweze kuhifadhi *genes* zetu hasa kwa kuku wale wa kienyeji *species* zingine hata za ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni katika hizi *Ranch* zetu za Taifa. Yametokea matatizo Mheshimiwa Laizer amezungumza hapa, ng'ombe walikufa katika maeneo mengi, lakini utakuta katika baadhi ya maeneo hata Kongwa na maeneo yale ya Ruvu kwenye zile *Ranch* za *NARCO* walikataliwa wafugaji wasiingie pale kwenda kulisha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mali ya umma, sasa pale umma unakuwa na maslahi kwa nini tusiruhusu kwa kushirikiana na wale wananchi, wakaenda kulisha mifugo yao, mara nyingine tungeweza kuokoa fedha nyingi ambazo Mheshimiwa Rais aliidhinisha ili wananchi waweze kulipwa fidia ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, nataka nizungumzie suala la *artificial insemination,* sijui kwa nini mpaka leo tunakwenda kusomesha watu kule kwenye chuo chetu cha *LITI*, lakini wakitoka pale vifaa hakuna, hawa Maofisa mifugo na kada nyingine katka sekta ya mifugo hawapewi ujuzi wa kutosha, wakishapewa ujuzi hawapewi vifaa vya kazi. Kwa hiyo, ni sawasawa na tunachota maji kwa uma tunatia kwenye tenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijakubali kuunga mkono hoja mpaka pale nitakapoona fedha imeongezwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mangungu. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa tutamsikiliza Mheshimiwa Kitandula na baada yake atafuatia Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa bajeti hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uzima mpaka siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kuwa siungi mkono hata kidogo hotuba hii. Siungi mkono katu, nasema hivi kwa sababu bajeti hii haituhakikishii watu wa Ukanda wa Pwani kupata maisha bora, nasema hivyo kwa sababu bajeti hii haiwahakikishii wananchi wangu kuondokana na umaskini. Naikataa bajeti hii kwa sababu ni mwendelezo wa ahadi hewa ambazo tumekuwa tukipewa watu tunaotoka kwenye ukanda wa uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuikubali bajeti hii ni kuwaambia watu wangu wa Mayomboni, Moa, Doga, Kichalikani, Kwale, Manza, Boma kwamba, waendelee kuhangaika na umaskini wao. Siko tayari katika hilo, nitakuwa tayari kuunga mkono bajeti hii pale tu kilio cha kila Mbunge aliyesimama hapa kusema Wizara hii iongezewe fedha kitakapotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera zetu na mipango yetu imewaangusha watu wanaotoka kwenye ukanda wa uvuvi. Leo nitajikita katika sekta ya uvuvi peke yake, sitagusia mifugo kwa sababu Mzee wangu Ole-Telele na Mzee wangu Laizer wamezungumza sana kuhusu sekta ya mifugo, walichosema kama hatusikii, basi hatutasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukubali bajeti hii ni kukubali kuendelea kwa migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima. Tusikubali, nawashawishi Wabunge wenzangu ambao tumepewa dhamana ya kuisimamia Serikali, tusimame kwa sauti moja, kuwaambia *this is unacceptable,* lazima tuongeze bajeti kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Shirika la Chakula Duniani, *State of the World Fisheries and Agriculture* kwa mwaka 2012, inatuambia hivi, kwa mwaka 2012 jumla ya tani milioni 154 zilivuliwa katika ukanda wa bahari na kwenye maeneo ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hizo tani milioni 131 zilitumika kwa chakula, lakini samaki waliopatikana kwa kufugwa ni tani milioni 79. Ripoti hii inatuambia kuwa, katika sekta ya uzalishaji wa chakula hakuna sekta inayokua kwa kasi ulimwenguni kwa sasa kama ufugaji wa samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miongo mitatu mfululizo, sekta ya ufugaji wa samaki imekuwa kwa 12% mfululizo. Hii inatakiwa kutufanya tufungue masikio, Wachina ambao tunawapigia mfano kwa mafanikio yao ya kiuchumi, wamelichukua hili, wameichukulia sekta ya ufugaji wa samaki kwa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti hii pia inaonesha kwamba, kwa mwaka jana ufugaji wao wa samaki wameweza ku-*export* kwenda soko la Marekani tani milioni 1.1 ambayo hii ni sawasawa na Dola za Kimarekani bilioni 5.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa kubwa la kiuchumi kama Uchina linaona umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya ufugaji wa samaki, sisi Tanzania si zaidi, lazima mipango yetu ijielekeze sasa kwenye kuhakikisha kuwa tunaipa kipaumbele sekta ya uvuvi hasa tukizingatia kuwa 5.7% ya eneo letu ni maji yanayofaa kwa uvuvi, kwa maana ya maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna ukanda wa bahari *square kilometer* 64,000, maeneo yote haya hayatumiki ipasavyo, hii haikubaliki hata kidogo. Miaka mitatu iliyopita wenzetu Wakenya baada ya kugundua kuwa upatikanaji wa samaki kwenye Ziwa Victoria unapungua kwa kasi, walianzisha mpango maalum wa kujielekeza kwenye kufuga samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango ule, walihakikisha kwamba, kila Jimbo walijenga mabwawa 200. Kwa hiyo, mwisho wa siku walikuwa na mabwawa 30,000 katika nchi nzima ya Kenya. *Target* yao walikuwa wanataka kuwa *rural direct investment* na *revenue* ya bilioni 20, jambo ambalo wamefikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wana samaki wengi kiasi kwamba wanapata shida ya kupata soko wana-*target* kuja Tanzania maana wameshashika soko la Kongo, Sudan, na Uganda, kwa hiyo, sasa wanataka kuingia Tanzania. Hivi sisi mpaka lini tutaendelea kuwa soko la watu wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fursa hizi, lakini hatuzitumii. Nilikuwa nasoma ripoti moja inaniambia kuwa, hata hawa *tilapia* ambao Wachina wanaongoza sasa, walichukua mbegu kwenye Ziwa Victoria, hadithi ni ile ile ya mafuta ya Mawese, hii haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kitandula. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Rose Sukum ajiandae.

**MHE. RICHARD N. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Mifugo, lakini kwa leo usinishangae sana kwa mara yangu ya kwanza mtambue kabisa kuwa siungi mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suing mkono kwa sababu nitaulizwa kule ninakotoka kwenye Jimbo langu, kwenye Wilaya yangu, kwenye Mkoa wangu, lakini ni pamoja na wafugaji wa ng'ombe Tanzania, umeunga mkono Hotuba ile kwa sababu gani? Niungane na mapendekezo ya Kamati ya kuiomba Serikali nyongeza ya shilingi bilioni 40 ipatikane. Bila nyongeza ya hiyo hela, sitaunga mkono, nitakwenda kulala na shilingi kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zikiongezwa hizo hela, tutapata madawa kwa ajili ya mifugo, malambo kwa ajili ya mifugo, utafiti kwa ajili ya mifugo, majosho na kadhalika. Lakini ili Waziri aende kutekeleza majukumu ambayo yamo kwenye kitabu chake kwa pesa hii, Waziri tutakuwa tunamwonea. Tunataka tumpe pesa za kutosha ili kwenye bajeti ijayo, tuje tumbane na nina uhakika Serikali tasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali bilioni 40 itafute kwa njia yoyote ile ili kusudi Wizara iongezewe pesa. Wamesema wenzangu hapa hivi unapotoa bilioni 47, zikafanye nini kwenye Wizara hii? Ni pesa kidogo sana hizi, naishauri Serikali na nafikiri imenisikia na imesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sekta ya mifugo na wenzangu wamesema na mimi naomba niseme. Ng'ombe wanadhalilishwa sana Tanzania, wafugaji wa ng'ombe wanadhalilishwa sana sijui wameikosea nini Tanzania, kila wanakopita wanazomewa, wanasumbuliwa, hawa wafugaji wa ng'ombe wamekuwa kama vile wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wananchi wangu wa pale Sumve, Malya na Nyambiti, Shimbamatoranya na Mponeja, wana mifugo yao. Wamesumbuliwa huwezi kuamini, utafikiri ni wakimbizi kwenye nchi yao. Ng'ombe wamekuwa kama vile paka, wakati tukitoka hapa tukienda Kantini tunakumbana na nyama za ng'ombe. Lakini tunaposikia ng'ombe, tunasikia kichefuchefu. Mimi sielewi ni kwanini?

Hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na wachumi wako wote ulionao, hivi hamjui kwamba ng'ombe ni mali? Kwanini msiwekeze kwenye ufugaji wa ng'ombe na mwenzangu Mheshimiwa Kitandula bahati nzuri amezungumza sana hapa. Ukiwekeza kwenye mifugo, uvuvi, hizi nakisi za bajeti za Serikali zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali utafikiri haina masikio, haisikii, haioni! Hivi wenzetu Botswana wao wamewezaje, sisi tusiweze? Hivi Watalaam tunao au hatunao? Naiomba Serikali kupitia Wizara hii, tusingependa tena mwakani kwenye bajeti ijayo, pamoja na maneno mazuri yaliyomo humu ndani, tusisikie huo upungufu.

Mheshimiwa Waziri wewe ni mtalaam, kijana uliyebobea kwenye fani hiyo, Naibu wako, Watalaam wako, Madokta, Maprofesa wa mifugo na uvuvi. Hivi inapofika tarehe 30 unakwenda dirishani kuchukua mshahara kwa kazi gani uliyofanya? Maana yake ni lazima ujiulize, huu mshahara ninaoupata ni kwa kazi gani kama yale ambayo umeambiwa utekeleze hutekelezi? Huku ni kuwanyonya na kuwaibia Watanzania na Serikali. Tunaomba kila mtu kwenye sehemu yake awajibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uwajibike vizuri, Serikali ni lazima itoe pesa Shilingi bilioni 40 ziwe Shilingi bilioni 87 na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba niende kwenye sekta ya ngozi. Tulipitisha sheria hapa, tukatoa kwenye asilimia 40 kwenda kwenye asilimia 90. Hii ina tatizo. Pamoja na

kwamba mnasema kuna mfanikio, lakini mafanikio hayo ni madogo mno. Naomba tufanye utaratibu wa kubadilisha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Kengele ya kwanza au ya pili?

**MWENYEKITI:** Kengele ya kwanza, endelea.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tubadilishe utaratibu. ile ngozi ghafi na yenyewe ikiwezekana itozwe ushuru kuliko ilivyo hivi sasa. Tatu, naomba Mheshimiwa Waziri katika hizi ranchi zako kumi, nenda ufanye sensa tena. Hizi ng'ombe ulizotaja kwenye kitabu chako, mimi nasema siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Watanzania hao wanaosimamia vyombo vilevile wanaweza wakajilimbikizia magari ya Serikali, sembuse ng'ombe! Anahamisha gari la Serikali linakuwa ni la kwake, lakini ni gari la Serikali. Sembuse ng'ombe! Naomba Mheshimiwa Waziri uende ufanye sensa upya. Hizi zinazotajwa kwenye ranchi kumi siyo halisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kwimba inaomba gari kwa ajili ya Idara ya Mifugo na barua ipo ofisini kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba siungi mkono hoja mpaka Shilingi bilioni arobaini zipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Ahsante Mheshimiwa Ndassa. Sasa tutamsikiliza Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, atafuatiwa na Mheshimiwa Mfutakamba na Mheshimiwa Malocha ajiandaye.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi fursa niweze kuwa mchangiaji mmojawapo. Lakini ninaanza kwa kusema, sisemi kushika Shilingi kwa sababu Waziri mmoja alisema ukishika Shilingi ya Uwaziri, napokea ya Ubunge. Sasa sisi tunasema tutakutoa ndani ya Uwaziri na sababu zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi maana yake ni kuendelea kutoka kwenye kitu kidogo au kibovu kwenda kizuri. Lakini Wizara hii ya Maendeleo kutenga fedha Shilingi bilioni 47, eti kwa sababu ni kwa ajili ya Wizara yote ikiwa ni mishahara pamoja na fedha ya Maendeleo, hii siyo kweli. Hii ni kudhalilishana au ni kuidharau Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kusema Wizara ya Mifugo inadharauliwa wapi, ni kwenye suala la maendeleo. Mimi suala la mishahara yenu, masuala ya *OC* shauri lenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutengwa Sh. 8,973,316,000/= kwa ajili ya maendeleo ni ndogo sana kwa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Tena matokeo yake kwenye randama mliyoandaa, mambo mengi yanayohusishwa humu ni makaratasi, sijui ku-*supply* kompyuta, sijui kitu gani, wala haihusiani na ng'ombe wenyewe, wala haihusiani na samaki wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Wizara hii ikipewa pesa, siyo bilioni 40, nadhani iwe ni Shilingi bilioni 200. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri mwenyewe tarehe 8 ulijibu swali langu ukasema Wizara hii ina-*retain* kwa kutokununua minofu nje ya nchi trilioni 15. Sasa kama ina-*retain* trilioni 15, maana yake ni minofu ya samaki na minofu ya nyama, ni kwanini sasa Wizara hii idhalilishwe kiasi hicho? Kwanini Wizara ya Uvuvi isipewe fedha za kutosha ili wavue vizuri au wenzetu wa mifugo au wachungaji wapewe fedha za kutosha kwa ajili ya malambo, kwa ajili ya kutengewa ardhi, na kwa ajili ya kuweza kupata dawa kwa bei nafuu. Lakini matokeo yake mmewaacha hawa wachungaji wanahangaika wenyewe, hawana hata maeneo.

Sasa mimi nasema hivi, hii Wizara ituambie, inapoomba pia hizi fedha za nyongeza, Shilingi bilioni 40 ni kwa ajili ya kununua haya makaratasi na kompyuta au kuwasaidia wavuvi na wachungaji. Mimi ninachoomba ni hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuielezea Wizara hii pia kwa sehemu nyingine. Wafugaji wanahangaika, migogoro imekuwa mikubwa, kila anayesimama hapa anazungumzia habari ya migogoro. Naomba utuambie Mheshimiwa Waziri, naona unasemeshwa hapo hutaki kutusikiliza, naomba utuambie, wafugaji ni lini wataacha kuhangaika? Wafugaji ni lini wataacha kuhamahama? Ni lini wafugaji wataacha mateso ya kuweza kuuza minofu yao? Kwa sababu tunauza ng'ombe kwa bei ya chini halafu matokeo yake wenzetu wanauza kwa bei ya juu kwa sababu ndio wenye viwanda. Je, utuambie sasa, sisi ni lini viwanda vyetu vitatengamaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, naona Mheshimiwa Waziri wa Fedha anakusumbua hapo, lakini mimi naomba aondoke kwa sababu anatusumbua na sisi, nawe usiweze kutusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuelezea kwamba hapa wamezungumza suala la kwamba wametenga maeneo, kuna Halmashauri zimetenga maeneo, ni uwongo mtupu! Kwa Babati tu ambako ni Mkoani kwetu. Babati ipi iliyotenga hekta 20,000? Wapi? Tuambieni, Babati ipi? Sisi ndiyo watu wa kule kwa nini mseme uwongo. Hii taarifa yako ni ya uwongo pia. Mnaandikia mezani, mnapeana taarifa ambazo siyo sahihi. Wilaya ya Hanang' iko wapi? Kwanini wasitengewe Wilaya ya Hanang' wakati ina wafugaji ni wengi? Simanjiro iko wapi? Kwanini wasitengewe maeneo yao ya ufugaji? Kiteto iko wapi? Maeneo ambayo Waziri yupo wa Kiteto, yake pia haikuwekwa hapa kwa sababu ni uwongo.

Kiteto wana mifugo mingi, lakini zimetengwa heka 400 tu, ni kidogo sana! Lakini mifugo ni mingi sana. Naomba utuambie hii taarifa umeitoa wapi? Waziri watu wako ni

waongo, wanakupa taarifa za uwongo Mheshimiwa Waziri. Nawe ni lini umekwenda kufanya Mikutano na wafugaji ili wakueleze. Tuambie ni sehemu gani ulikwenda? Wilaya gani? Kama ni Wilaya ya Hanang', uniambie ulikutana na wafugaji wa Kijiji gani ambao wanahangaika na maeneo, ukawaeleza kwamba mmetengewa eneo fulani. Hawa wengine uliowatembelea ukaja kuwadanganya Waheshimiwa Wabunge kwamba wametengewa eneo, ni wapi? Hiyo ni uwongo kabisa! Naomba kweli Mheshimiwa Waziri, mimi nitatoka na wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kwenye suala la malambo, fedha zimetengwa Wilaya nzima unaipa lambo moja, tena ni malambo ya mwaka 2012 ya mwaka huu hatuyaoni. Niambie Wilaya ya Hanang' inapata lini malambo? Yale ambayo ni ya *PADEP* yaliyojengwa zamani unayarekebisha lini ili yawe na maji? Kwa sababu hakuna hata lambo moja lenye maji. Tunaomba utuambie, tunafanyaje kwa ajili ya malambo? Kwa sababu bila malambo ndiyo maana ng'ombe wanahamahama, hakuna maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na sehemu ya *NARCO.* Wenzetu *NARCO* ni shirika lililopo ndani ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Kilimo naomba kuwaelezeni kama hamkufuatilia; Baraza la Mawaziri mwaka 2002 Waraka Na. 2 walitoa kwamba mashamba ya *NARCO* sasa hivi yanatakiwa yagawanywe kwa *blocks* ili wafugaji wadogo wadogo wapewe. Juzi mmetangaza Mkata. Mlipotangaza Mkata, mmeweka mambo magumu. Mnataka wawekezaji kutoka nje wawekeze badala ya wawekezaji kutoka ndani. Wakati Serikali hii ilisema hatutawapa wawekezaji kutoka nje bali watakuwa wa ndani.

Sasa hebu niambie tusaidiane hapo, Wizara ndiyo mmehusika. Mimi nasema Mheshimiwa Waziri wewe ndiyo umehusika kwa asilimia mia moja. Kwa nini muweke mazingira magumu ili wafugaji wadogo wadogo wasiweze kuomba kuwa Wawekezaji kwenye mashamba ya *NARCO*? Kwanini mnawawekeza watu wa nje? Tutaangalia kwa shamba la

*NARCO* la Mkata. Kama atawekwa mtu wa Oman, maana yake mnauza nchi hii. Tunataka watu wa Kilosa waingie, Watanzania waingie ndiyo wawekezaji lakini sio kutoka Oman. Maana yake tumeona *list* ya majina lakini hatujui ni nani anapewa. Kwa kuwa hatujui ni nani anapewa na sisi tuna uhakika anayepewa ni yule mwenye hela kubwa; sasa kama mmekwenda kwenye hela kubwa mewaacha wafugaji wadogo wadogo wana ng'ombe, *NARCO* wangekuwa wanashiriki pamoja na kuchunga na wawekezaji wa mashamba hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Uvuvi kidogo, na namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu haya yametokea kwenye Mkoa wa Manyara; kufungwa kwa maziwa. Wavuvi wanategemea uvuvi tu na wachuuzi wana tegemea uvuvi tu. Mkiwafungia maziwa: Je, hawa Wavuvi hawafi na njaa? Mmewapa mbadala nini? Matokeo yake watu wanahangaika wanakuwa wezi! Hivi ni utaratibu wa namna gani wa Wizara kufunga maziwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kujua, kwa sababu maziwa yote katika Mikoa karibia mitatu, wanasema Mkoa wa Manyara, Tanga na Kilimanjaro wamefunga maziwa kwa miezi sita. Unategemea wale wataishije kama siyo kuwatesa? Tuambieni mbadala wa kuwasaidia wale ambao walikuwa ni wavuvi na walilipa leseni. Je, Serikali inasemaje kwa kulipa leseni? Wale wachuuzi: Je, wanaishije ili waweze kukimu maisha yao. Kwa nini Serikali inajichukulia tu hatua au kila mtu anaweza kuamua kufunga ziwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haya yametokea kwenye ziwa Basotu, ziwa Babati, ziwa Burunge pamoja na ziwa la Nyumba ya Mungu. Tunaomba msaada wenu na mtuambie tunawasaidiaje wananchi wanaohangaika na maisha yao? Matokeo yake wanafungwa na kusingiziwa kesi za ajabu ajabu kwa sababu watu wamelipia leseni, wanadai leseni zao walipwe na bado hawalipwi, wengine wanalipishwa faini za ajabu ajabu. Tunaomba msaada wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba kusema kwamba siungi mkono hoja, na ninasema kwamba Waziri huwezi kazi ya mifugo kwa sababu umeshindwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rose ni kengele ya pili, naomba uheshimu muda.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Naomba Waheshimiwa Wabunge muwe mnajali kengele ya muda.

Nilisema nitamwita Mheshimiwa Mfutakamba na nikasema nitamwita Mheshimiwa Malocha, mnisamehe sana, nimeangalia vibaya kwenye orodha yangu. Mheshimiwa Malocha hajaomba kuchangia Wizara hii, lakini badala yake atachangia Mheshimiwa Kilufi ambaye yupo kwenye orodha ya Wabunge wa CCM. Mheshimiwa Mfutakamba atafuatiwa na Mheshimiwa Kilufi.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika Wizara hii muhimu ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Wizara hii inahitaji kuwa na Wakala wa Miundombinu ya Ufugaji. Kwa maana hiyo, Wizara hii ni lazima iongezewe pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara hii ni makubwa. Kama bajeti finyu hii waliyopewa tutakuwa tunawalaumu, tunamlaumu Mheshimiwa Waziri, tunamlaumu Naibu Waziri na tunamlaumu Katibu Mkuu, waongezewe fedha ili waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina imani kubwa na Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, sina matatizo naye kabisa, ni mtalaam aliyebobea, na Naibu wake ni mzoefu mkubwa pamoja na Katibu Mkuu wao Dkt. Charles Nyamlundwa. Tuwape *support*, tuwasaidie ili Wizara hii iweze kuwa na fedha

za kutosha na kuanzisha Wakala wa Miundombinu ya Ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Serikali au nchi kuagiza samaki au kuagiza nyama kutoka nje, hili halikubaliki. Hili halikubaliki kwa sababu wao wakiongezewa pesa wataweza kufanya kazi. Nanong'onezwa hapa, watawezaje kazi? Nataka kusema hivi, tuwape bajeti ya kutosha, halafu tuangalie kama hawatendi. Hiyo ndiyo haja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuweza kujipanga. Mimi mwaka 2009 nilikuwa *DC* Kilolo, tulifanya safari ya China, mimi ndiye niliyeongoza msafara huo, nilikuwa na Wawakilishi kutoka Zanzibar kwenye masuala ya uvuvi, lakini kutoka Bara ilikuwa ni masuala ya kilimo cha Chai. Lakini tuliporudi hapa tulikuja na Mwekezaji wa Ranchi ya Ruvu kuanzisha kiwanda cha nyama.

Nataka Mheshimiwa Waziri aniambie nini kilitokea, kwa sababu wale watu wlaisema wana fedha, wanataka kuja kuwekeza hapa, na nilikuwa naamini kile kiwanda kingekuwa tayari sasa 2013. Ninahitaji majibu kwa suala hilo la kiwanda cha nyama; nini kimetokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja suala la *pasture development*. Tarehe 27 Oktoba, 2010, Rais wa Jamhuri ya Muungano - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, pale Isikizya, Ilolasimba, alitoa kauli kwamba kutakuwa na mpango kabambe wa kuanzisha maeneo ya malisho. Ninashukuru sana katika kitabu cha hotuba ya Waziri, nimeona kabisa ukurasa wa picha kule mwishoni, nimeona eneo ambalo zinapandwa nyasi aina ya mikunde kwa ajili ya malisho.

Nimeona Kongwa malundo ya majani ya kulisha hii mifugo. Naomba utaratibu huu, bajeti zitosheleze. Mimi Igalula nina Kata 10. Zile Kata zote 10 ni za Wafugaji, Loya, Goweko, Nsololo, Kigwa, Miswaki, Lutende, Igalula kote ni wafugaji. Lakini wanatangatanga, mazingira yanaharibika, miti inakatwa, vyanzo vya maji vinaharibika. Ni lazima Wizara isimamie mpango wa matumizi bora ya ardhi ili tuweze

kuweka maneo ya wafugaji, maeneo ya kilimo, na tuweze kuhifadhi mazingira ili maji yaweze kuendelea kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kupata jangwa haraka sana Jimbo la Igalula na sehemu nyingine zote. Uwekwe utaratibu maalum utakaosaidia maeneo ambayo kutakuwa na malambo, kutakuwa na majosho na maeneo hayo tuweze kuangalia utaratibu mzima wa viwanda vya kusindika nyama na viwanda vya kusindika ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani jamani tuagize nyama kutoka nje ya nchi wakati sisi ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo. Ethiopia na Sudan, nikubali kabisa kwamba wenzetu utaratibu mzuri wanao wa matumizi bora ya ardhi. Botswana kila mfugaji sharti moja la kuwa na mifugo, ni lazima uwe na kisima uwe na *bore hole.* Nasi tufuate utaratibu ule kwa sababu ndugu zetu wanatangatanga kwa sababu wanatafuta maji, wanatafuta mbuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbuga hizo hizo tunataka kulima mpunga, mbuga hizo hizo tunataka kulima mahindi. Lakini sasa kama kwato za ng'ombe zitakwenda kwenye maeneo kama hayo; nimekaa Iringa nimeona Ihefu, Ihefu uharibifu ni mkubwa. Lakini hawa wafugaji wanapotangatanga, kwa nini tuwalaumu? Ni lazima tuwawekee mazingira, lazima tuwawekee miundombinu ambayo hawatakuwa na sababu ya kwenda kwa jirani yangu Ifakara, hawatakuwa na sababu ya kwenda Morogoro, hawatakuwa na sababu ya kuja Igalula kama maeneo yao kutakuwa na *bow holes* za kutosha, watakukwa na eneo la malisho, malisho ya kupanda, ambayo kiangazi watavuna kama ninavyoona malundo hayo ya nyasi za kula mifugo Wilaya ya Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya utunzaji wa mazingira ni muhimu sana. Wafugaji, wakulima lazima elimu hii iweze kuendelea. Ndugu zangu wengi wametoka Simiyu, wametoka Geita, wametoka Mwanza, wametoka Bariadi, wamekuja wote Igalula na mifugo, nami nawakaribisha.

Lakini Sasa mifugo inanilemea kwenye Jimbo la Igalula. Nitafanyaje na mimi ni mtu rahimu, mtu mkarimu? Lakini sasa mazingira yanaharibika. Wao wanasema lazima akikaa nyumbani kwake pale kilomita moja awaone ng'ombe wake wanavyokuja. Kwa hiyo, lazima akate miti kuangalia kule mbali. Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa sababu mimi nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, fedha hata zinazotolewa Sekretarieti za Mikoa kusimamia masuala ya mifugo, ni kidogo sana. Haiwezekani! naomba sana Bajeti iongezwe ili Wizara hii iweze kufanya kazi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la Kilolo. Kilolo nilikuwa *DC* Mawambala; kwa kutumia ufugaji wa kisasa, yuko ng'ombe ana tani moja; siyo ng'ombe mmoja, wako wengi; yako mashamba yale mazuri na kuna wafugaji wengine wanakuja kujifunza pale shamba la *ASAS* shamba la Philips na kule Mawambala. Tuwapeleke wafugaji wetu kwa utaratibu waende *NAIC (National Artificial Insemination Center)* kujifunza ufugaji bora ili tuwe na mifugo bora michache. Ng'ombe wachache lakini waonenepa vizuri. Kule ng'ombe mmoja ana kilo 1,000. Anatoa maziwa lita 35. Asubuhi lita 15, jioni amekula nyasi lita 20. Hili linawezekana! Tutumie wataalamu wetu wa ugani wa mifugo, wasikae maofisini, waende kila Kata, kila Kijiji wafanye kazi na wafugaji na hili tatizo litapunguza ile idadi ya mifugo kuwa mingi na tutaweza kupata tija kubwa katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembea, nilikwenda Thailand, sehemu zenye maji maji, sehemu zenye mabwawa, samaki wengi wanapatikana kutoka kwenye haya mabwawa. Sijaona jitihada kubwa kutoka kwenye Wizara katika kusaidia kilimo cha ufugaji wa samaki kwenye vijiji husika. Tupeleke ile mbegu ndogo ya wale samaki tuweze kufuga na hii itasaidia pia. Tusiendelee tu kuchoma nyavu, tuwawezeshe hawa wavuvi kuwapa nyenzo bora za kufuga na tuwape elimu. *(Makofi)*

Kuna wengine bahati mbaya wanavua samaki kwa *dynamites.* Yuko rafiki yangu mmoja karibu na *Sea Cliff* pale, kila siku akikaa kwenye *balcony* anaona bahari inalipuka puu hapo Dar es Salaam. Tuwe na watu ambao watadhibiti hawa watu kwa sababu wanaharibu mazalia ya samaki, wanaharibu mazingira yetu, lakini pia tuwawezeshe na pia tuwaelimishe. Tukikamata nyavu, tukizichoma, yule mtu tunampa elimu, kwamba wewe uvuaji wako utakuwa hivi na nyenzo ni hizi, sheria taratibu na kanuni zifuatwe kulinda mazingira ya bahari na raslimali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuongeze pesa Wizara hii ili iweze kutenda kazi zake kikamilifu. Kwa hayo machache naunga mkono hoja, kwa sababu nataka hawa wafanye kazi Mheshimiwa Dkt. David Mathayo na Naibu wake Mheshimiwa Ole-Nangoro na Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu, Prof. Makungu, wanaweza kazi hawa. Tuwaongezee pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mfutakamba kwa mchango wako na kwa kujali muda vizuri. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa, namwita mchangiaji anayefuata kama nilivyosema, namwita Mheshimiwa Kilufi - Mbunge wa Mbarali, lakini atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Mabumba Masele na atafuatiwa na Mheshimiwa Mkiwa Kiwanga.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii. Naomba nichukue nafasi hii kuwapa pole sana wafugaji wote waliopo katika nchi hii, kwa mazingira magumu ya ufugaji ambayo wanayapata na bado hakuna hatua yoyote ya msingi ambayo imechukuliwa kuhakikisha wafugaji hawa nao wanaishi kama Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ndiyo tegemeo letu sisi wote humu ndani. Hakuna mtu mwingine anayenda

buchani akauliza nyama kutoka labda kwa wanyama wa porini. Anauliza nyama ya ng'ombe, nyama ya mbuzi na nyama ya kondoo. Lakini huyu anayetufanya tupate kitoweo hicho ndio tumemwacha kama mtoto yatima. Hii haikubaliki kabisa. Lazima tufike mahali sasa tukubali kwamba uundwe mpango maalum, Wizara ijipange, iandae mkakati ambao utaonyesha namna gani tunawasaidia wafugaji waliopo katika nchi hii. Haiwezekani tukaendelea kuzungumza tu humu Bungeni, kila siku tunasema wafugaji wanateseka, wanateseka, lakini hakuna hatua ya msingi ambayo inaonekana katika kuondoa tatizo hili la wafugaji katika nchi hii. Wafugaji wanaishi kama wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya bidii sana kupanua hifadhi zetu za Taifa kwa maana ya wanyamapori, tunashindwaje kuweka eneo kwa ajili ya mifugo yetu ambao tunapata kitoweo kila siku? Mimi sijaridhika kabisa. Nadhani Wizara lazima iseme kitu, ilete mpango ambao tutaridhika kuona namna gani tunaweka mazingira mazuri ya ufugaji katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu sana, nchi hii wafugaji wakishirikishwa wana uwezo wa kushiriki kuchimba malambo. Wanao! Wanachongoja ni mpango tu wa Serikali. Hakuna mpango madhubuti unaoonesha ushirikishwaji kwa wafugaji katika kuondoa matati yao, haupo. Wafugaji ni kama hawana Wizara, afadhali hata ingebaki kama ilivyokuwa zamani. Kwa sababu gani? Tulitegemea Wizara hii ya Mifugo sasa itakuwa karibu kabisa na kuondoa matatizo ya wafugaji, lakini imekuwa ni kinyume kabisa. Wizara hii mimi nasema sitaunga mkono kama sitapata majibu ya msingi kuonyesha ni mpango gani mkakati umeandaliwa ili kuweka mazingira mazuri ya wafugaji katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mbarali, kwa bahati nzuri, nasema nzuri, tumesogelewa na Hifadhi. Tumekubali. Wananchi wameondoka, tumenusuru Ihefu, tumekubali. Lakini mpaka leo hii taabu wanayopata wafugaji wale haipimiki hata kwenye mizani. Kila siku kwa sababu mpaka haueleweki na mimi nimepiga kelele mpaka nimechoka,

jamani tuweke mpaka, wafugaji wanaumia, lakini mpaka sasa bado Wizara hainisaidii. Maana yake Wizara ya Maliasili na Utalii ina majukumu mengi, inawezekana, lakini ingepata nguvu hata ya Wizara husika kwa taabu wanayopata wafugaji kwenye mipaka, pengine ingewezekana hawa watu wa Hifadhi wakafanya utaratibu wa haraka wa kuona mipaka kwenye maeneo yanayopakana na wananchi inaandaliwa mapema ili wafugaji wasipate shida. Hakuna mpaka unaoonekana. Lakini mfugaji akikutwa pale, ng'ombe mmoja faini Sh. 25,000/=, ng'ombe mmoja Sh. 10,000/= wafugaji wanaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara haioni matatizo haya ikasimama na yenyewe? Kwa nini Wizara hii haioni kilio cha wafugaji? Kama haiwezekani, basi mimi niombe iundwe Kamati Maalum kwa ajili ya kuchunguza matatizo ya wafugaji. Vinginevyo, hawa wafugaji itafika mahali watakimbia nchi hii. Kama tunaweza kulipa fedha kuhamisha wananchi kwa ajili ya kupisha kupanua Hifadhi kwa ajili ya wanyamapori, tunashindwaje kufanya hivyo kwa ajili ya kutenga maeneo ya wafugaji? *(Makofi)*

Kwa nini tusiwashirikishe hawa wafugaji kwenye kuchimba malambo kwenye maeneo yao wakaona na wao wanawajibika kuchangia? Kwa nini mpango huo usije hapa? Sasa sisi kama Wabunge tunaiteteaje Wizara? Hakuna mpango mkakati unaoonekana kwa ajili ya kunusuru wafugaji, hatuuoni uko wapi? Kama kungekuwa na mpango, sisi tungesimama imara kuwasaidia. Tungesimama imara kuhakikisha Serikali inatoa bajeti kwa ajili ya kusaidia kuhakikisha mpango huu mkakati unatimia. Lakini sasa mimi sijaona jitihada kabisa. Watanisamehe. Kilio cha wafugaji katika nchi hii hakitakwenda hivi hivi, haiwezekani kabisa. Wananchi hawa wanapata mateso makubwa sana.

Ndugu zangu kama hamwamini, kama kuna matatizo ambayo ni sawa na maafa ni pamoja na kilio cha wafugaji katika nchi hii. Wanatozwa faini huko mipakani; tulikuwa na mashamba ya Taifa *NARCO*, tumewapa watu wanayachezea tu, hakuna kazi ya maana inayofanyika kule.

Naomba Wizara kuanzia sasa waache kubaki ofisini, wapite kwa wafugaji wakaone matatizo yao. Wapite wazunguke hii nchi waone matatizo ya wafugaji. Washirikiane nao waainishe maeneo ya kujenga malambo, wawashirikishe wale watachangia. Mifugo siyo kwamba ni bidhaa ambayo haiuziki, inawezekana kabisa! Nchi hii tunaonekana kama tuna ng'ombe wengi sana, lakini sisi siyo wa kwanza katika Bara la Afrika kuwa na mifugo mingi. Zipo nchi ambazo zina mifugo mingi, lakini hawapati taabu wafugaji wao kama sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kama sitapata majibu ya kuridhisha juu ya mipango kamili na thabiti kwa ajili ya kuboresha hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sitaunga mkono kuipitisha hoja ya Wizara hii. Sisi Wabunge tunaotoka maeneo ya wafugaji, adha ya wafugaji tunaijua. Taabu wanayoipata tunaifahamu. Wameshindwa tu kuja Bungeni kuandamana. Wengeweza, wangekuja hapa. Wangekuja kabisa, wangefika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni *serious.* Kama lilikuwa linachukuliwa kwa mzaha mzaha, naomba kuanzia sasa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tuungane, tuhakikishe tunawaokoa hawa wafugaji wetu. Haiwezekani wakapata taabu katika nchi hii, wakakaa kama wakimbizi na sisi viongozi wao tupo. Serikali ni ya kwetu, kwa nini isisikie? Kwanini tusiungane tukatenga maeneo ya wafugaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha wafugaji hakiwezi kwenda hivi hivi. Sisi tunaotoka maeneo, tuliojitoa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja baada ya maelekezo na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuona kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hiyo tayari ni kengele ya pili. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mchangiaji anayefuata. Nilisema atafuata Mheshimiwa Sylvester Masele na Mheshimiwa Mkiwa ajiandae. Naomba tena kuwakumbusha kutunza muda.

**MHE. SYLVESTER MABUMBA MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa muda huu niweze kuchangia hoja hii. Kwanza siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema siungi mkono hoja kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wabunge wa CCM watakumbuka tulipokutana na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama chetu alisema, fedha siyo tatizo. Kama unazo kazi ambazo zinaridhisha jamii na wananchi wa Tanzania, kama wewe huna uwezo wa kutafuta pesa, umwambie yeye atazitafuta pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo hii tunaposema bajeti ya Wizara ni ndogo, Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wameridhika. Hii inaonesha ni namna gani sio wazalendo, wananchi wetu wanateseka, wanaranda randa kila mahali, hakuna wa kuwatetea. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, ameorodhesha wahisani wengi *page* mbili. Hebu atuambie, katika sekta zote mbili; maana yeke yeye ana sekta zake kuu mbili, mifugo na uvuvi. Amewashajiisha namna gani ili waweze kuisaidia Wizara yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wahisani hawa tunategemeana sana na wao. Sasa kama wao wamekuja kumuunga mkono kwa kuorodhesha hapa wote kwamba wanashirikiana na yeye, ni fedha kiasi gani ambazo wamesaidia kwenye mifugo na kwenye uvuvi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mifugo, kwanza atusaidie, ameshirikiana vipi kutenga maeneo ambayo wafugaji watatumia kulisha wanyama wao? Lakini la pili,

amesaidia kiasi gani wafugaji ili wasihame hame, kuwa na mabwawa ya kutosha ili wanyama hao wapate maji, lakini vile vile kuwa na majosho ili wanyama hawa waepukane na maradhi? Lakini la tatu, ametuelezea hapa mamilioni ya wanyama tulio nao Tanzania. Hao wahisani ambao amewaorodhesha hapa, ni wangapi wamejitokeza kujenga viwanda vya kusindika mazao ya wanyama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wasemaji wote waliopita kwamba sekta hii imekosa wasimamizi. Tunahitaji kuhakikisha rasilimali ya wanyama inabadili maisha ya wafugaji na Tanzania kwa ujumla. Lakini hakuna ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kama kweli sisi ni wazalendo, na kama kweli Wizara hii haijaridhika na pesa ambazo imetengewa, na tuone Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wakisimama hapa kujiuzulu. Lakini kwa sababu wako kwa ajili ya mishahara yao, wafugaji na wavuvi sio kipaumbele kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwamba Tanzania inaagiza samaki. Nina taarifa hapa ya utafiti iliyofadhiliwa na *FAO* ya mwaka 2007 ambako inaonyesha wazi kwamba Tanzania inaagiza hata samaki, pamoja na ukweli kwamba tuna maziwa makubwa matatu Victoria, Tanganyika na Nyasa; tuna maziwa madogo Rukwa, Eyasi, Momera kule Arusha; lakini tuna ukanda mkuu wa Bahari na tuna mito mingi sana. Pamoja na yote hayo, bado tunaagiza samaki. Tunatumia zaidi ya bilioni kuagiza samaki. Ni aibu kwa Tanzania.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie ni mikakati gani wanaitumia hata kwa hao wavuvi kuwawezesha kuwa na zana za kileo siyo kwenda kuchukua nyavu na kuchoma moto. Mimi naomba maeneo ya wafugaji wote tuhamasishe wafugaji kama vile wanafunzi wanavyoandamana kwenda kumsumbua Waziri wetu wa Elimu na wafugaji waongoze ng'ombe wao wamfuate Waziri Ofisini kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo Waziri ataweza kuona uchungu wanaoupata watu hawa. Akienda tu na *Land Cruiser* lake, V8, na nini, V8 hili ni kwa sababu ya pesa za walipa kodi. Naomba sana Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji na wavuvi hawa kama tungewasaidia, hata maneno ambayo yanatoka hapa yasingetokea hapa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna hizi *Ranch* za Taifa ambako tumeambiwa hapa, atuambie, basi kutokana na *ranch* za Taifa hili ni viwanda vingapi ambavyo vimehamasishwa kujengwa au ambavyo sasa hivi tunavyo au ambavyo amefufua Mheshimiwa Waziri toka akalie nafasi ile kwa sababu kwa elimu hatuna hofu naye. Lakini kwenye uthubutu, tuna hofu. Kwenye uthubutu tuna hofu kwamba hawezi kuanzisha jambo hata moja ili watu wakajifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angeanza japo na Mikoa miwili tu ili baadae tuone sasa kwamba kuna haja ya kumsaidia Waziri apanue Mikoa mingine. Leo hii ni aibu kwamba tunakaa hapa tunaweka mikakati kwa ajili ya wanyama pori ambao kwa hakika wakati wa ukame kule Serengeti na Ngorongoro wanakwenda Kenya na kule Kenya kurudi kwao huku ni hiari yao, inakuwa ni mali ya Kenya. Lakini hawa wafugaji wenye ng'ombe tuna hakika ni mali ya Watanzania. Lakini kwa nini hatuweki mkakati kwa hawa wafugaji tuweka mikakati mikubwa kwa wanyamapori ambao wakati wa ukame kama ninavyosema wana-*migrate,* na waki-*migrate,* wengine wanauawa kule wanang'olewa meno yale yanauzwa na wengine ndiyo wananufaisha sekta za kiutalii katika nchi ambazo wana-*migrate.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwahurumie wafugaji. Lakini pia tunaposema tuhurumie wafugaji lazima tuisaidie Mikoa. Naomba Mheshimiwa Waziri akija kujumuisha aniambie ni lini alifanya mikutano na Wakuu wa Mikoa kuhamasisha namna gani wao kwa kuanzia watahudumia wafugaji? Kwa sababu, kama alivyosema Mheshimiwa Mfutakamba, tumekaa Kamati ya TAMISEMI, tumeangalia bajeti ile, lakini hatujaona wapi Mheshimiwa Waziri wa Mifugo

na Uvuvi amekuwa mkereketwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa. Zaidi sana wanahangaika sana wale. Tukikaa hapa tunasema Mkuu wa Mkoa fulani hafai, lakini kumbe kuna Wizara ambazo zingeweza kuwasaidia wakawa wanapunguza lawama hizi za kuhudumia wafugaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji hawa kwa upande mwingine ni kura za CCM. Lakini tunapodharau kura zile, itakula kwetu. Ni jambo dogo sana, wakiingia wenzetu wakawapa maneno ya matumaini, watatuasi sisi. Rafiki wa kweli ni yule anayeshughulikia kero zako. Maneno matupu hayavunji mfupa, kwa hiyo, watu watatukimbia. Mwaka 2015 haiko mbali. Naomba tuanze sasa, mna maneno matamu kweli! *Big Result Now! Big Result Now, how?* Sehemu kubwa ya wafugaji hatuwajali, hatuwasaidii na hata wavuvi wetu hatuwasaidii, rasilimali ya samaki inaporwa. Tuna udhibiti gani kwenye bahari kuu? Kama walivyosema wenzangu, hii *Exclusive Economic Zone* tunahudumia vipi? Tuna vyombo vingapi kwenda ku-*monitor* meli zinazokuja kule ndani? Hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanavua samaki wana-*dissapper Japan* wapi, baadae eti tuna *import* tani saba za samaki. *Shame on us*. Naomba tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema machache haya, naomba nisubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri, vinginevyo siungi mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Massele. Waheshimiwa Wabunge, naendelea na orodha yangu. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mkiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo, ajiandae.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai na nguvu kwa siku hii ya leo na mimi nikasimama kwenye Bunge lako hili, kuchangia Wizara iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema neno moja. Wizara hii nafikiri kama sijakosea, haijui nini inachokisimamia. Kwa nini nasema hivyo? Wavuvi wanapiga kelele, wafugaji wanapiga kelele. Sasa hivi ni kipi ambacho hasa kinasimamiwa kwenye Wizara hii ambacho kina uafadhali tukasema angalau huku kuna nafuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kidogo kuongelea wavuvi wa Ziwa Victoria. Hii ni mara ya pili kama siyo ya tatu nimesimama kwenye Bunge hili na kumwomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na TAMISEMI ili mvuvi anapoweza kukata leseni ya mwaka mmoja, leseni hiyo anapotoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine asiombwe tena mchango unaozidi laki, laki na kitu, kwa sababu Ziwa ni hilo hilo la Victoria. Wakati anaweza akatoka Wilaya ya Ilemela akaenda Wilaya ya Ukerewe akaombwa tena fedha nyingine. Lakini upande wa magari, ukishalipia tu kodi utatembea Tanzania nzima, hakuna mtu atakuuliza wewe umelipia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii inawakwaza wavuvi na kama Halmashauri wanategemea wavuvi ndiyo waweze kuchangia katika mapato ya Halmashauri, tunawaumiza wavuvi na hasa ukizingatia wavuvi hawa wanavua kizamani, hamna mtu anawawezesha, hawana elimu, hawana mikopo, lakini wanachangia pato la Taifa kwa akili zao wenyewe bila kusaidiwa na mtu yoyote. Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi ninakuomba kaa na Wizara ya TAMISEMI, kama ni kiwango cha kulipia leseni, kiwe kiwango kimoja, ilimradi mtu akishalipa aweze kuvua ndani ya Ziwa Victoria bila kikwazo chochote. Wavuvi hawa wanaumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wa Ziwa Victoria kwanza bado wana vua kizamani lakini wanachangia pato la Taifa. Tunaambiwa katika pato la Taifa uvuvi unachangia 1.4% lakini zaidi ya 60% zinatoka Ziwa Victoria. Zinapotoka Ziwa Victoria, tunaposema kwamba kazi yetu sasa Wizara ya uvuvi imekuwa ni kukamata nyavu na kuchoma. Tunaomba nyavu mlizoshika madukani hazitoshi mkakague magodauni, mkakague maduka na nyavu za milimita sita

zinauzwa dukani, lakini zikiwa dukani siyo haramu, haramu tu zikishaingia kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba sasa mkakague godauni zote nyavu zinazotengenezwa nchini, nyavu zinazotoka nje ya nchi kwa sababu zinalipiwa na *VAT* kwa sababu Serikali inapata fedha, ili mweze kuanzia hapo nafikiri wavuvi wakikosa hizo nyavu haramu hawataweza kuchukua nyavu haramu wakaingiza ndani ya maji. Isiwe ikiingia ndani ya maji haramu, ikiwa dukani ni halali na pia kodi mnataka, ushuru mnachukua; hivi huyu mvuvi akimbilie wapi? Hana pa kukimbilia, tunawaomba sasa mkae chini, Wizara yako, Wizara ya TAMISEMI mwambizane, muweze kuwahurumia wavuvi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema kwamba kuna doria, hakuna doria inayofanywa kwenye Ziwa Victoria. Wavuvi wanavamiwa na majambazi, wanaibiwa mashine zao, wavuvi wanakaa visiwani; siku moja naomba Mheshimiwa Mathayo aje tumpeleke Bezi, tumpeleke visiwa vya mbali ili akaone ni namna gani wavuvi wanapata matatizo na siyo awe anakuja anaishia nchi kavu.

Sasa tunaomba aje tuvuke wote na mitumbwi akaone wavuvi wanavyopata shida, michango wanayochangishwa lakini hakuna huduma yoyote inayoendelea ya kijamii kwenye maeneo hayo. Hata mwanamke akitaka kujifungua usiku inakuwa tatizo, mpaka avushwe kwa mtumbwi apalekwe nchi kavu. Tunaomba sasa asiishie nchi kavu. Aje apande mitumbwi wanayopanda wavuvi kwa sababu ndiyo watu wake alionao kwenye Wizara yake ili aweze kuwasemea na aweze kuona matatizo waliyonayo, huenda na yeye akapatwa na huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nichangie kidogo uvuvi wa bahari kuu. Uvuvi wa bahari kuu mwaka 2009 ulipewa mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu, lakini tangu 2009 Mheshimiwa Waziri upewe Mamlaka hiyo mpaka leo hujapewa kibali cha kuajiri wafanyakazi wa mamlaka hiyo. Wamekuwa na wafanyakazi wa kuazima tu katika Vitengo

vya uvuvi. Kuna tatizo gani, mnashindwa kuipa hii mamlaka mliyoiteua kibali cha kuajiri wafanyakazi ili waweze kufanya kazi zao kwa uhakika? Wamebakia na wafanyakazi watano, tena wafanyakazi wenyewe wa kuazima! Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanaazima na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Wafanyakazi wenyewe ni watano, hivi wanafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Mathayo utakapokuja uniambie, ni kwa nini hutoi vibali vya hawa, ukawapa hii mamlaka ikaweza kuajiri wafanyakazi wakaweza kuendeleza uvuvi katika bahari kuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, katika bahari kuu kuna Sheria ambayo inasajili meli za kigeni. Baada ya kusajili inabidi itakapoingia kuvua lazima irudi kwenye bandari ili ikaguliwe imevuna kiasi gani. Iende aidha bandari ya Zanzibar, iende bandari ya Dar es Salaam, Mtwara au Tanga. Sheria hii ina vifungu vyake.

Kama meli iliyopewa leseni haikufanya hivyo, inatakiwa mwenye meli huyo atozwe Shilingi bilioni moja ama afungwe miaka 20 kwa kukiuka Sheria hiyo. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametuambia ndiyo wanaanza sasa kuja kukaguliwa, ndiyo wanaanza. Hiyo miaka yote mliyokuwa mnasajili ukija hapa utuambie ni meli ngapi zimepigwa faini ya Shilingi bilioni moja na ni wamiliki wa meli ngapi wamefungwa miaka isiyopongua 20, au mambo yote mawili kwa pamoja? Uje utuambie kwa sababu hii inatukosesha Tanzania mapato, wavuvi hawa wanakuja, Sheria zipo Wizara mnashindwa kusimamia Sheria. Mtuambie mna njama gani za kushindwa kusimamia Sheria zilizotungwa na sisi wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 59 Mheshimiwa Waziri amesema wanafanya doria. Wana ndege inafanya doria kwa masaa 180. Lakini doria hii inayofanywa kwa masaa 180 kwa utafiti wangu, saa moja ya ndege hiyo wanalipa dola 2,000 kwa saa moja, tuzidishe mara 180 ili tujue ni Shilingi ngapi Serikali inapata hasara. Siyo chini ya Shilingi milioni mia tano sabini na kitu, Serikali inaingia hasara, tena

ukaguzi huo unafanyika usiku, wakati usiku meli hiyo hata kama itaonwa na hiyo ndege, siyo rahisi kuikamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali itafute mbinu nyingine ya kuweza kukamata hawa wavuvi haramu ni wengi ambao wanakuwa kwenye bahari kuu, lakini hawawezi kuvua bila kukaguliwa na bila kutozwa *fine.* Hii yote inaendana na sisi wenyewe kuwa wazembe, kushindwa kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwenye mifugo kidogo. Mheshimiwa Waziri amekuja hapa akatutolea takwimu za mifugo. Mimi naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri hivi, sensa ya mifugo Wizarani kwako mara ya mwisho umeifanya lini? Utakapokuja utuambie sensa ya mifugo Wizarani kwako kwa mara ya mwisho imefanyika lini? Kwa kumbukumbu zangu ni miaka 20 iliyopita. Sheria inasema sensa inatakiwa ifanywe kila baada ya miaka kumi ya mifugo, lakini wewe kila siku ukija unakuja na takwimu; takwimu hizi unazokuja nazo zisizokuwa na uhakika ndizo hizi zinashindwa kujua tuna mifugo kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifugo Mheshimiwa Waziri ajue iko chini yake. Wavuvi wanaonewa, wavuvi wananyanyaswa, wavuvi wanauliwa kwa haki zao. Yeye kama Waziri wa Mifugo anawatetea vipi wavuvi hawa? Anajua. Kuna Wakuu wa Wilaya wanachukua mamilioni kwa wavuvi. Je, hujui? Kama unajua, umechukua hatua gani kwa wafugaji hawa? Mimi mwenyewe nimeshuhudia mfugaji amekamatiwa ng'ombe 75, anapewa risiti ya ng'ombe watano. Ng'ombe wengine wote wanakwenda bure, Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Wilaya wanachukua fedha, wanawachukulia Wasukuma ng'ombe zao. Kwani Wasukuma wana makosa gani hapa duniani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, mnasema wavune mifugo, mwatafutie njia ya kuvuna mifugo, siyo umwambie mtu tu vuna mfugo, hajui apeleke wapi. Ahsante. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mkiwa, kengele hiyo ni ya pili. Nakushukuru sana. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Diana, naona hayupo. Basi naomba nimwite Mheshimiwa Opulukwa, halafu Mheshimiwa Pamba ajiandae.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nisisahau, kwanza siungi mkono hoja. Nilikuwa naangalia kitabu cha bajeti *Volume IV* kwenye ile *vote* namba 99, wakati naangalia hiki kitabu nikadhani kwamba nilikuwa nasoma matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2012 kabla ya kufanyiwa marekebisho, kwa sababu nilikuwa naona *zero* ni nyingi sana. Nikaangalia *vote, subvote* 4486 *zero* kila mahali sifuri, sifuri nikafananisha hizi na *division four* ambazo zilifanyiwa marekebisho juzi na leo hii matokeo yameweza kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama bajeti hii haitaongezwa na kama zile fedha ambazo Kamati imeomba kwamba ziongezwe kwenye Wizara hii ili angalau kazi ziende; kama hazitakwenda sitaunga mkono kabisa hoja hii. Lakini siyo kuunga mkono tu hoja hii, lakini hata kama fedha zitaongezwa ili niweze kuunga mkono, lazima sasa niweze kuona maeneo ambayo yamesahaulika kwenye Jimbo la Meatu, Jimbo ninalotoka mimi hakuna majosho, hakuna mabwawa, ukienda kule Ng'wangundo, Bukundi, Mwabuzo, Mwamalole, Mwamanimba, Nkoma, hawa watu wanahitaji maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naunga mkono hoja hii namna gani wakati ambapo kwenye Jimbo langu na kwenye Wilaya yangu hawa watu bado hawajasikilizwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu ndiyo Serikali iliyopo madarakani. Sera ya Chama cha Mapinduzi wanasema ni kupunguza mifugo kwa sababu mifugo inaharibu mazingira.

Sisi kwetu wafugaji na hasa ukienda Meatu na ukienda Simiyu, ukienda Shinyanga, ng'ombe ndiyo benki yetu. Ni sawa na Mbunge mwingine au mtu mwingine yeyote anachukua fedha zake anapeleka benki kwa ajili ya kwenda kujihifadhi pale. Sisi benki yetu ni ng'ombe. Unapokuwa na ng'ombe utauza ng'ombe utapeleka mtoto shule atasoma; unapokuwa na ng'ombe utauza utapata fedha utajenga nyumba ya bati; unapouza ng'ombe utapata pesa utapeleka mtoto hospitali atatibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaambiwa punguza ng'ombe. Mimi naomba hii sera ya Serikali kwa kweli badala ya kupunguza ng'ombe, iwe ni kuongeza ng'ombe na wala siyo kupunguza ng'ombe. Wakati nasoma kitabu cha hotuba ya Mheshimwia Waziri kuna sehemu inasema Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu kidogo. Inasema: "Sekta ya Mifugo ni moja kati ya sekta zilizopewa umuhimu katika kutekeleza mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini". Inasema, mifugo inatoa ajira. Kama tunapunguza mifugo, ajira itapatikana wapi? Watoto watakwenda kuchunga ng'ombe wapi? Hii ni ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama nina mifugo yangu itachungwa na nani kwa sababu tunaamini kwamba ajira siyo ajira ya kukaa darasani, siyo *white collar job* peke yake! Ajira ziko nyingi, lakini tunawaambia leo watu wapunguze mifugo, wapunguze ng'ombe waendelee kuwa masikini, waendelee kutawaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema ili tuweze kuwatendea haki Watanzania wengi ambao ni wafugaji, wanaotoka maeneo ya wafugaji, ni lazima bajeti hii iweze kuongezwa kama ambavyo Kamati imependekeza lakini pia

lazima Meatu ikumbukwe kwenye mambo ambayo hayako katika kitabu cha bajeti cha Mheshimiwa Waziri ili angalau tuweze kwenda sambamba pamoja na Wabunge wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea kwamba katika kitabu cha bajeti hii kwenye ule ukurasa wa 85 Mheshimiwa Waziri ame-*indicate* kwamba Meatu imetengewa hekta 11,000 kwa ajili ya wafugaji peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Meatu na nahudhuria pia vikao vya Baraza la Madiwani, hizi hekta 11,000 hazipo! Kama zipo, ziko wapi? Kama zipo labda zipo heka mbili au tatu, ndiyo maana wafugaji wa Meatu, wafugaji wa Simiyu, wafugaji wa Bariadi wanahama kila siku wako Sumbawanga, wako Mbeya, wako Rufiji, wako Morogoro kwa sababu hakuna maeneo ya kulisha mifugo yao. Nilikuwa naomba sasa ili angalau wananchi hawa, ili angalau haya maeneo anayosema hekta 11,000 kwamba zipo, Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili kuisha uende Meatu ukajiridhishe na hizi hekta 11,000 zinazoelezwa. Nadhani Watendaji wako ndio wamekuandikia hotuba hii, lakini wewe bila kufuatilia wala kuangalia, ukaitoa kama ilivyo. Hakuna hekta 11,000 kwa Meatu na ndiyo maana wananchi wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi huwa sipendi kupigiwa kengele. Napenda kusema neno la mwisho. Watanzania wengi, wananchi wengi na karibia dunia nzima wanapenda nyama na hasa nyama ya ng'ombe na nyama ya mbuzi. Ukienda kwenye ma-*deep frezers* ya watu mbalimbali na Mawaziri wetu akiwemo na wewe labda Mheshimiwa Mwenyekiti ukiwemo utakuta friji imejaa nyama, lakini cha ajabu hawa mifugo, hawa ng'ombe hii nyama ndiyo inapigiwa vita kila siku watu wapunguze ng'ombe. Nilikuwa naomba, hebu tuwajali watu hawa, wameteseka kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana mkono na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamesema hawaungi mkono hoja hii. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Opulukwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Saleh A. Pamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi, na kama muda utatosha, namwona Mheshimiwa Diana Chilolo amerejea, nadhani alikuwa na udhuru. Basi tutaona.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ambayo sikuitegemea. Awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja. Naunga mkono hoja kwa sababu Wabunge wote waliozungumza kuanzia asubuhi, wamezungumzia juu ya suala la bajeti ndogo ya Wizara hii. Serikali yetu ni sikivu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, inasikia kilio cha wananchi wake, inasikia kilio cha wafugaji, inasikia kilio cha wavuvi. Nina uhakika kabisa kwamba Serikali yetu sikivu itaongeza bajeti hii ili Mheshimiwa Waziri aweze kufanya kazi yeke vizuri. Ninaamini kabisa bila wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza pale ambapo amemalizia Mheshimiwa Kitandula. Mheshimiwa Kitandula alizungumzia juu ya masuala na takwimu na Taarifa ya Uvuvi Duniani iliyotolewa na *FAO* mwaka 2012. Alizungumzia juu ya takwimu zile ambazo sitaki kuzirudia, lakini nataka nizungumzie kitu kimoja kikubwa kabisa ambacho amekizungumzia, nalo ni suala la ufugaji wa samaki. *(Makofi)*

Ufugaji wa Samaki katika takwimu alizozungumzia unachangia takribani nusu ya samaki wote wanaouzwa duniani. Ufugaji huu unachangia fedha karibu dola bilioni 119. Sasa nataka kuiangalia nchi yetu tuko wapi, hasa katika ufugaji wa samaki? Hasa nataka kuangalia nchi za Kiafrika, ili niweze kuleta msisitizo kwa Wizara hii kwamba suala la ufugaji wa samaki ni muhimu sana na lazima lifanyiwe kazi na lazima liwe katika mipango. *(Makofi)*

Katika nchi kumi zinazofuga samaki, au zinazoongoza kwa ufugaji Afrika, ya kwanza ni Misri, inazalisha tani 900,000;

ya pili, Nigeria, inazalisha tani 200,535; ya tatu, Uganda, tani 12,000; Zambia, tani 10,000, Ghana, tani 10,000; Madgascar, tani 6,000; Tunisia tani elfu 5,000; Malawi, tani 3,000; nyingine zote za Kiafrika ni tani 21,000 pamoja na Tanzania. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba, Tanzania nchi iliyo na maziwa makuu matatu; Victoria, Nyasa na Tanganyika; Mito, Maziwa madogo madogo, hatujafanya jitiada za kutosha katika sekta hii. Naoimba Wizara katika mipango yake, ihakikishe kwamba, suala la ufugaji wa samaki, ambalo ni suala muhimu linalo-*contribute* takribani asilimia 50 ya samaki zote duniani, wanatokana na ufugaji. Suala hili lazima walitilie mkazo katika mipango yao yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie haraka haraka katika eneo la uvuvi wa bahari kuu. Tumeanzisha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari kuu mwaka 2009. Mamlaka hii inafanya kazi kwa matatizo kama Wabunge wengi walivyo zungumzia. Haina meli ya doria. Nadhani bajeti hiyo itakayoongezwa, naiomba Wizara, kwamba kitu cha kwanza cha kufanya ni lazima wanunue meli ya doria, ili kusudi waweze kupambana na majangili walioko katika bahari kuu. Kwa sababu tunapoteza fedha nyingi sana, dola 1,900,000 zinazotolewa na leseni tu, hazitoshi hata kidogo! Tunapoteza takribani dola zaidi ya bilioni 100, kutokana na samaki wetu wanaovuliwa katika bahari kuu, ambao tunashindwa kukamata Meli hizi, na tunashindwa kupata *royalty* katika meli hizi.

Kwa hiyo, bajeti hiyo itakayoongezwa, naamini kabisa Serikali itaongeza bajeti hii. Fedha hizo suala la kwanza ambalo Wizara hii lazima ifanye, ni lazima inunue meli kubwa ya kupambana na majagili baharini, ili kusudi tuweze kupata fedha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende haraka haraka kwenye suala la wavuvi wadogo wadogo. Katika mikakati ya Wizara, na nimesoma bajeti ya Mheshimiwa Waziri, sijaona mkakati hasa wa kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo. Badala yake, Wavuvi wadogo wadogo katika nchi yetu, maeneo mbalimbali, pamoja na wavuvi wa Pangani,

hawapati misaada ya kutosha kutoka Serikalini. Wenzetu wa Wizara wanachofanya ni doria, kukamata nyavu na kadhalika. Kama mvuvi mdogo mdogo hujampa nyavu ya kisasa, unafikiri afanye nini? Sasa nataka nitoe pendekezo kwamba, ili tuweze kufaidika na wavuvi wadogo wadogo, na ili tuweze kuwasaidia, tufanye kama walivyofanya katika Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo wana kitu wanakiita Mfuko wa Pembejeo, *Agricultural Inputs Fund*. Ule mfuko wavuvi wanakwenda kukopa, wanapata mikopo nafuu, wanalipa kwa muda mrefu, ili kusudi waweze kupata vifaa vya kisasa. Haisaidii kuchoma nyavu za wavuvi wadogo wadogo, huko ni kuwaonea kama hukuwapa uwezo wa kuweza kupata zana na boti za kisasa na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwamba hili uliweke katika mipango yako, na fedha utakazopata za nyongeza, uanzishe mara moja Mfuko wa Wavuvi Wadogo Wadogo ili waweze kupata fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka kuzungumzia, Mheshimiwa Waziri mwaka 2012 ulituahidi kwamba utatusaidia katika Wilaya ya Pangani kwamba utatupatia Kituo cha Mitamba, Kituo cha ng'ombe bora. Hilo halijafanyika. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Pangani sasa hivi ni wafugaji wazuri, wanafuga kisasa, wanapata kila mwezi karibu Shilingi milioni 150 zinazoingia mfukoni kwa wafugaji wadogo wadogo, lakini tunahitaji kituo hiki ili kusudi tuweze kupata mitamba ambayo itatusaidia kupata ng'ombe bora na kuongeza uzalishaji wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala la kutunza mazingira. Uvuvi haramu unaendelea, uvuvi haramu katika mito, uvuvi haramu katika maziwa; lazima Wizara itenge fedha za kutosha za kuhakikisha kwamba, wanapambana na waharibifu wa mazingira. Kwa sababu samaki hawa, ni *renewable resource*. Kama tukiwatunza vizuri, tutaendelea kupata samaki wengi zaidi. Kwa hiyo, suala la

kutunza mazingira ni eneo mojawapo ambalo nafikiri ni muhimu sana ili kusudi uvuvi wetu wa baharini, katika maziwa, katika mito, na maeneo yote mengine, unakuwa endelevu.

Naomba Mheshimiwa Waziri kwa kumalizia, niseme kwamba, ninaamini kabisa kwamba Wizara hii ina mipango mizuri, mimi mwenyewe nimeiona mipango hiyo katika *fisheries masterplan* ambayo wameitengeneza, nimeona mipango hiyo mizuri katika *livestock development program*, haya yote ya majosho, kupanga maeneo mbalimbali ya wafugaji na wakulima na kadhalika yote yanawezekana. Naomba Wabunge wenzangu, tuisaidie Wizara, waweze kwa kuanzia angalau hiyo Shilingi bilioni 40 ambayo wameiomba, waweze kuendelea na mpango wao huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Makilagi!

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika sekta hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu na Sekta ya Uvuvi na Mifugo, Sekta ambayo kama tutaijengea miundombinu mizuri ya kutosha, inaweza kuchangia pato la Taifa na tukaondokana na tatizo la kuwa ombaomba; Tukaondokana na tatizo la kutegemea wafanyabiashara wachache ndiyo walipe kodi na tuendeshe nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niunge mkono bajeti hii asilimia mia moja, kwa sababu mimi ni mdau ya Kamati hii ya Mifugo na Uvuvi na naomba niunge mkono kabisa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kuunga mkono, naomba sasa na mimi niungane na wenzangu wote waliosema kwamba bajeti ya Wizara hii kwa kweli ni ndogo. Ni ndogo ukilinganisha na mahitaji ya Wizara hii, ukilinganisha umuhimu wa sekta hii na ukilinganisha hata na ukubwa wa

Wizara yenyewe. Mimi kusema ukweli, nimefuatilia michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi. Nilivyokuwa naitazama, wengi wanafikiri pengine Mheshimiwa Waziri, watendaji wake, siyo wa kiwango cha kuridhisha, pengine Katibu Mkuu na Watendaji wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenzenu nipo kwenye Kamati. Naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuwapongeze hawa Watendaji wetu; Mheshimwia Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa kufanya kazi katika mazingira magumu. Nafikiri ni ukweli usiopingika kwamba wote tumeiangalia bajeti hii. Hivi wangefanya nini, asilimia 56 ya fedha walizozipata katika fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hivi wangefanya nini katika fedha za maendeleo? Kiasi walichopata ni asilimi 36 tu! *(Makofi)*

Kusema ukweli, hata kama wangekuwa na miujiza ya namna gani, wasingeweza ku-*perform* vizuri. Mimi nilikuwa naomba niwashawishi Wabunge wenzangu, tuwapongeze hawa Watendaji wetu na Viongozi wetu kwa kazi kubwa na ngumu wanayoifanya katika mazingira magumu sana, kwa kweli ya kupigiwa mfano. Wangekuwa kama sio watu makini, ingekuwa Wizara imeshaanguka kabisa kutokana na hali ninavyoiona hapa. Kwa sababu wako makini, wanachokipata wanakitumia; tena nataka niwaambie hawa Watendaji wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni Watendaji ambao wana wito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa nakutana nao, huwa nawaona jinsi ambavyo wana uchungu; unawaona jinsi ambavyo wanataka kushuka huku vijijini wakafanye kazi; unaona jinsi ambavyo wana hamu ya kwenda kujenga malambo kwa ajili ya wafugaji; lakini ukija kwenye bajeti, hawapati kitu. Kwa kweli wanashindwa kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hebu tuwatie moyo hawa Watendaji wetu, tuwasaidie kama ambavyo mmesema hapa. Serikali sasa isikie kilio cha Watendaji, isikie kilio ha Kamati, ichukue

maoni yote ya Kamati kama ambavyo tumeyaleta hapa, tupewe Shilingi bilioni 40 na nawaomba wenzangu waliochangia hapa, hata ikiwezekana zaidi kama walivyoziomba zote, ili sasa wakirudi waweze kutenda kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sasa migogoro ya wakulima na wafugaji. Jambo hili la migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kweli limekuwa ni jambo sugu, jambo ambalo kila tunapokutana hapa, linajirudia, lakini kwa kweli hatujaona hatua za makusudi za hizi Wizara mtambuka. Kamati ya Mifugo tumejieleza vizuri, kwamba jambo hili la kupima ardhi kwa ajili ya wafugaji; jambo la kupima ardhi kwa ajili ya wakulima, huwezi ukaachia Sekta ya Mifugo peke yake. TAMISEMI wako wapi? *(Makofi)*

Maana ukisema pia TAMISEMI unaachia Halmashauri peke yake, kuna Halmashauri nyingine hapa nchini, hali ya uchumi wao ni mdogo. Kuna migogoro pale niliwahi kusema Bunge lilopita, kwamba pale Rufiji na maeneo mengine, huwezi ukasema Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, kwa mapato yake peke yake au Kisarawe au maeneo mengine wao ndiyo watenge maeneo ya wakulima, watengeneze bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza kwenye Bunge lilopita na hapa ninarudia; na kwenye Sekta ya Ardhi nimesema na hapa tena narudia kwa mara nyingine. Hebu Serikali itafute fedha popote, ipeleke kwenye Halmashauri zetu, kwa ajili ya kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji ili kuondoa hii migogoro inayotokea mara kwa mara na kuleta maafa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na katika Kamati yetu hapa tumetoa ushauri, huoni kabisa mkakati wa kupunguza hii migogoro. Wafugaji wa Mwanza, wafugaji wa Geita, Wafugaji wa Shinyanga, na hata Mara na wote hawa niliowataja, utawaambiaje akae pale, hakuna lambo? Atakaa pale namna gani, hakuna majosho? Hakuna madawa! Wanahamahama kwa sababu ya haya matatizo yaliyopo.

Tunaiomba Serikali kusema ukweli ijitahidi kadri inavyowezekana, kama ambavyo Kamati ya Kilimo na Uvuvi imeshauri, Serikali itafute fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mifugo, ili wafugaji waendelee kukaa katika maeneo waliyopo, waachane na hii tabia ya kuhamahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara ni miongoni mwa Mikoa ya wafugaji, ambao sio wa kuhamahama. Lakini wale wa Mkoa wa Mara wanafanya uvumilivu kwa sababu wakati mwingine wanawakimbiza mtoni, wakati mwingine kuna vijilambo. Kadri hali ninavyoiona na wenyewe wataanza kuhamahama. Sasa hivi mnazungumzia Wasukuma wanahama, wanatembea, sasa wanakuja na Wakurya, wanakuja na Wajaluo, tutakwenda wapi? Wajita nao wanakuja sasa, maana hata kule mifugo imeshakuwa mingi, hawana elimu ya kufuga mifugo ya kisasa, hawana malambo na majasho, na wao wanataka kuhama kwa ajili ya kwenda maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana, hebu tupeleke hii elimu ya ufugaji. Tujitahidi sasa kupeleka elimu hii ya ufugaji kwa Tanzania nzima na Serikali itafute fedha za kutosha kwenda kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano, Mkoa wa Pwani, Mtwara, Tanga na hata kule Katavi na Rukwa walikohamia wafugaji, wale utamaduni wao haukuwa wa kufuga. Leo mmekwenda kuwachanganya na wafugaji, hakuna elimu yoyote, matokeo yake sasa Wazaramo na Wakwere wanaona kama siyo wenzao na migogoro ndiyo inapoanzia. Hivi hii elimu niliyoidai mwaka 2012, mmeshapeleka wapi? Je, kuna mkakati gani? Nilikuwa naiomba Serikali itutafute fedha kwa ajili ya kwenda kuelimisha watu wetu, ili migogoro hii iweze kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kusema kwamba, Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa kweli ni sekta muhimu

sana. Kama tutawekeza kama wenzetu wa Kenya hapa jirani walivyofanya; wenzetu Wakenya, wamejielekeza katika suala zima la kuchimba malambo, wakawapatia vijana, hawa waliotoka Vyuo Vikuu wako mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea na mtu mmoja mvuvi hapo Kibaha, ananiambia mama, mimi katika miezi sita, nina uhakika wa kupata Shilingi milioni 60, bwawa dogo kabisa, nilishangaa. Akanihamasisha! Hivi kama tungetenga fedha kwa ajili ya kuchimba mabwawa tukawasaidia kuwapa vijana wetu, vikundi vya akina mama na vijana, wakaendelea kufuga samaki za kutosha, soko lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwa kweli tutapata ajira, pato la Taifa litaongezeka na hawa wanawake na vijana wataondoka katika suala zima la umasikini. Nilikuwa naiomba Serikali kwa kweli ijielekeze kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga haya malambo, ili kuwapataia vijana na wanawake ili kuimarisha uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la uimalishaji wa Sekta ya Viwanda ya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi. Mimi kwanza nilipenda Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akifanya majumuisho, atupe tena maelezo kwa pamoja kama ulivyotueleza kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi huu mkakati wa kufufua viwanda vya maziwa uko wapi? Umepotelea wapi? Kiwanda kiko kule Musoma, tunashukuru kwa jitihada zinazoendelea juzi nimeona kwenye Kamati na hapa taarifa inaonyesha. Vile vichache vichache havitoshi! Nilikuwa naiomba Serikali itafute fedha nyingi kabisa kwenye mabenki, iwakopeshe wazalendo wa Tanzania, walio tayari kujenga viwanda katika nchi yetu, kwa ajili ya kusindika mazao ya samaki, mazao ya mifugo ili kuleta tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunaona shida gani, kuchukua benki ya *CRDB*, tukatenga hata Shilingi bilioni mbili, tukawatafuta Wazalendo hata watatu, tukawakabidhi, hebu

kajenge kiwanda kule Mara, hebu kajenge kiwanda kule Singida kwa ajili ya kusindika mazao ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri tukifanya hivyo, na wenzetu ndivyo walivyofanya. Tusikae kutegemea hawa wafanyabiashara. Kila mtu ajihamasishe, suala la kujenga viwanda linahitaji fedha, linahitaji ujasiri, ni lazima Serikali iwawezeshe ili kuleta tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la wafanyakazi wetu katika sekta hii muhimu sana. Kama mlivyoona kwenye taarifa na hata kama Kamati ambavyo tumesema hapa, katika Wagani nchi nzima ni zaidi ya 17,000 na tulionao ni 5,000 tu. Lakini tunapombana Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati mara atuambie TAMISEMI, mara atuambie Utumishi, hana Mamlaka yoyote. Anasema ameshapeleka barua huko, hajapata majibu. Mimi nataka wakati mnafanya majumuisho, kama ni TAMISEMI watuambie, upo mkakati gani wa kuajiri wagani?

Kama ni suala la Utumishi, watuambie. Katika huu mpango mzuri alikokuja nao Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Utumishi, watueleze, katika ajira zitakazotengenezwa mwaka huu, Wagani wangapi ni wa Mifugo, na Wagani wangapi ni wa uvuvi? Kwa sababu, bila hawa wataalam itakuwa sawa sawa na kutwanga maji kwenye kinu. Nilikuwa naiomba sana Serikali hebu ijielekeze kutafuta fedha kwa ajili ya kuajiri Wagani wa kutosha na hili jambo libaki kuwa historia. Haiwezekani kila wakati tunapokuja tatizo ni la Wagani, tatizo ni la Wagani linajirudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Uimarishaji wa sekta ya ....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni kengele ya kwanza hiyo.

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Amina Makilagi kwa kukubushwa na kukumbuka muda umepita. Mheshimiwa Diana kwa dakika tatu nne.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu.

Kabla sijatoa mawazo yangu, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote waliotangulia kwamba, bajeti ya Wizara ya Uvuvi na Mifugo ni ndogo. Jamani naiomba Serikali iwe inaangalia maeneo ambayo yanagusa Watanzania walio wengi moja kwa moja. Hatuna ujanja na wafugaji, hatuna ujanja na wavuvi, hatuna ujanja na wakulima, lazima tuangalie maeneo haya. Tutaendelea kugombana na Watanzania mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba, nilimwona Naibu Waziri alikuja kunong'ona na Waziri pale, ninaamini kuna kapu la hela labda amepeleka. Mimi nashanga Mheshimiwa Rose Kamili ulikuwa unagomba bure, pale kuna hela imekwenda. Naomba kesho Mheshimiwa Waziri atuambie ameongezewa Shilingi ngapi, ili wavuvi, wafugaji wafurahi, na waweze kufanya kazi vizuri kwa sababu watakuwa na uwezesho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Kiwanda changu cha Singida cha kusindika maziwa. Tuna kiwanda kidogo cha kusindika maziwa Singida katika Kijiji cha Msepuka Wilaya ya Ikungi. Mheshimiwa Waziri, ndani ya bajeti hii, tembelea kiwanda hiki kidogo. Kiwanda hakina miundombinu, hakina wataalam, kina mazingira magumu na kinahitaji uwezesho. Nakuomba utembelee Singida na mimi unichukue nikusindikize uende uone hali halisi ya kiwanda hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kiwanda hicho tu, pale Msunguwa, Tarafa ya Isepuka, tuna kiwanda cha kuwamba ngozi. Kiwanda hicho nacho hivyo hivyo ni duni kabisa, hakina wataalam, hakina miundombinu, yaani kinahitaji uwezesho. Tena vinakaa eneo moja kama Bunge hili hapa. Ninakuomba uondoke uende uvione hivi viwanda, tunatakiwa kuvinusuru, kwa sababu tayari Halmashauri na Wilaya ilishawekeza pale, na Mkoa umetazama pale, ninaomba na Serikali itazame pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la kuku. Jamani Tanzania nzima tunalisha kuku watu wana-Singida. Kuku wanapitishwa hapa wamening'inizwa bila huruma. Kwa nini tunawatesa namna hiyo? Tuangalie mazingira ya kuwabeba kuku, na ikiwezekana kuku hawa, tutengeneze kiwanda cha kusindika nyama za kuku Singida. Tuache tabia ya kuwatesa hawa ndege wadogo, nao pia wanahitaji kulindwa. Tutengeneze kiwanda Singida, tusindike nyama za kuku, tusindike nyama nchi nzima, tusambaze nchi nzima, watu wale kuku, kuku wa asili ambao hawana maradhi wala tatizo lolote la kumdhuru binadamu, siyo sawa na kuku wa kisasa ambao wanatumia madawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, Mheshimiwa Waziri asikie ombi langu la wana-Singida kuhusu kuku. Tunahitaji kiwanda cha kuku Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kuhusu ugonvi wa wafugaji na wakulima, sasa upate muafaka na uishe. Wafungaji wategewe maeneo ya kufugia, ili waache kuchungia kwenye mashamba; wanadumaza mashamba. Mashamba yanaharibika kwa sababu ya ng'ombe kupita humo kila siku. Kunakuwa na ugumu wa kulima kwa sababu ya mifugo kukanyaga humo kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida tuna Ziwa Kitangiri, tuna Maziwa mawili pale mjini; Ziwa Singida na Ziwa Kindai. Maziwa haya hayana samaki. Hivi jamani, si kuna kupandikiza samaki! Nakuomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wako,

wakague haya maziwa; Kitangiri, na Ziwa la Singida pale mjini, na Ziwa Kindai tupandikiziwe samaki ili vijana waweze kujiajiri katika maziwa haya, na wana-Singida waweze kupata kitoweo cha samaki, tuweze kuwapa na majirani zetu wa Mikoa inayotuzunguka kama Tabora, Manyara, Shinyanga na kwingine. Tunaweza tukalisha! Jamani, Tanzania hakuna umaskini. Mungu alitupendelea tukapewa kila aina ya rasilimali, ni sisi wenyewe ndio tunashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri tunaomba, wewe ni kijana mchapakazi, una Naibu Waziri mchapakazi, hebu pitia haya maziwa, fanya utafiti, weka Samaki pale, tayari vijana watakupenda, kwa sababu watajiajiri. *(Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, niongelee kuhusu machinjio ya kisasa. Katika Mikoa ambayo inafuga ng'ombe kwa wingi au mifugo kwa wingi ni pamoja na Singida, Singida ni Mkoa wa nne. Naomba sana jamani, tutengenezewe machinjio ya kisasa ili na sisi tuweze kula nyama ambazo zimekaa katika mazingira safi kuliko kuchinja ovyo ovyo, holela namna hii. Kama wenzetu hapa Dodoma wana machinjio ya kisasa, Singida kuna tatizo gani? Tunaomba tupewe machinjio ya kisasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli hizi, nimepokea tangazo la kuwepo kwa mechi ya Timu ya Bunge kesho. Sasa nimepokea tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, Mheshimiwa Iddi M. Azzan, anaomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote, wakiwemo wachezaji na washabiki wote wa timu zetu za Bunge, kwamba, kesho timu zote mbili zitakuwa na mchezo na *NSSF* wakifanya zoezi la kujiandaa na mechi zao.

Sasa wameniambia hapa, timu ya *football* ya Bunge, itaongozwa na mshambuliaji wao mahiri, Mheshimiwa *Capt*. John Komba, ataongoza timu ya *football*. Ameniambia hapa kwamba timu ya *netball* itaongozwa na *goal keeper* wao mahiri, ambaye ni Mheshimiwa Maria Hewa. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nami naungana mkono kabisa na Mheshimiwa Azzan kama hawa ndio wataongoza timu zetu kesho, na kama *Prof*. Maji Marefu amefanya mambo yake, basi nadhani mambo yatakuwa mazuri sana kesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Jumamosi saa 3.00 asubuhi ndani ya Ukumbi huu wa Bunge.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumamosi, Tarehe 1 Juni, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*